ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe

21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 22 Juni, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Uingizaji na Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Naomba kuwasilisha.

Nam. 92

Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Daladala Kijangwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar imekuwa na nia nzuri ya kuimarisha sekta ya usafiri wa umma Zanzibar na hivi karibuni kumeanza mpango wa kulifanya eneo la Kijangwani kuwa Kituo Kikuu cha Daladala. Hata hivyo, ni muda mrefu sasa tokea eneo hilo walipoondoshwa wafanyabiashara wa mbao halijaanza kutumika kama lilivyokusudiwa, huku wafanyabishara wa mbao wakiendelea kukosa riziki zao.

Je, mpango wa kuweka Kituo Kikuu cha Daladala Kijangwani (*stand*) utaanza lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi Mahiri, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Paje swali lake Nam. 92 naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imo katika hatua za kuimarisha na kupandisha hadhi miji ya mbali mbali hapa nchini ikiwemo Mji Mkuu wa Zanzibar uliopo Mkoa wa Mjini Magharibi. Katika kutekeleza dhamira hiyo njema ya Serikali, Ofisi imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana

na wahusika wengine wakiwemo Kamisheni ya Ardhi kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Usafirishaji na Leseni na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.

Mhe. Spika, Ushirikiano wa taasisi hizi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kazi ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi Mijini na Vijijini inafanywa kwa mujibu wa sheria kwa lengo la kuepusha migongano ya matumizi ya ardhi na mipango ya maendeleo iliyopo.

Mhe. Spika, hivi karibuni mnamo mwezi wa Febuari, 2017 Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi imepitisha Mpango Mkuu wa Matumizi Bora ya Ardhi yaani *(Master Plan)* ambapo eneo la ujenzi wa kituo cha daladala ni sehemu ya mpango. Sambamba na hilo Serikali imeridhia mpango mdogo wa Ng'ambo tuitakayo ambayo utabainisha wazi eneo la Mji wa Zanzibar yaani *(Zanzibar City Center)* kwa lengo la kuimarisha mvuto na haiba ya Mji wetu. Vilevile kwa mujibu wa Sheria ya Mipango miji na Vijiji ya mwaka 1955 na Kanuni zake, maombi ya upangaji wa maeneo yamewasilishwa katika Idara ya Mipango miji na Vijiji kwa hatua za kufaa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Kabla ya zoezi la kuwaondosha Wafanyabiashara wa eneo la Kijangwani kuchukuliwa, matayarisho makubwa yalifanyika ikiwemo kutafuta eneo mbadala. Matayarisho yaliyofanyika yalilenga kuwaondoshea usumbufu Wafanyabiashara kwa kuwapatia eneo muafaka na kuendeleza biashara zao. Hivyo suala kwamba zoezi lile limepelekea Wafanyabiashara hao kukosa riziki zao halipo.

Mhe. Spika, kufuatia taratibu nilizozieleza kazi zilizokamilika katika eneo hilo ni pamoja na kupeleka ombi la kupangwa kwa eneo husika, kufanya utafiti mdogo juu ya mwenendo wa daladala ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi na kuandaa michoro inayozunguka eneo la Kijangwani ambayo imekamilika. Kazi inayoendelea sasa ni kuandaa michoro ya kina *(Detail design)* kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho, kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mapema iwezekanavyo ili hatua zinazofuata ziweze kuanza kazi za ujenzi. Hivyo inatarajia kukamilika mapema iwezekanavyo naomba nirejee ili hatua zinazofuata zikiwemo za ujenzi ziweze kuanza.

Mhe. Spika, Kwa sasa Serikali kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Wilaya, Manispaa, UUB, Idara ya Usafirishaji na Leseni na wahusika wengine wanaendelea na hatua nyengine za kuandaa eneo hilo ili liweze kutumika kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo hatua hizo zilisita kutokana na kipindi cha mvua. Kwa kuwa hivi sasa hali ya hewa inaruhusu, kazi za matayarisho zitaendelea ili hatimae daladala zinazoegesha Michenzani ziweze kutumia eneo hilo la Kijangwani. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika kwanza kabla ya kuja kusahau naomba achukuwe salamu zangu kupelekea kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwa kazi aliyofanya katika Mwezi Mtufukufu wa Ramadhani kusimamia zoezi zima la watu wanaokula mchana.

Mhe. Naibu Waziri jee, kitachukuwa muda gani kituo hicho kukamilika na kipi kinafatia mwanzo katika kujenga mwanzo kabla kujenga ni mchoro au ramani. Tukishuhudia karibu

miaka miwili hivi sasa inakaribia kipi kinachofatia mwanzo kabla ya kujenga ni michoro au ramani na muda gani itachukuwa kukamilika kituo hicho.

Kwanini Serikali haijipangi mapema kabla ya maamuzi hivi sasa temuekuwa tukishuhudia mji wetu kukua kama Tunguu hakuna kituo cha daladala, Chukwani hakuna kituo cha daladala, Mbweni hakuna kituo cha daladala hebu utaratibu gani au *formula* gani mheshimiwa ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako namuomba Mhe. Mwakilishi swali la mwisho linalomalizia naomba alirejee.

Mhe. Spika: Lirejee swali la mwisho Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika ninachomuuliza kabla Serikali kupanga mipango yake kwanini haipangi mipango yake mwanzo baadaye kutokeza matatizo ndio wanapanga mipango yake, hivi sasa mji wetu umekuwa kwa kiasi kikubwa Chukwani, Mbweni,Tunguu gari zinasimama bila mpangilio. Kwa nini hakuna utaratibu wa kupanga vituo maalum na huu mji umekuwa hivi sasa muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Paje maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa naomba niseme kwamba kama ambavyo nimeleza awali katika eneo lile la Kijangwani na maeneo mengine muda ni mrefu ni kwamba umepita lakini muda huo ambao umepita ningeeleza sababu mbali mbali ambazo zimepelekea hali hiyo.

Moja nilieleza kwamba ni hali ya hewa lakini pamoja na hayo ni kucheleweshwa kuchelewa kidogo kutokana na kazi ambayo inafanywa na wataalamu, kwa hiyo kama ni sehemu ya utekelezaji sisemi kwamba hii tumechelewa iko katika utaratibu, kwa kuwa kazi ile ya eneo palikuwa na wafanya biashara inabidi lazima tupate utaratibu wa hatua moja badala ya hatua nyengine.

Hatua ya kwanza ambayo imefanyika ni kuwaondosha wafanyabiashara, hatua ya pili ni Kamati pia ya Wataalamu ili kufanya kazi yao ya kitaalamu kwa sababu kama tunavyosema kutokana na hali halisi ya mrundikano na hivyo vituo ambavyo kwa kweli vya msongomano wa magari na kuelekea mji wetu unataka kuujengea hadhi zaidi na ulete kuvutia zaidi, sasa imepelekea kwamba tuwape kazi hiyo muwe na wataalamu ambao wanaifanya kwa kina kabisa na kwa umakini mkubwa ili baadaye ifike siku tuje tufarahiye kile ambacho kazi ya utalaamu ambayo inafanywa. Kwa hiyo nimuombe Mhe. Mwakilishi kutokana na hali hiyo kwamba aelewe bado hatujachelewa tuko katika hatua kama vile ambavyo nimesema awali.

Lakini kuhusu ni lini kama kazi hiyo itakamilika nimesema mheshimiwa hapa kuna kazi nyengine zinafanyika kwa hiyo pale ambapo watakamilisha kwa sababu hili jambo linafanywa la kitaalamu ni mapema mno Mhe. Mwakilishi kumwambia kwamba tutamaliza kesho, kwa sababu inawezekana pengine utalamu bado kuna mambo mengine kuna hatua nyengine zinahitajika

zipite. Kwa hiyo Mhe. Mwakilishi nimuombe tuu kwamba awe na subira, dhamira ya Serikali ni njema na naamini kazi ambayo inafanywa ni kazi nzuri na mwisho wa siku tutakuja kuifurahia sote kwa pamoja, Serikali haina lengo la kuwakomoa wananchi.

Lakini swali jengine la mwisho ambao mheshimiwa alitaka kuona kwamba kuangalia uwezekano wa kuweka vituo vyengine katika maeneo yetu ya mjini kama vile ambavyo ameanisha maneo ya Tunguu na maeneo mengine katika kuangalia vituo. Kazi hii pia niseme kwamba ushauri huo ambao ameuelezea au mapendekezo hayo aliyoelekeza ni kazi ambayo sasa hivi katika mpango mbali mbali kama nilivyosema Mkoa wa Mjini Magharibi sasa hivi umeandaa *Master Plan* kwa ajili kwamba kuainisha eneo lipi lifanyike shughuli gani na eneo lipi halitofaa kwa shughuli gani. Kwa hiyo niombe tuu kwamba yote hayo yataenda sambamba na naamini mipango hii itakapokamilika nadhani kila kitu kitakaa sawa, naomba tuwe na subra waheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu ijapokuwa marefu sana lakini tumeelewa kwa hiyo tumechukuwa yake ambayo tunayahitaji, lakini ameonesha wazi kuwa katika jambo hili hakuna *work plan* ambayo itaonysha hata ile *time frame* tunamshukuru hasa kwa majibu ambayo ametuelekeza kabisa.

Naomba sasa niuulize swala kama ifuatavyo kwa kuwa utekelezaji huu baada ya zile taasisi tatu kuzieleza kwa Mkuu wa Mkoa, UUB pamoja na Manispaa najua wazi kwamba utekekeleza huu mpango wake unatakiwa uidhinishwe na Baraza la Manispaa mjini.

a) Jee hadi hivi sasa wakati hatua hizo zinaendelea huu mpango wa utekelezaji umepitishwa na kupata aidhini katika Baraza la Manispaa ya Mjini.

b) Ujenzi huu baada ya kukamilika na kwasababu alizitaja zile hatua tatu alizitaja taasisi tatu nani ambaye atakuwa ni mmiliki katika kulisimamia na kuendesha hii *parking*. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Miraji Khamis Mussa Mwakilishi Makini wa Jimbo la Chumbuni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa kuhusu *work plan* ambayo mheshimiwa amesema kwamba kutokana na maelezo ambayo nimeyatoa kuwa na wasiwasi kwamba labda hakuna *work plan*. Mheshimiwa nikwambie *work plan* zipo na kubwa zaidi ni kwamba kuna mambo mengi ambayo sasa hivi ni mapema mno mimi kuyazungumzia kwa sababu kazi hii ina wataalamu, kwa vile kazi ina wataalamu niseme tu kwamba kwa kupitia majibu haya tuseme kuna kazi moja ambayo ilikuwa Wizara tunapaswa tuiifanye lakini naamini tutaifanya karibuni angalau yakuweza kutoa *presentation* kujua Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kujua ni kitu gani ambacho kinaendelea.

Lakini naomba kwa hilo tuvute subira lakini nyote ni mambo ambayo kwa kweli tayari tunayo na yameshamilika, yale ambayo kwa kweli yanahitajika yakamilike mapema. Lakini kuhusu mpango huu Mhe. Mwakilishi niseme kazi hii ni maagizo au ni kazi ambazo Serikali imeridhia kama imeridhia ni kwamba sisi Baraza la Manispaa na watalamu wengine hiyo *team* ya watalaamu ambayo nimeizungumzia imekuwa *include* na pia na Baraza la Manispaa. Kwa

maana hiyo niseme kwamba kazi hii tunaifanya kwa pamoja na *team* nyengine ya watalaamu au taasisi nyengine ambazo nimezitaja tuko pamoja tunaenda bega kwa bega na hakuna kitu ambacho kwa kweli labda sisi kwa upande wetu tume-*miss,* na kwetu tunalifanya na taasisi nyengine wanafanya lile ambalo ni la kwao.

Lakini baada ya kukamilika mpango huu Mhe. Spika naomba nimjibu mheshimiwa usimamizi katika eneo lile bado kwa hadi sasa hivi kama vile sheria na kanuni zilizopo za Manispaa kwa hiyo ni vile vile kwamba usimamizi baada ya kukamilika kama hakutatokea mabadiliko mengine basi tutangalia sheria zilizopo na kanuni zile za manispaa zetu na naamini kwamba utaratibu wa usimamizi utakuwepo pale pale kwa manufaa kama vile maeneo mengine.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hili swali limechukuwa muda mrefu sana na ndio kwanza swali la mwanzo kwa hiyo tunaendelea.

Nam. 177

Wakuu wa Wizara Kutembelea Skuli na Taasisi Za Elimu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwa na changamoto nyingi kwenye skuli zetu Unguja na Pemba ambazo nyengine Uongozi wa Wizara hauzijuwi kwa vile hawafiki kwenye maeneo yenye changamoto hizo kama inavyopasa.

Je, Uongozi wa Wizara umejipanga vipi kuhakikisha wanapita kila mara kujuwa matatizo ya skuli na taasisi za elimu Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 177 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kutoa maelezo ya utangulizi. Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanafanya ziara za kutembelea skuli zetu mara kwa mara na kukutana na walimu wakuu, walimu na wajumbe wa Kamati za Skuli na masheha na hata wakati mwengine na wanafunzi kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya skuli na kuweza kufahamu matatizo mbali mbali yanazozikabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Hatua zinazochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kufuatilia matatizo na changamoto zilizoko skuli ni kama ifuatavyo:-

i. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanzisha Ukaguzi wa Kanda ambapo Ofisi za ukaguzi huo zitakuwepo katika kila Mkoa. Hii itasaidia kuzifikia skuli zilizomo katika Mikoa hiyo kwa urahisi na kwa wingi zaidi kulinganisha na utaratibu wa sasa ambapo wakaguzi wote lazima watoke Makao Makuu mjini kufuatilia skuli katika maeneo ya vijijini.

ii. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka huu wa fedha wa 2017/18 itaongeza idadi ya wakaguzi 18 kwa lengo la kukagua skuli nyingi zaidi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji

iii. Kuwashirikisha Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, kwani wao wapo karibu na maeneo ya skuli na hivyo kuanza kulitatua baadhi ya changamoto zilizopo katika skuli na pale ambapo zitawashinda basi huliwasilisha Wizarani kwa utatuzi.

iv. Wizara kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na uongozi wa skuli na hivyo uongozi wa skuli huwasilisha matatizo ya skuli hasa ya dharura kwa Wizara kwa ajili ya hatua za haraka.

v. Watendaji wakuu waliopo wizarani wana utaratibu wa kuzitembelea skuli mara kwa mara kwa lengo la kuona na kuzungumzia changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi.

Chengine ni ziara za mara kwa mara za Waziri na Naibu Waziri kukutana na wadau mbali mbali wa elimu katika skuli, Wilaya na Mikoa. Nyingine ni mawasiliano mazuri yaliyopo baina ya viongozi wa wizara na viongozi wengine wa majimbo, masheha na hata wa Wilaya na Mikoa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni uhusiano mzuri uliopo kwa wananchi ambao mara kwa mara hutuletea taarifa ambazo zinatusaidia kutatua matatizo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya serikali naomba kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza, na hili la mwisho naomba alifikirie maana yake itakuwa mara ya tatu tena kama muungwana atakuwa muungwana kweli.

a) Ukaguzi huo wa kanda au Mkoa kwa mwaka mnafanya mara ngapi.

b) Kwa nini skuli zangu za Bwejuu na Mtule na nimekwambia mara tatu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani kwamba kuna tatizo la choo na ukaambiwa kuna pesa za mfuko wa Bunge, hizo pesa za mfuko wa Bunge mpaka leo hata zikafika nafikiri zinatambaa hazijafika mpaka muda huu. Lini utaenda kukijenga choo kile, hivi sasa Bwejuu kuna matatizo ya maji, *pump* imeharibika, Michamvi napeleka magari ya maji na hii si kazi ya mwakilishi ni kazi ya serikali wamenichagua kuja kuwaelezea matatizo yao. Ni lini utakwenda kukijenga choo kile kama Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza. Tunaposema kwamba tutaanzisha kanda hizi za ukaguzi, hizi maana yake kwamba huduma ya ukaguzi inasogezwa karibu na skuli na kwa maana hiyo katika utaratibu wa ukaguzi nnazo kaguzi za aina tatu. Kuna kaguzi maalum, kuna kaguzi za ziara na kuna kaguzi nyengine ambayo tunaita katasisi. Hizi kila moja inafanywa kwa madhumuni yake.

Kwa mfano, ukaguzi wa dharura linapotokea jambo fulani tunataka kujua taarifa zake zaidi tunapeleka wakaguzi kufanya ukaguzi huo, na kuna ukaguzi mwengine wa kawaida. Sasa tunachosema kwamba tunaongeza wakaguzi, tunaongeza huduma za ukaguzi ili skuli ziweze

kukaguliwa mara kwa mara. Niseme tu ukaguzi huu ni nyongeza ya ukaguzi kwa sababu tayari waliku wakuu tumeshaelekeza kwamba na wao pia watakuwa wakaguzi katika skuli zao.

Pili, tumekuwa tukilijibu swali hili na tutaendelea kulijibu swali la vyoo huko Bwejuu. Tumesema kwamba katika kutoa huduma za elimu wako viongozi kama wawakilishi hujitolea kusaidia, wapo wabunge hujitolea kusaidia na tumeshasema mbunge wa sehemu ile ameahidi kwamba atafanya kazi hiyo. Kwa hivyo, siku yoyote ambayo atamaliza hatuna sababu ya kutomuamini kiongozi mwenzetu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ni kweli jitihada tunaifanya kupitia pesa za mifuko ya jimbo na zetu sisi wenyewe lakini katika changamoto zinazoikabili skuli ni uchakavu na ubovu wa majengo. Katika jimbo langu skuli ya Kwale kuna jengo lenye vyumba vinne na ofisi ya Mwalimu Mkuu, jengo lile ni bovu na linahatarisha maisha ya wanafunzi wetu waliopo pale, na wizara yako wanalijua hili.

Je, ni lini jengo lile mtalivunja ili kunusuru maisha ya wanafunzi waliopo pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza. Ni kwamba Wizara ya Elimu inajaribu kuyapitia majengo yake mbali mbali, na yale ambayo itadhihirika kwamba yako katika hali ya kuhatarisha maisha ya wanafunzi na wapita njia majengo hayo huwa tunayabomoa. Tumeshafanya kama hivyo skuli ya Mkanyageni/Bogoa, tumeshafanya hivyo Michenzani na tumeshafanya sehemu hizo Wambaa na skuli yako kama iko hali hiyo baada ya kupeleka wataalamu wetu wa Wizara ya Elimu itabomolewa mara moja.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya utatuzi wa changamoto kupitia maskuli yetu, lakini Mhe. Naibu Waziri kama unakumbuka uliwahi kukiri uwepo wa changamoto wa skuli ya Kiwengwa Kairo na ukaeleza mengi. Sasa leo naomba kukuliza maswali ya changamoto ya uvamizi wa eneo la ardhi katika eneo lile.

a) Ni hatua gani za utekelezaji zilizofikiwa hadi sasa katika kutatua tatizo lile la Kiwengwa Kairo.

b) Wananchi unawaahidi nini katika kulimaliza tatizo lile haraka iwezekanavyo ili skuli iendelee na ujenzi wake kama hatua za wananchi wanavyojipanga katika eneo lile la Kiwengwa Kairo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Serikali imeunda kamati ambayo wajumbe wake niko mimi kutoka Wizara ya Elimu, kutoka Wizara ya Ardhi na kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili suala hilo tunalifuatilia na tutakapolipatia ufumbuzi basi tutalieleza. Kwa hivyo, wananchi tunawaahidi kwamba watulie wawe na subra na suala hilo linafanyiwa kazi.

Nam. 131

Uzinduzi wa Baraza ya Watoto ya Shehia

Mhe. Shaib Said Ali (Kny: Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza:

Kwa kuwa wizara ilipanga kuimarisha mabaraza ya watoto kwa kila shehia na kulipia pensheni za wazee.

(a) Je, mwaka 2016/2017 zilitumika kiasi gani cha fedha kwa ajili ya uzinduzi wa mabaraza mapya ya watoto ya shehia.

(b) Je, kuna mabaraza mangapi ya watoto yaliyoanzishwa katika Jimbo la Konde au Wilaya yoyote ya Micheweni.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kunipa pumzi zake na asubuhi hii nikaweza kusimama katika Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 131 la lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli wizara yangu ilipanga kuimarisha Mabaraza ya Watoto ya Shehia za Unguja na Pemba kwa kuyakagua na kuwapatia mafunzo ya uendeshaji wa mabaraza ili kuimarisha ushiriki wa watoto katika mambo yanayowahusu ikiwa ni pamoja na kutoa maoni yao, kushiriki na kushirikishwa katika mipango ya kifamilia na kitaifa. Pia fursa za kujifunza pamoja na masuala mengine ya hifadhi ya mtoto kama vile kuripoti viashiria na matukio ya udhalilishaji wa watoto.

(a) Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hakuna kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya uzinduzi wa mabaraza mapya ya watoto ya shehia. Wizara imeweza kutumia shilingi milioni mbili, laki tano na tisini elfu (2,590,000/-) kwa ajili ya kuyapatia mafunzo mabaraza mapya na yaliyokwisha kuundwa katika shehia.

Aidha, wizara kwa kushirikiana na "*Save the Children*" inaendelea kutoa elimu ya kujenga uwezo wa mabaraza ya watoto katika kila Wilaya zote Unguja na Pemba kwa kuwapa muongozo wa mabaraza ya watoto pamoja na kufanya uchaguzi wa mabaraza ya watoto ngazi ya Wilaya.

(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu na muongozo wa uundaji na uanzishwaji wa mabaraza ya watoto ni kwamba kila shehia inatakiwa kuwa na baraza moja la watoto ambalo linatakiwa kuundwa na watu wasiozidi 30. Hivyo, Jimbo la Konde kuna Mabaraza ya Watoto saba (7) yaliyoanzishwa kwa kufuatana na idadi ya Shehia zilizopo

katika Jimbo la Konde. Aidha, Wilaya ya Micheweni ina jumla ya mabaraza ya watoto 25 kufuatana na idadi ya shehia zilizoko katika Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kushirikiana na wizara yangu katika kuyasaidia Mabaraza hayo kutimiza wajibu wake na haki za msingi. Pia wazazi na walezi kuwa karibu na mabaraza kwa kuyatembelea na kutoa ushauri juu ya mambo ya msingi kwa mujibu wa taratibu za nchi yetu na muongozo wa uendeshaji wa mabaraza ya watoto.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa sababu mabaraza haya bado ni machanga je kutoyapatia fedha mabaraza haya huoni kuwa ni kuyarudisha nyuma kimaendeleo na majukumu waliyojipangia.

b) Kwa kuwa swali langu lilikuwa na pensheni ya wazee je ni wazee wangapi mpaka hivi sasa wamepata pensheni hiyo, na wale ambao hawajapata kuna utaratibu gani wa kuwapatia pensheni hiyo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Spika, kutowapa ruzuku mabaraza ya watoto si kwamba tunawavunjia sisi, bali wizara iko karibu sana na mabaraza haya na inawapa misaada kwa kila wakati na pale inapoona wanahitajika basi wizara yangu haisiti kuyasaidia mabaraza haya, tukiamini kwamba sisi ndio walezi wa mabaraza haya ya watoto.

Mhe. Spika, swali lake la (b) naomba alirejee kidogo.

Mhe. Spika: Mhe. Shaib Said Ali lirejee swali la (b).

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Spika, katika swali lake aliuliza kwamba pensheni ya wazee lakini sikulisikia jibu lake. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri je ni wazee wangapi na ni kiasi gani cha pensheni ambacho kimetolewa mpaka hivi sasa, na wale ambao hawajapata pensheni hiyo kuna utaratibu gani wa kuwapatia na wameshafika kiwango hicho. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mpaka hivi sasa kutokana na pesa iliyotumika kwa ajili ya kuwalipa wazee hawa kuanzia Julai, 2016 mpaka Mei, 2017 ni shilingi bilioni 5,220,966,500. Wazee ambao hawajapata kulipwa pensheni hakuna mzee ambaye amefikia wakati wa kulipwa na wakati taarifa zake tunazo wizarani akawa hajalipwa, hakuna mzee huyo, isipokuwa nitoe wito kwa wananchi wale ambao wana wazee na wana uhakika kwamba wazee wao tayari wameshafikia umri wa kulipwa pensheni basi wafuate utaratibu wa kuorodhesha wazee wale. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini napenda nimuulize swali moja lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa wizara ilipanga kuimarisha mabaraza ya watoto ndani ya shehia je ni taratibu gani ambazo zilitumika kuhakikisha haya mabaraza kwa kila shehia yanafanyika.

b) Na ni shehia ngapi ambazo zina mabaraza haya ya watoto na zinajuulikana kwa Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Utaratibu wa uundwaji wa mabaraza haya napenda kumuelezea Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu huu unaanzwa na viongozi wa majimbo na baadae sisi wizara tunafatilia na tukaona pale wale viongozi wa majimbo walipounda na sisi kuweza kuyasaidia mabaraza yale.

Lakini kama alivyouliza swali lake la (b) kwamba ni mabaraza mangapi ambayo yanajuulikana kwa Unguja na Pemba naomba kumjibu kwamba mabaraza yanayojuulikana kwa Unguja na Pemba ni mabaraza 384.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona kuweza kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Lakini kabla nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha yaliyotangulia.

Mhe. Spika, katika suala zima la mabaraza ya watoto Naibu Waziri amejibu kwamba wameweza kuwasaidia fedha ambazo wamezitaja wastani wa shilingi milioni mbili ni jambo la kushukuru na ametuomba sisi wawakilishi vile vile tusaidie na tuko tayari kumpa *support* juu ya mabaraza haya.

Mhe. Spika, je fedha hizi ambazo zimetolewa kwa ajili ya kusaidia mabaraza ya watoto walizitoa katika fungu gani, kwa sababu hazikuwa katika bajeti ambayo ilipita. Lakini na katika bajeti hii ambayo tumeipitisha hatukuona fungu linalogharamia mabaraza ya watoto, tuliyoona ni mabaraza ya vijana. Je, watazipata wapi fedha kwa ajili yak u-*support* mabaraza haya katika mwaka huu wa fedha. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake analotaka kujua kwamba fedha hizi ambazo zilitumika kwa ajili ya kuwasaidia mabaraza ya vijana tulizitoa wapi. Kwa hiyo, naomba Mhe. Mwakilishi swali lake hili niweze kumjibu kwa maandishi ili tuone pesa zile zilitoka katika fungu gani.

Nam. 75

Ahadi ya Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na ahadi ya ujenzi wa soko kubwa la samaki la Malindi na mpaka hivi sasa hakuna dalili za ujenzi wa soko hilo ambao ilielezwa kuwa ujenzi huo utafadhiliwa na washirika wa maendeleo wa Japan.

Je, ahadi ya ujenzi wa soko hilo imekwama wapi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu eneo la Mji Mkongwe ni eneo la Hifadhi ya Maendeleo ya Mji Mkongwe kwa maana ya kuwa lipo kwenye urithi wa duania na pindipo unapohitaji kujenga ndani ya eneo hilo ni lazima upate kibali maalum kupitia Hifadhi ya Maendeleo ya Mji Mkongwe kwa makubaliano na *UNESCO*. Kwa hivyo, kuchelewa kupatikana kwa kibali cha ujenzi wa soko mwaka 2014 ni moja ya sababu iliyopelekea kuchelewa kuanza kwa ujenzi huo mwaka 2016 bahati nzuri mwaka huo 2016 tayari kibali hicho kimeshapatikana.

Mhe. Spika, kuchelewa kupata kibali cha *UNESCO* kumepelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi kutokana na kupanda kwa thamani ya dola ambapo awali gharama ya ujenzi zilikuwa jumla ya dola za Kimarekani 9,292,176 kwa mwaka 2015. Kufikia mwaka 2017 fedha kwa ajili ya ujenzi zimeongezeka na kufikia jumla ya dola za Kimarekani 11,523,200 ambazo zilikuwa na tofauti ya kasoro ya dola za Kimarekani 2,321,024.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Japan kufikia mwezi Machi mwaka 2017 zilikubaliana kama ifuatavyo:-

i) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachangia jumla ya dola za Kimarekani 1,616,092.

ii) Serikali ya Japan inakadiriwa itaongeza jumla ya dola za Kimarekani 614,932 ambapo kwa pamoja na makubaliano ya awali yatafanya jumla yote ni 9,907,108.

Mhe. Spika, hizi ndio sababu kuu zilizosababisha ucheleweshaji wa ujenzi wa soko la Malindi. Aidha, ujenzi huo sasa unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2017.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha sana tena sana na kutokuwa na afya, Baraza lilopita wakati huo wizara hii inaongozwa na Mhe. Said Ali Mbarouk iliahidi ndani ya chombo hiki na *hansard* tukienda tutazikuta kuwa ujenzi huo utaanza mara moja, mwaka wa nne karibu sasa hivi. Hebu Mhe. Waziri tufahamishe na wananchi wapate kufahamu hicho kibali kimetoka mwaka gani, siku gani na tarehe gani.

La pili, kuna taarifa kuwa soko hilo lilikuwa lijengwe Kilimani tokea Awamu ya Sita na baadae pesa hizo zikaondoka zikenda kujengewa Kirumba, Mwanza. Hebu tuelezwe sababu gani za msingi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Kibali kimepatikana mwaka 2016 kama nilivyosema na mwaka huu 2017 tayari tumeshaanza. Nataka nimthibitishie tu Mheshimiwa kwamba ujenzi utakamilika na hivi sasa michoro imeshafanywa na hii hapa ndio ramani ya jengo litakalojengwa, nategemea wakati wowote litajengwa. *(Makofi)*

Hii habari ya Kilimani ndio kwanza naisikia hapa na kumbukumbu zote nilizozisoma mimi ni kwamba soko linajengwa pale Malindi, hii ya Kilimani ndio kwanza namsikia yeye na sijawahi kuona pahala popote.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mwanana sana ya utekelezaji wa mradi huu na niipongeze sana serikali. Kwa kuwa alisema mwezi Agosti tunategemea kuanza kwa ujenzi huu na mara nyingi ujenzi huwa tunawatafuta ma-*contractor* katika kuingia nao mikataba ili kuelekea kwenye ujenzi huo. Kuna utaratibu gani uliotumika wa kuwatafuta *contractor* hadi sasa ukizingatia kuwa kiutaratibu wa tender unachukua miezi mitatu, upungufu wake siku 40. Sasa kuna utaratibu gani wa kumpata huyo *contractor* wa kukabiliana na hiyo tarehe aliyoitoa kwa mwezi wa Agosti.

Pili, ujenzi huu alitaja gharama ambazo serikali mbili zitachangia ya Japan na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utaratibu wake, pesa hizi kwa mwezi wa Agosti zitatumika katika kifungu gani ambacho hatukukiona kwenye bajeti yake aliyoipitisha katika mwaka huu wa fedha. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. *Contractor* kwa mujibu wa makubaliano yetu na Serikali ya Japani kwanza lazima kampuni itoke Japani kwa sababu wao ndio *main fundax* katika hili na ndio maana *contractor* wa kwanza kuchora hii niliyoionesha sasa hivi vile vile alitokea Japani. Tumekaa nao, tumeshazungumza nao hata juzi tulikuwa na kikao nao, wametuahidi kabisa *tender system* yao na utaratibu wao mwezi wa Agosti tayari ujenzi utakuwa umeanza. Kwa hivyo, hili nataka kumhakikishia kabisa *tender system* inayofuata tunategemea sheria ile ya *procurement* ya Kijapani pamoja na ya kwetu kwa kiasi fulani; lakini zaidi wao ndio wafadhili wakubwa na wajengaji wanatoka katika nchi yao. Huo ndio utaratibu ambao unatumika.

Kuhusu kwamba hakuna fedha za mradi huu, nafikiri labda tuangalie tena kwenye bajeti yetu, ziko fedha ambazo kwa upande wetu sisi tumechanga na iko *foreign component* ambayo inatoka Serikali ya Japani, tumeonesha kwenye bajeti yetu na mimi nitampatia takwimu sahihi kumuonesha kwenye bajeti yetu kwamba fedha hizi zipo.

Nam. 133

Kuanza Kazi kwa Kituo cha Kuzalisha Samaki cha Beit-el-Ras

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali imejenga kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki kilichopo Beit el–Ras kwa lengo la kuwanufaisha wananchi wetu na kuwaongezea kipato, sambamba na kupunguza tatizo la upungufu wa samaki hapa Zanzibar.

(a) Je, kituo hicho cha kuzalisha vifaranga vya samaki kimeshaanza kuzalisha vifaranga hivyo kama ilivyotegemewa, kama bado ni lini kituo hicho kitaanza kazi za uzalishaji ili wananchi wetu waanze kunufaika na mradi huo.

(b) Kama uzalishaji umeanza, ni wananchi wangapi na maeneo gani ambao wamepatiwa vifaranga hivyo sambamba na kupatiwa elimu ya kutosha kuhusiana na ufugaji wa samaki.

(c) Kama mpango huo umeanza na kuonesha mafanikio. Je, serikali haioni kwamba ipo haja ya kupiga marufuku uingizwaji wa samaki kutoka nje ili kumlinda mvuvi na mfugaji wa samaki wa hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 133 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kituo cha uzalishaji vifaranga vya samaki huko *Beit-el-Ras* hakijamalizika kujengwa, katika hatua za ujenzi kituo hicho kimeanza kwa kazi ya kujenga uzio (*fence*) ambapo umekamilika na uchimbaji wa kisima cha maji ya chumvi tayari umekamilika. Mapipa 26 kwa ajili ya uzalishaji vifaranga vya samaki tayari yameshafikishwa *Beit-el-Ras* pamoja na vifaa vya uchunguzi wa maabara, sambamba na *transformer* moja ambayo tayari imeshafungwa.

Mhe. Spika, mchakato wa kumpata mkandarasi wa kupitia michoro na usimamizi wa ujenzi rasmi umekamilika, ujenzi rasmi utaanza mara baada ya kupatikana mkandarasi wa ujenzi wa kituo hicho. Ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu 2017. Hivyo utakuwa ndani ya muda uliopangwa.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Kituo cha kuzalisha viranga vya samaki hakijaanza kuzalisha vifaranga hivyo kwa sasa, kipo katika hatua ya ujenzi na kinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2017. Kituo hicho kinatarajiwa kuanza kazi ya uzalishaji hapo mwakani 2018 mara baada ya kumalizika.

(b) Uzalishaji wa vifaranga vya samaki kwa sasa haujaanza. Aidha, serikali inaendelea kuwapatia elimu zaidi wafugaji wazalishe kwa ufanisi.

(c) Mpango wa uzalishaji vifaranga vya samaki kwa sasa haujaanza, mpango huu utakapoanza na uzalishaji wa samaki utapofikia kiwango cha kutosheleza mahitaji ya

samaki nchini, serikali italifanyia kazi suala la kuzingatia kwa kuingiza samaki nchini ili kumlinda mvuvi na mfugaji wa samaki hapa nchini.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Waziri kwa kuwa anasema bado uzalishaji wa vitoto hivi vya samaki haujaanza.

(a) Je, ana utaratibu gani wa kuwapatia wavuvi hao vifaranga hivyo ambao tayari sasa wameshaandaa mabwawa yao ya kutilia samaki hao.

(b) Je, mradi huo utakapomalizika utagharimu shilingi ngapi mpaka kumalizika kwake. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, la pili sikulisikia.

Mhe. Spika: Swali la pili halikusikika vizuri.

Mhe. Shaib Said Ali: Ni kiasi gani cha gharama kitakachotumika mpaka mradi huo kumalizika.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza maandalizi ambayo tumeyafanya Mheshimiwa ni kuwapatia wafugaji wetu taaluma na kazi hiyo nasema imefanyika kwa ufanisi sana. Kwanza tumeweza kujua kiwango cha samaki wanaotakiwa kwa mfano Pemba wanahitaji samaki kama vifaranga milioni mbili, hapa Zanzibar laki saba kwa sababu Pemba wana mabwawa mengi sana ya kufuga samaki. Pili, hatua ya pili iliyochukuliwa ni hivi vifaranga ambavyo vinapatikana sasa hivi ndani ya bahari yetu kuvichukua na kuvisarifu ili kuangalia vina ubora gani, ili tuweze kuzalisha samaki ambao wanahitajika katika soko. Tatu, ni kuwasaidia kujua masoko hawa samaki tutakaozalisha je soko lake liko wapi na wapi. Hizo ni hatua ambazo tumechukua katika kuwaeleza watu wetu.

Pale Beit-el-Ras kulikuwa na kituo kidogo chini ya *SUZA*, kile kituo tumeweza kukiendeleza sasa hivi tunafuga kaa, jongoo na samaki kidogo kuwapa taaluma watu wetu namna gani tunaweza kufuga kwa kutumia taaluma hii ya ufugaji. Kwa hivyo, maandalizi hayo yamefanyika na yanaendelea na mafunzo mbali mbali yanafanyika.

Juzi tulikuwa na timu ya Wachina wamewapa *training* vijana wetu kama 50 namna gani ya kuweza kufuga samaki kwenye mabwawa ya samaki. Kwa hiyo, kazi imefanyika, mradi huu uta-*cost* kama US$ 3,000,000 Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze wizara kupitia serikali yetu kwamba ina mpango mzuri wa kuwaendeleza wananchi wetu na kujitafutia riziki zao kutoka na kufuga samaki hao, ambapo itakuwa ni utoshelezaji mzima wa kupatikana samaki katika nchi yetu.

Lakini swali langu liko hapa, kwa asilimia mia moja Zanzibar imezungukwa na bahari, lakini bahati nzuri kuna wengine wanaishi kama vijijini sehemu za mashamba. Je, wizara ina mpango

gani au itafanya nini kuhakikisha kwamba wanaoishi baharini wanafuga samaki wa maji ya bahari na wanaoishi juu katika sehemu za mashamba wanafuga samaki katika maji baridi. Wana mpango gani katika mbegu hizo au vifaranga hivyo vya aina mbili hizo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake kama ifuatavyo. Kwanza samaki ambao tunawazalisha sasa hivi ni wa maji ya baharini sio maji baridi. Hata sasa hivi mabwawa yote utakayotembelea ni yale ambayo yanaingia maji ya chumvi hakuna mabwawa ambayo yana maji baridi peke yake, yako mengine yanachanganyika kwa kiasi fulani na maji baridi lakini samaki hasa tunaofuga ni wa maji ya chumvi. Kwa hivyo, hiyo ndio taaluma tunayoitoa na haya ndio mabwawa tutakayoendeleza kuyafugia samaki.

Mhe. Hamida Abdallah Issa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vitoto (a) na (b).

(a) Ni wakandarasi gani ambao walikwenda kuomba maombi hayo na ni nani alishinda katika *tender* ya ujenzi huo.

(b) Utaratibu gani ulitumika katika kumpata mkandarasi huyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi kwamba suala la kuteuliwa mkandarasi bado tuko kwenye *process* na haijakamilika. Kwa hivyo, siwezi kujua ni mkandarasi gani aliyechaguliwa. Mkandarasi atatangazwa rasmi kwenye magazeti, lakini nasema serikali mara nyingi ile nchi ambayo inatoa fedha ndio mkandarasi anatoka katika nchi hiyo. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi haijatangazwa.

Mhe. Spika, kuhusu utaratibu ni huo niliosema Mhe. Spika.

Nam. 80

Uhaba wa Vituo vya Kuuzia Umeme wa TUKUZA

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Pamoja na bei ya umeme kupanda na kuwaumiza wananchi, bado kumekuwa na usumbufu kwa wananchi hao wanaokwenda kununua umeme kwa vile vituo vya ununuzi ni vichache na vyengine vimefungwa kabla ya wakati kama vile kituo cha Malindi na Gulioni na kunakuwa na msongamano mkubwa wa foleni kwenye vituo hivyo vichache vinavyobakia.

(a) Serikali haioni haja ya kuja na mkakati mpya wa kuuza umeme kwenye vituo vya mafuta kama wanavyofanya wenzetu wa nchi jirani.

(b) Serikali haioni ni vyema sasa ikatafuta mtu au kampuni binafsi ikasimamia huduma za kuuza umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ili kutanua wigo wa utoaji huduma za mauzo ya umeme kwa wananchi, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme imo katika ukamilishaji wa mpango wa uuzaji umeme kwa kutumia makampuni binafsi yatakayofungua vituo vidogo vidogo vya kuuzia umeme karibu na maeneo ya wananchi. Mpango huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa 2017.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mafupi ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo sana ya nyongeza. Sababu gani za msingi zilizopelekea vituo hivyo kama Malindi, Gulioni na ndio kituo kikuu cha kuuzia umeme pale ndio *head office* hasa, nasema kufungwa kabla ya wakati. Mimi mwenyewe ni shahidi.

La pili, haoni ipo haja ya kuajiri wafanyakazi wenye imani nyengine kwa hivi sasa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani baada ya kufunga vituo hivyo saa nane na nusu mchana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, naomba arudie la pili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, katika Mwezi Mtukufu huu wa Ramadhani vituo vinafungwa saa nane na nusu mchana, haoni ipo haja ya kuawaajiri watu wenye imani nyengine ili kuendelea na kazi kama utaratibu wa mwanzo ulivyokuwepo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ahsante kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Nianze na swali la pili, leo tuko mwezi 27 Ramadhani, ushauri huu labda ungekuja mapema ingekuwa ni wakati muwafaka, lakini sasa na kwa vile tuna mpango tunasema ndani ya mwaka 2017 juu ya makampuni *Inshaallah* usumbufu huo ambao anahisi umetokea hautotokea tena kwa sababu ndio hivyo Ramadhani inamalizika.

La kwanza kwa nini imefanywa hivyo. Taarifa hii sina na niseme nimeichukua kama vinafungwa mapema na marekebisho yatafanyika *Inshaallah*.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kutokana na umuhimu wa huduma hii ya umeme haoni kwamba ipo haja sasa kuanzisha utaratibu kama *ATM* mtu anakwenda ananunua mwenyewe na kuacha utaratibu wa mpaka akalipe na vituo kufunguliwa kwa muda tu ambao unaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi. Haoni ipo haja kuanzisha *system* kama *ATM*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ipo haja serikali inaona hivyo na ndio maana nilipokuwa nimesema kwamba mpango huu unategemewa kuanza mwaka huu 2017 unahusisha pia moja katika kampuni ambayo tunaingia nayo ni *PBZ* ambapo mwenye

account ya *PBZ* anaweza akanunua umeme kwa kupitia *ATM* halikadhalika kupigia simu, lakini pia mpaka kwenye vituo vya mafuta utaanza kununuliwa umeme. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza niipongeze sana serikali kwa kutoa huduma nzuri za umeme kwa wananchi wake, lakini swali langu liko hapa. Katika Mkoa wa Mjini Magharibi tuna wilaya tatu, tuna Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi 'A' na Wilaya ya Magharibi 'B'. Hizi wilaya mbili za mjini zina vituo kama vitatu vya kununulia umeme ikiwemo Michenzani, Gulioni na Malindi; na Wilaya ya Magharibi 'B' wana vituo viwili, kituo cha Mazizini na Mwanakwerekwe; lakini Wilaya ya Magharibi 'A' haina kituo chochote cha kununulia umeme.

Je ni lini serikali kupitia Shirika la Umeme itaanzisha kituo cha kununulia umeme kwa wilaya mpya ya Magharibi 'A'.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni baada ya kuanza huu mpango kama nilivyokuwa nimesema hakutakuwa na wilaya ambayo imeachwa nyuma katika wilaya ambazo amezitaja. Kwa sababu mote humo muha *petrol station* lakini pia mna watu ambao wana *account*. Kwa hiyo, kama nilivyosema moja kati ya kampuni *Max Malipo* itajenga vituo. Kwa hiyo, miongoni mwa maeneo ambayo yatajengwa pia katika wilaya hiyo ambayo ameitaja. Kwa hivyo, ndani ya mwaka huu *Inshaallah* ataona mabadiliko makubwa ahsante.

Nam. 82

Malalamiko ya Kutoa Huduma kwa Upendeleo kwa Mamlaka ya Nishati Zanzibar (*ZURA*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kumekuwa na Malalamiko kutoka kwa baadhi ya Wawekezaji wa Sekta ya Nishati ya Mafuta kuhusu Mamlaka ya Nishati Zanzibar (*ZURA*). Malalamiko yao yanahusu kwa baadhi ya wawekezaji kupatiwa ruhusa ya kufanya biashara ya mafuta kwenye vituo ambavyo havijajengwa "*canopy*" na baadhi ya wawekezaji wengine kutopewa ruhusa kama hiyo.

Je, kwa nini Mamlaka ya Nishati Zanzibar (*ZURA*) inafanya ubaguzi wa namna hiyo kwa wawekezaji, kinyume na Katiba ya Zanzibar ambayo inatoa haki kwa kila mtu kufanya shughuli halali za kuendesha maisha yake bila kubaguliwa au kubughudhiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 82 kama ifuatavyo**:**

Mhe. Spika, kabla ya kuundwa kwa *ZURA* mwaka 2015, vibali vya ujenzi wa vituo vya mafuta vikitolewa na Kamati Maalumu iliyokuwa ikisimamia suala hilo chini ya wizara iliyohusika na

nishati, Muombaji hupeleka barua yake kwa kamati hiyo na baada ya kukamilisha vigezo vyote vilivyowekwa, maamuzi yalifanyika na muhusika kupatiwa kibali cha ujenzi.

Mhe. Spika, baada ya kuanzishwa kwa *ZURA*, ruhusa ya ujenzi wa vituo vya mafuta na leseni za uendeshaji wa vituo vya mafuta, zimekuwa zikitolewa na *ZURA* kwa kufuata Kanuni ya usimamizi wa vituo vya mafuta ya mwaka 2016. Kanuni hiyo imetoa miongozo kadhaa inayohusiana na ujenzi wa vituo vya mafuta ambayo inapaswa itimizwe na muombaji kabla ya kukifungua kituo hicho cha mafuta.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu ya kanuni ya uendeshaji wa vituo vya mafuta ya mwaka 2016, inaelezea juu ya masharti ya ujenzi na kufanya ukarabati wa vituo vya mafuta, katika kifungu cha 21 cha kanuni hiyo, kinamtaka muombaji wa leseni lazima aweke sakafu kwa kutumia lami au zege katika eneo la kituo kwa ajili ya kuhimili uzito wa magari yanayotia mafuta. Aidha, kifungu cha 23 cha kanuni hiyo, kinamtaka muombaji leseni lazima ajenge paa (*canopy*) katika eneo la kituo kwa lengo la kulinda na kukinga mashine na vifaa vya kutilia mafuta na kuwakinga wafanyakazi katika hali ya jua na mvua.

Mhe. Spika, ni kweli kuna vituo vya mafuta ambavyo havina sakafu wala havina mapaa na vinaendelea kutoa huduma lakini vituo hivi ni vya zamani na ruhusa za ujenzi wake zilitolewa kabla ya kuja kwa *ZURA*. Kwa sasa *ZURA* imeviruhusu vituo hivyo kuendelea na kuuza mafuta na imewapa muda wamiliki wa vituo kufanya marekebisho yakiwemo ya kuweka sakafu na mapaa ili viweze kuendana na kanuni inayosimamia vituo vya mafuta.

Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Jaku Hashim pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba *ZURA* haifanyi kazi kwa ubaguzi wowote, kwani kutokanaa na masharti ya kazi yake ya kuwa mdhibiti, *ZURA* inaongozwa na sheria na kanuni. *ZURA* hairuhusu kituo chochote kipya kufanya bishara ya kuuza mafuta bila ya kuwa na paa au sakafu. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya kutokuridhisha ya Mhe. Naibu Waziri kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa *ZURA* Bwana Haji kwa umakini wake na utendaji wake mzuri.

Lakini nakwambia tena ubaguzi upo na ukitaka barua mimi nitakuletea ilitoka huko *ZURA*. Huoni ipo haja ya kukaa na watendaji wako wakaondosha tafauti hizo ushahidi upo ni hilo tu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mheshimiwa sijamuelewa.

Mhe. Spika: Huoni ipo haja ya kuondosha huo ubaguzi kukaa na watendaji mkaondosha huo ubaguzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Kama nilivyokuwa nimesema kwamba hakuna aina yoyote ya ubaguzi sasa kama yeye anao ushahidi wa hayo angeleta. Lakini pia nilitegemea kwamba kwa mujibu wa kanuni ya 59 fasili ya 9 ange-*declare* kwanza *interests* halafu tukaendelea.

Mhe. Spika: Mhe. Nassor Salim Ali kuhusu swala la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah ananambia ni-*declare interests* wapi athibitishe asizungumze .....

Mhe. Spika: Mheshimiwa sijakuruhusu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza a na b.

Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini vile vile nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa *ZURA* kwa kazi zake nzuri anazozifanya.

Mhe. Spika, kanuni ya uendeshaji wa vituo vya mafuta ya mwaka 2016 kifungu cha 21 kinamtaka muombaji wa leseni lazima awe na sakafu kwa kutumia lami au zege. Sasa katika majibu yake amesema kwamba *ZURA* hairuhusu kituo chochote kipya kufanya biashara ya kuu za mafuta bila ya kuwa na paa au sakafu.

Je, ni kwa nini baadhi ya vituo vimeruhusiwa kufanya biashara hiyo bila ya kufuata masharti hayo, kwa mfano kituo cha mafuta cha Maungani. Ni utaratibu gani ulioufanya kupewa ruhusa kufanya biashara hiyo bila ya kufata masharti hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Taarifa hiyo ndio kwanza naisikia lakini ni vyema tukafatana tukenda tukaangalia kwanza kituo hicho kilijengwa mwaka gani maana kama nilivyokuwa nimejibu kwamba baada ya kuanzishwa kwa *ZURA* hairuhusu kujengwa kituo bila ya paa na sakafu na huo ndio msimamo kwa mujibu wa sheria sasa ni vizuri tungeenda tukaona kwamba kweli kituo hiki na kimejengwa mwaka gani kusudi tukajua kulikuwa na tatizo gani. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa kwanza nataka niipongeze wizara kupitia *ZURA*, lakini kwa dhati kabisa nawapongeza *ZURA* kwa kuona kwamba umefika wakati tubadilike. Suala la uuzaji wa mafuta na wauza mafuta ni watu ambao wanaumia afya zao kama hapana *canopy* ya kusawaidia kwenye jua na mvua. Lakini pia kama hakuna zege chini ni hatari pia kwa maisha yao.

Kwa kuwa kuna vituo ambavyo zimeanza zamani vinaendelea lakini vimepewa muda ambapo vitoke katika vilivyo viingie katika muelekeo wa sasa. Ni muda gani hasa waliopewa, ili

wakamilishe hilo ili zoezi lao liende vizuri na wananchi wetu wapate afya nzuri katika wafanyakazi wasipate athari za hali ya hewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kila kituo kimepewa mwaka mmoja kwa ajili ya kukamilisha baada ya hapo hatua nyengine zitafata kama hajakamilisha. Ahsante sana.

Nam. 121

Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Tumbe

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza**:**

Kwa kuwa Jumuiya ya Maendeleo Jimbo la Tumbe katika kituo cha Afya cha Tumbe kwa mashirikiano na wananchi walijitokeza kujenga jengo kwa ajili ya kupatikana huduma za mama wajawazito kuweza kujifungulia hapo hapo kituoni pao. Ujenzi ambao umefikia hatua ya linta na kusubiri kumaliziwa jengo hilo ili liweze kutoa huduma.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kumalizia jengo hilo ili wananchi wa Tumbe wapate kufaidika na huduma hiyo.

(b) Je, Serikali haioni kumalizika kwa jengo hilo litapunguza shida za kina mama hao.

(c) Je, Serikali haioni endapo itamalizia jengo hilo itawafanya wananchi kupata ari na moyo wa kujitolea zaidi ili kuibua miradi mengine ya maendeleo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 121 lenye vipengele (a), (b) na c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kupongeza Jumuiya ya Maendeleo ya Jimbo la Tumbe pamoja na majimbo jirani ya Tumbe. Tunaomba Jumuiya nyengine zifanye mfano wa Jumuiya hii kwa kujitolea kufanya shughuli za maendeleo katika majimbo yao na hakika serikali inathamini juhudi zao na haitasita kuwanga mkono kwa faida yao na vizazi vijavyo.

(b) Mhe. Spika, viongozi wa Wizara ya Afya tukifuatana na Maafisa wa Idara ya Huduma za Hospitali tulifanya zaira na kukagua jengo hilo ambalo liko nyumba ya Kituo cha Afya cha Tumbe na kwa kweli tumeridhika na hatua iliyofikiwa. Hata hivyo wizara ilitoa maelekezo kidogo na sasa inasubiri kukabidhiwa jengo hilo ili kuliingiza katika mpango wa ujenzi wa wizara kwa hatua za kumalizia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kuwa sababu nyingi zinazopelekea akina mama kujifungua majumbani hasa vijijini kunatokana na umbali wa majengo, ubovu wa majengo, uhaba wa vituo na kumalizika kwa vituo kama hivi.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa makusudi kabisa kuvikamilisha vituo hivi ili akina mama hao waepekane na shida hii wanayoipata. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wizara ina mpango madhubuti wa kukamilisha jengo hili pamoja na majengo yote ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na ambayo yamo katika viwango na *formula* ambayo wizara tulitaka ifate.

Wizara itakamilisha majengo hayo kupitia nguvu ya serikali pamoja na misaada mbali mbali ya wafadhili ambao wanatusaidia. Ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri serikali ina mpango wa kumaliza haya majengo, nalizungumzia jengo hili hili ambalo Mhe. Shaib Said Ali aliliulizia suala la msingi.

(a) Ni kiasi gani cha fedha katika kumalizia hili jengo serikali imeweza kuzitambua kwa sababu nitajua hasa kama kuna umadhubuti ya kwenda kulitambua hili.

(b) Ni kwa bajeti ipi itakayokwenda kumaliza hii tuliyoipitisha juzi au bajeti ijayo katika kukamilisha huo mpango au Mhe. Naibu Waziri alizungumza. Lakini zaidi kwa kitu hichi ambacho kimeuliziwa suala la msingi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba arudie swali la (b).

Mhe: Spika: Naomba urejee swali la (b) Mheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Kwa kuwa ameshasema serikali inataka kukamilisha huo mpango utakamilishwa kwa bajeti ipi kwa sababu bajeti hii tuliyoipitisha hatujaona mle ndani yake. Lakini labda wao kuna maeneo wametenga ni kiasi gani ambazo zitatumika katika bajeti hii na kama si bajeti hii basi ni bajeti ipi ambapo huo mpango uliouzungumza kuwa serikali itamaliza utaweza kukamilisha kituo hichi ambacho kimezungumziwa suala la msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya huwa tunakamilisha vituo vingi kutokana na misaada ya wafadhili mbali mbali ambao wanaendelea kutuunga mkono. Kwa hivyo, kituo hichi na vituo vyengine vilivyopo vitakamilishwa kupitia misaada na nikisema kupitia kwa mashirikiano na wizara ni

kwamba wizara itaingiza nguvu kupitia mapato mbali mbali yanayopatikana katika Wizara ya Afya.

Nam. 150

Matumizi ya Usafiri wa Baharini Kinyume na Taratibu zilizowekwa Kisheria

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Pamoja na pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala zima la kubinafsisha shughuli yote ya usafiri wa baharini na kumpongeza Muwekezaji Mzalendo kwa uwezo wake wa kumiliki asilimia kubwa ya usafiri huo, lakini bado kumejitokeza baadhi ya changamoto mbali mbali katika shughuli hiyo kupitia vyombo hivyo.

(a) Je, serikali imetoa ruhusa ya kuegeshwa vyombo hivyo katika eneo binafsi la muwekezaji huyo yaani Mtoni Marine.

(b) Je, sehemu hiyo lini imeanza kutekeleza shughuli hiyo katika eneo hilo ambalo halina hata vikosi vya Ulinzi vya Zanzibar wala Polisi.

(c) Serikali imejipanga vipi katika kukabiliana na matokeo mbali mbali yatakayotokea katika eneo ambalo sio rasmi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la 150 lenye vipengele (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, eneo linalotumika sasa la Mtoni Marine hadi katika eneo la Beit el Ras skuli ni eneo lililo chini ya usimamizi wa Shirika la Bandari. Hivyo, bado eneo hilo limo ndani ya udhibiti mzuri.

(b) Mhe. Spika, meli zinazotumia eneo hilo kwa sasa hutumia kwa shughuli za kuegesha tu na wala meli hizo hazijatumika kwa shughuli za kuingizia mizigo wala abiria katika eneo hilo.

(c) Mhe. Spika, kwa kuwa hakuna shughuli zozote za kibiashara zinazoendelea katika eneo hilo hatutegemei kutokea matukio hatarishi kwa usalama. Hata hivyo, Wizara kupitia Shirika la Bandari inalipokea hili na itaendelea kuwa muangalifu na kuongeza umakini katika kulisimamia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na kutojibiwa ipasavyo swali langu (a) la msingi narudia tena.

(a) Je, serikali imetoa ruhusa ya kuegeshwa chombo kile pale.

(b) Na kama serikali haijatoa ruhusa ni sheria gani au hatua gani zilizochukuliwa kwa ukiukwaji wa taratibu zile vyombo vya abiria mara baada ya kumalizika abiria kuegeshwa katika eneo la mfanyabiashara yule.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Sisi serikalini kupitia wizara yetu tulipata taarifa kwamba kuna baadhi ya meli zimeegeshwa kule na tukachukua hatua moja kwa moja ya kuhakikisha kwamba zile meli zilizokuwepo kule ili baadae zisije kuleta hiyo sitofahamu tukaziagiza ziondoke pale zirudi maeneo mengine ya bandari.

Kwa hivyo, hiyo ndio hali iliyofanyika na kama sheria yetu inavyosema ya mwaka 1997 namba 1. Majukumu yote ya kuhakikisha kwamba meli zinafunga na kutofunga bandarini yapo chini ya mamlaka ya Shirika la bandari. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza.Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa mwazo hizi meli zilikuwa zinapakiwa katika eneo ambalo amekiri kulijua lakini sisi tunalieleza tu moja kwa moja eneo ambalo anafanya ujenzi Bakhresa na ni meli za *Azam Marine*. Kukiri kwamba baadae akasema serikali imechukua hatua za kuzirejesha katika eneo linalohusika kwa maana zisipakiwe kule. Kwa utaratibu huu tayari kosa kisheria kwa mujibu wa hizo kanuni ambazo amezisema zimetendeka.

Ni hatua gani zilizochukuliwa katika kutoa adhabu kwa yule aliyefanya kadhia hii kwa sababu kakiuka ile sheria ya *parking* ya meli kama ambavyo ilivyokuwa inasema. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema Shirika la Bandari baada ya kupata hizo taarifa na mimi napenda sana Wawakilishi mnapohisi kuna mambo kama haya basi tuwasiliane na sisi ili hatua za kisheria zichukuliwe mara moja.

Kwa hivyo, sisi baada ya kupata hizo taarifa tumewaomba na tukawataka mara moja wale walioweka meli pale waondoshe ili kuondosha wenyewe wanasema wasiwasi wa kwamba anaweza akaja kufunga pale na kupitisha mizigo yake ambapo kwa utaratibu wa bandari hairuhusiwi mtu yoyote kufunga isipokuwa katika zile gati ambazo au bandari zinajulikana kwa mujibu wa sheria yetu namba 1 ya mwaka 1997.

Kwa hiyo, mara moja ameondosha na hatua nyengine tutazichukuwa na baada ya hapo tutazielezea Baraza letu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 186

Kukosekana Kituo cha Afya katika Bandari ya Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Kwa vile kituo cha ukaguzi wa afya za abiria wanaotoka na kuingia Zanzibar kupitia Bandari ya Malindi ni muhimu kwa nchi yetu, na kukosekana kwake kunaweza kuhatarisha afya ya nchi nzima kama vile kusambaa magonjwa hatari ya ebola, mafua ya ndege n.k. Hata hivyo, bado eneo la bandari ya abiria vituo vyote muhimu vimepatiwa nafasi ya kujenga ofisi lakini Kituo cha afya ambacho ni muhimu zaidi hakijapatiwa nafasi ya kuwa na ofisi yake.

(a) Je, kukosekana nafasi ya ofisi ya kituo cha afya si kuhatarisha afya za wananchi wetu kwa vile udhibiti wa uingiaji na utokaji wa maradhi hautafanyika kwa ufanisi.

(b) Hatua gani za haraka zitachukuliwa kwa kituo hicho kujengwa haraka haraka katika Bandari ya abiria Malindi.

(c) Kwa kuwa imeonekana mwekezaji hana tatizo na uwepo wa kituo hicho isipokuwa washauri wake, je Serikali ambayo ndiyo dhamana wa kusimamia sera ya afya nchini, haioni ulazima wa kumlazimisha mwekezaji wa eneo la bandari ya abiria kutoa nafasi ya ujenzi wa kituo cha afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 186 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kuwa Shirika la Bandari lina Kituo cha Afya kwa ajili ya abiria wanaoingia na kutoka katika Bandari ndogo ya Abiria Malindi. Vile vile kuna kituo cha Afya katika Bandari Kuu ambacho kinahudumia abiria pamoja na wafanyakazi wote wa Bandarini pamoja na Taasisi nyengine zilizomo ndani ya Bandari pale Malindi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokujibu suala la msingi kama lilivyo. Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii wanalalamika katika ripoti yao hawana kituo. Je, baada ya kikao hichi tutakwenda kule bandarini ukanioneshe kituo hicho ili tukione mimi na wewe mguu kwa mguu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako namwambie tuko tayari akakione na mimi nitamshangaa sana Mhe. Jaku Hashim kwa sababu yeye yuko mdau mkubwa wa bandari asikijue kitu kile. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, na nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kutuelekeza pamoja na Mhe. Jaku Hashim ule utaratibu wa kuungana nae mkono.

Lakini kwa kuwa yeye ni mdau mkubwa wa wizara hii na anayajua mengi katika maeneo hayo. Naomba tu atwambie ule uwepo wa kituo tumechaukubali ni daktari gani dhamana wa vituo hivi viwili ambavyo serikali imemuanisha kukaa pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama tunavyojua utaratibu wa vituo vile vya afya wanakuwepo zaidi madaktari ambao wanatoka Wizara ya Afya na ile ni kazi ya Wizara ya Afya kuidhinisha madaktari. Lakini kwa kituo kilichokuwepo pale katika uingiaji na utokaji wa abiria yupo muunguzi anaitwa ndugu Mustafa. Ahsante sana Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Sawa subiri nitakupa. Waheshimiwa nina tangazo la wageni. Wageni wetu waliofika leo ni wageni wa Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mgogoni wageni wenyewe kama ifuatavyo:

1. Halima Shehe Hamad - Mwanasheria
2. Shakira Ahmed Ali - Mwanafunzi
3. Rutfa Bien Panye - Injinia Ujenzi Skuli ya Daya Mtambwe. Ahsante. Baada ya hapo

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Muongozo Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante naanza kwanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana kwanza nikushukuru. Mhe. Spika, roho ina choyo na ina sehemu binaadamu hakutolewa nyongo. Mhe. Spika, leo tarehe 22 Juni, kuna hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na uingizaji na utumiaji, kuna maazimio kama mawili.

Mhe. Spika, katika kikao kilichopita cha tarehe 27/10/2014 nilileta hoja binafsi kutoka Wizara ya Afya na nikawa na maazimio saba. Tarehe 27/10/2014 nilileta hoja binafsi katika kikao cha Baraza lilichopita na nikasema hata ukiwa na duka lako, Mhe. Abdalla ana duka linatoka milango halitoki roho inauma. Nilileta azimio hili muda mrefu na serikali maazio hayo kimsingi wameyakubali na kama utaniruhusu Mhe. Spika, nilifanya kazi kubwa sana ya kuyatafuta ni saba, moja tu serikali ililikataa. Leo naona ni mwaka wa sita huu hakuna jawabu lililopatikana na mimi sikutolewa nyongo.

Nataka muongozo wa kiti chako Mhe. Spika, na kama utaniruhusu naomba kujikumbusha kidogo ili wajumbe waweze kufahamu wakumbuke hii katika kipindi kilichopita.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hoja yako yaani huo muongozo unaotaka unataka kitu gani sijakupata bado.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja yangu ni kwamba serikali haikuja na majibu ya swali langu la hoja binafsi. Leo naziona hoja binafsi mbili zimekubaliwa na serikali kuzirekebisha, lakini langu mimi halijajibiwa tokea mwaka 2014. Hili Mhe. Spika, likiwa ni geni kwako. Kama utaniruhusu hoja yenyewe ilikuwa, waheshimiwa kiutaratibu maazimio yapo saba, nitasoma moja nitahoji ukimaliza utakwenda la pili, mpaka tuyamalize wale wanaounga mkono wataonyesha mikono na wanaokataa wataonesha mikono vile vile.

Katibu Waheshimiwa Wajumbe, tunasoma maadhimio yanayotakiwa na hoja ya mjumbe kuhusu uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi Zanzibar.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hiyo hoja unayozungumza ilikuwa kwenye Baraza lililopita si ndio.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa sawa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, wengi wetu hapa hatukuwepo. Sasa suala hili pamoja na umuhimu wake mimi ningekushauri tungekutana mimi wewe na hao wahusika nje ya Baraza hapa, ili tukalitafutia ufumbuzi na baadae tukalileta humu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimekubali Mhe. Spika, muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kuniona. Mhe. Spika, naomba muongozo wako nikitilia maanani kifungu cha 18 cha katiba, naomba nikisome baadae nitakazia na kifungu cha 2(2).

> "Bila ya kuathiri sheria ya nchi kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote ya kutoa nje mawazo yake na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi na pia ana uhuru ya mawasiliano yake kutokuingiliwa.

Fasili ya 2:

> 'Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambapo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu ya kijamii'.

Mhe. Spika, baada ya kunukuu kifungu hicho na fasili ya 2, *ZBC* imekuwa na mtindo wa kuto kutoa habari kwa Baraza lako tukufu. Mara kwa mara imekuwa inakatika na jambo hili linawaathiri sana wananchi wetu. Kwa hivyo, tungeomba muongozo wako ili tujuwe kitu gani kinachosababisha kitu hiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe, na bahati nzuri Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pia yupo hapa. Lakini hapa kubwa ni matangazo kutokuonekana moja kwa moja.

Sehemu ya unachokizungumza ina ukweli, lakini kwa kiasi kikubwa kwa sababu mara nyingi hata mimi ninapokuwa sipo kwenye kiti, basi huwa nafuatilia shughuli za Baraza kwa kupitia TV na inarushwa na hao hao *ZBC*. Kuna wakati kunakuwa na matatizo kweli matangazo huwa yanakatika, lakini mara nyingi sana matangazo yanakuwepo hewani. Sasa labda tumsikilize Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kama analo neno kidogo ili atusaidie katika hili. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba chombo kinachotoa habari ni chombo cha *electronic*, na *electronic* ni chombo ambacho kinatengenezwa na binadamu. Kwa uwezo unaofanywa na *ZBC* ni kuhakikisha kwamba habari na taarifa zote zinapatikana masaa 24 kama kilivyoidhinishwa katika sheria zake chombo kile cha serikali.

Kwa hivyo, sio televisheni tu ni pamoja na redio zote zinapaswa kutoa taarifa kwa muda huo na kama wananchi wanavyotarajia kuzipokea hizo taarifa ndivyo inavyopaswa kupatikana. Kukatika matangazo kwa kipindi hiki, natumaini hata matangazo yetu pia tumeyaeleza kwamba tumo katika kipindi cha matengenezo.

Mhe. Spika, juzi nilieleza katika kujibu moja katika swali mama hapa kwamba tumo katika matengenezo na nikawaomba Waheshimiwa Wawakilishi, wawe wakwanza mashahidi wende wakatazame mule matengenezo ambayo yanafaywa.

Kwa mfano, studio zile zetu za zamani tulipokuwa tukitumia matangazo zote tumehama kwa kuzifanyia matengenezo mapya. Hivi sasa tunatumia studio za dharura, kwa hivyo vitu kama hivyo kujitokeza ni wajibu wake.

Lakini vile vile suala la kukatika kwa umeme nalo pia linaathiri, bado hatujawa na ile *stability* ya asilimia mia, wakati unapokatika umeme tunarudi kwenye jenereta, hali kama hiyo inatokea hata humu ndani ya Baraza, kuna saa tunakaa kiza taa zote zinaondoka, kuna wakati matangazo yanakuwa hayaonekani pale kwa sababu ya umeme. Kwa hivyo, pale panapokatika umeme ni lazima kuwe kuna *short time* ambayo kutoka matangazo yalivyotokea na matangazo yanavyoundwa. Kwa hivyo, ni kweli nakubaliana na hilo, lakini muda mfupi tu tumwambie tatizo hilo litapoa vifaa vipya vyote tumevipata na vyote vimefika na awe tayari kununua na king'amuzi kipya kinachokuja na bei tutaitoa hivi karibuni. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa taarifa ambayo umeitoa hapo nafikiri itakuwa imeturidhisha sote.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita katibu, naomba sasa nimwite Mwenyekiti Mhe. Shehe Hamad Mattar aje achukuwe nafasi kwa ajili ya kuendesha shughuli zilizobaki. Mhe. Mwenyekiti, karibu sana.

Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Katibu tunaendelea.

TAARIFA ZA SERIKALI

Maelezo ya Utekelezaji wa Maazimio ya Baraza La Wawakilishi Kuhusu Ongezeko la Uingizaji na Utumiaji wa Dawa za Kulevya Zanzibar

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia kukutana hapa tena leo, lakini kwa kutupa uwezo wa kufunga katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa furaha na salama kubwa. Tumuombe yeye Mola wetu atuzidishie heri, baraka na mafanikio katika nchi yetu, atupe umoja, amani na utulivu wa nchi, ili atuwezesha kukamilisha Ramadhani yetu, na tuweze kupata fursa ya kusherehekea vizuri Skukuu ya Iddi, ewe Mola Muweza tufikishe kwa salama na amani.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi pamoja na viongozi wetu wote wa Baraza hili tukufu, kwa kuliongoza vyema Baraza hili. Aidha, nimshukuru kwa namna ya pekee mtoa hoja hii Mhe. Mohamed Said Mohamed Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mpendae, pamoja na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa maelekezo yao katika hoja hii na hatimaye kukubaliana na maazimio ya Baraza lako tukufu juu ya hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia Kanuni ya 58(9) ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2016, na kwa ruhusa yako, kabla ya kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa maazimio ya Baraza lako Tukufu juu hoja ya ongezeko la uingizwaji na utumiaji wa dawa za kulevya, naomba kuielezea kwa ufupi Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar pamoja na majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya 2009 ya Sheria za Zanzibar, ambapo katika kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo kinataja majukumu ya Tume kuwa ni Kuiainisha, Kuifafanua, Kuitangaza na Kuiratibu Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Matumizi na Biashara haramu ya Dawa za Kulevya.

Aidha kifungu cha 7 cha Sheria hiyo kinataja kazi za Tume kuwa ni kufanya yafuatayo:-

a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya.
b) Kusimamia utekelezaji wa mikataba na itifaki za Kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya.
c) Kupitia sheria na kanuni za udhibiti wa dawa za kulevya na kupendekeza marekebisho ili ziendane na wakati.
d) Kuimarisha na kuendeleza jitihada za kuzuia matumizi ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya dawa hizo.
e) Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya.

f) Kuendeleza mipango ya tiba na urekebishaji wa tabia za waathirika wa dawa za kulevya.
g) Kufanya tafiti kuhusu ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya.
h) Kutoa mafunzo kwa watu wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya.
i) Kuimarisha na kuendeleza uhusiano wa Kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya.
j) Kuratibu na kusaidia shughuli zinazofanywa na asasi zisizokuwa za kiserikali (*NGO's*) na vikundi mbali mbali vya kijamii vinavyoshiriki katika kupiga vita dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa maelezo kuhusu maazimio ya Baraza lako Tukufu kuhusu hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, msingi wa hoja iliyozaa maazimio haya ya Baraza unatokana na maeneo makuu matatu:

1. Kisheria.
2. Mipaka yetu inavyotumika vibaya kwa kuhusishwa na biashara ya dawa za kulevya kutokana na jiografia yake.
3. Mashirikiano ya taasisi za ndani na nje katika kupambana na mtandao wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa suala la kisheria, serikali imejipanga katika usimamizi wake kupitia sheria ambazo zinalenga katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Miongoni mwa sheria hizo ni pamoja na sheria yenyewe ya dawa za kulevya, Sheria Namba 9 ya 2009 ambayo imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili iendane na mahitaji na wakati uliopo na ujao. Aidha, serikali imetunga kanuni mbili ikiwa moja ni ya viwango vidogo vya dawa za kulevya na moja ni ya uangamizaji kwa ajili ya kuendeleza mapambano ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mantiki ya kanuni hizi ni kutofautisha viwango vya dawa za kulevya, kumtambua mfanyabiashara wa dawa za kulevya na mtumiaji wa dawa za kulevya na kuzuia dhamana kwa wale wote watakaokutwa na dawa za kulevya. Aidha, kanuni hizi zitasaidia kuzuia dawa za kulevya kutokurudia tena mitaani na pia kuzuia uharibifu wa kesi za dawa za kulevya kutokana na upotevu wa vielelezo pamoja na kuharibika kwa vielelezo, msingi ni kuwa na ushahidi imara.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali, sheria hii pia imeunda Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya hapa Zanzibar, ambayo ndani yake kuna viongozi mbali mbali ambao taasisi zao kwa njia moja au nyengine zinahusika na upambanaji wa biashara hii au zinahusika na matibabu kwa wanaotumia dawa hizo. Taasisi hizo huwa zinapokea maelekezo ya tume yenye lengo la kuleta na kuongeza ufanisi katika vita dhidi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, wafuatao ni Wajumbe wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Zanzibar kama ifuatavyo:-

1. Mwenyekiti – ambae anateuliwa na Mhe. Rais ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa sasa Balozi Seif Ali Iddi.
2. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. (Mjumbe) ambae pia ni Makamu Mwenyekiti.

3. Waziri anaeshughulikia masuala ya Afya (Mjumbe)
4. Waziri anaeshughulikia Vijana (Mjumbe)
5. Waziri anaeshughulikia Elimu (Mjumbe)
6. Waziri anaeshughulikia Bandari na Viwanja vya Ndege (Mjumbe)
7. Waziri anaeshughulikia Utalii (Mjumbe)
8. Waziri anaeshughulikia Tawala za Mikao (Mjumbe)
9. Waziri anaeshughulikia Sheria (Mjumbe)
10. Mkurugenzi wa Mashtaka (Mjumbe)
11. Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar (Mjumbe)
12. Kamishna wa Polisi Zanzibar (Mjumbe)
13. Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa Zanzibar (Mjumbe)
14. Naibu Mkurugenzi wa Forodha Zanzibar (Mjumbe)
15. Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar (Mjumbe)

Wajumbe wawili ambao watateuliwa na waziri husika ambao ni:-

16. Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Rushwa (Mjumbe)
17. Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mjumbe)
18. Na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ambae anakuwa Katibu wa Tume.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na mipaka yetu, serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imehamasisha na kutoa taaluma juu ya athari zinazotokana na dawa za kulevya pamoja na mbinu zinazotumiwa na wahalifu katika kuingiza na kusambaza dawa hizo. Aidha, tume imetoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria wanaofanya kazi katika mipaka yetu pamoja na mafunzo maalum kwa wapelelezi, mafunzo hayo pia yanatolewa kwa masheha na wajumbe wao.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mashirikiano na taasisi za ndani na nje katika kupambana na mtandao wa dawa za kulevya serikali imezingatia mashirikiano mema yatakayoleta tija dhidi ya uhalifu, serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa inapambana na mitandao ya kihalifu ya ndani na nje ya nchi, kwatunga Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya 2012; na kuanzisha Sheria ya Kupambana na Utakatishaji wa Fedha Haramu Nam. 10 ya 2009 (*Anti Money Laundry and Proceed of Crimes Act*), aidha Sheria ya Kuzuia Ugaidi (*Prevention of Terrorism Act*) pamoja na Sheria ya Dawa za Kulevya yenyewe. Sheria hizi zimetoa uwezo kwa wasimamizi wake kuwa na mahusiano na mataifa mengine katika kupambana na uhalifu huo. Pia taasisi hizo huwa zinafanya kazi kwa karibu mno na taasisi za kikanda na kimataifa ambazo ni *SADC, INTERPOL, EAC, AU* na *UNODC,* na kadhalika. Hii yote ni dhamira njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kupambana na mitandao ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa maazimio ya Baraza la Wawakilishi juu ya ongezeko la uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya hapa Zanzibar kama ifuatavyo:-

Azimio Nambari 1. Serikali ihakikishe kuwa inasimamia bila muhali wowote utekelezaji wa Sheria Namb. 9 ya 2009 ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ili kulinusuru Taifa pamoja na vijana wetu katika kujiingiza kwenye biashara haramu na matumizi ya za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inasimamia sheria hii bila ya muhali kwani muda wote inazingatia utekelezaji wake kwa kuona inatekelezeka vizuri na ndio maana inachukua hatua kila pale inapoona kunahitajikakufanya marekebisho huwa inafanya hivyo. Ili kuhakikisha kuwa watuhumiwa wa dawa za kulevya hawapati mwanya, serikali imetengeneza kanuni ya viwango vidogo kwa lengo la kuzuia kuwapa dhamana watuhumiwa wote wa dawa za kulevya, na katika kudhibiti upotevu wa vielelezo kanuni ya uangamizaji nayo pia imetengenezwa. Mhe. Mwenyekiti, kanuni hizo zimeshakamilika na sasa ziko tayari kwa kufanyakazi, ili zisaidie katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.

Azimio Nambari 2. Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar (*ZAECA*) ihakikishe inafuatilia kwa ukaribu kesi zote zinazohusiana na dawa za kulevya ili kubaini wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika kesi hizi, pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa yeyote atakaebainika kuchukua rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha Sheria Namba 9 ya 2009 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya kinampa Waziri husika uwezo wa kuteua wajumbe wawili wa Tume, kwa kuzingatia umuhimu wa vita hivi, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ameteuliwa kuwa mjumbe wa tume, ili ahusike moja kwa moja na kuleta wepesi katika mapambano.

Azimio Nambari 3 na Nambari 4. Jeshi la Polisi, Waendesha Mashitaka pamoja na Mahakama ziandae utaratibu maalum ambao utasaidia ushahidi wa kesi za dawa za kulevya kukamilika kwa haraka ili kesi zimalizike kwa wakati na kwa mujibu wa sheria ili kurudisha imani kwa wananchi kwa vyombo vyao vya kutoa haki katika kesi zinazohusiana na dawa zakulevya. Kwani takwimu zinaonesha kuwa kiasi ya kesi zisizopungua 294 za dawa za kulevya bado zinaendelea na uchunguzi.

Wakuu wa Wilaya, Masheha pamoja na wananchi watoe ushirikiano mkubwa kwa vyombo vya dola kwa kutoa taarifa haraka iwezekavyo pale wanapobaini vitendo vya uingizwaji au utumiaji wa dawa za kulevya katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Katika maazimio ya Namba 3 na 4 ambayo kimsingi yanashabihiyana naomba kutoa maelezo ya pamoja ya maazimio haya kama ifuatavyo. Serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imekuwa ikifanya vikao *(round table)* vya kila mara ambavyo vinawashirikisha Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha na Watendaji wa taasisi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa kesi za dawa za kulevya zinaenda kwa haraka na zinapata hatia kwa mujibu wa sheria. Aidha Tume hutoa maelekezo mbalimbali kwa viongozi wote wanahusika kisheria katika mapambano haya ili haki itendeke na sheria ichukue mkondo wake.

Azimio Nambari 5. Serikali iimarishe ulinzi ikiwemo pamoja na kununua vifaa vya ukaguzi vya kisasa vikiwemo *X-Ray machine na test kit* katika maeneo ya usafiri ikiwemo uwanja wa ndege na bandarini ili kuhakikisha kuwa njia hizo hazitumiki kuingiza madawa ya kulevyanchini. Kwani imebainika kuwa maeneo hayo ndiyo njia kuu zinazotumika kuingiza dawa za kulevya. Hii *test kit* Zanzibar bado haijawahi kuja lakini unaweza ku-*detect* madawa ya kulevya palepale

katika *destination*. Hii itatusaidia sana kuliko kutegemea zile *X-Ray machine* ambazo zile za kupekua mizigo haziwezi ku-*detect* mambo ya unga.

Majibu ya Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la vifaa vya kubaini uwepo wa dawa za kulevya katika maeneo ya usafiri ikiwemo uwanja wa ndege na bandarini, Serikali imepanga kuwa na mradi wa pamoja ambao utahusisha uwekaji wa vifaa na mfumo wa kisasa wa kuweza kubaini mienendo na vitendo vyote vya kiuhalifu katika maeneo hayo ikiwemo usafirishaji wa dawa za kulevya. Huo ndio mtazamo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuwa na mashine za kisasa zenye uwezo mkubwa wa kubaini uhalifu katika maeneo hayo pamoja na maeneo mengine nchini.

Azimio Nambari 6. Serikali itafute suluhisho la kudumu juu ya kukomesha matumizi ya bandari bubu nchini, jambo ambalo ni sehemu ambazo hutumika mara kwa mara kuingiza dawa za kulevya ikiwemo bangi na mirungi.

Majibu ya Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli bandari zisizo rasmi hapa nchini zimekuwa zikitumika kwa vitendo vya uvunjaji wa sheria za nchi ikiwemo ukwepaji wa kodi, usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya magendo, vitendo vya kihalifu na uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya. Hata hivyo, bandari hizi pia zimekuwa zikitumika katika shughuli za kijamii na kiuchumi ikiwemo uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inatekeleza mpango maalum wa kufanya uhamasishaji katika shehia zote zenye madiko na bandari kwa lengo la kuwahamasisha watendaji, wananchi na wale wote ambao wako karibu na shehia zilizozungukwa na maji ya bahari kwa kuwapa taaluma ya kutambua mbinu za wahalifu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya pamoja na kutoa taarifa katika vyombo husika. Tume itaendelea na utekelezaji wa mpango huo katika maeneo yote yenye madiko na bandari zisizo rasmi pamoja na kuhakikisha kuwa Jeshi la Polisi linaimarisha doria katika maeneo hayo ili kudhibiti biashara hii haramu.

Azimio Nambari 7. Serikali ihakikishe inaleta Barazani Ripoti ya Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za kulevya ya Zanzibar ya mwaka 2016, ili kukidhi masharti ya Kifungu cha 8 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2009 na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi waelewe kuhusu taarifa zinazohusiana na na dawa za kulevya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya Zanzibar Namb. 9 ya 2009, Serikali inapaswa kuwasilisha Taarifa ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya katika vikao vya Baraza la Wawakilishi kila mwaka. Tume inaahidi kulifanyia kazi suala hili ili iweze kutoa taarifa hizo kwa mujibu wa Sheria.

Azimio Nambari 8. Pamoja na juhudi za serikali za kuwatoa vijana katika matumizi ya dawa za kulevya, tunaomba Serikali ianzishe operesheni maalum ya kuwasaka wananwake wote au wale wote wanaotumia dawa za kulevya ili kuwanusuru na janga hili, kwani endapo tutaendelea kulifumbia macho tatizo hili tunaweza tukalikuta kundi kubwa la watumiaji wa dawa za kulevya

ni wanawake na wale wengine na hivyo kuipelekea jamii kubwa katika sehemu mbaya zaidi hasa ukiangalia ule msemo ukielimisha mwanamke mmoja unaelimisha jamii kubwa sana.

Majibu ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea na juhudi za kuwasaka wale wote wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya bila kujali jinsia ili kuweza kuwanusuru na janga hilo. Ndio maana kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Serikali imekuwa ikitoa ruzuku maalum kwa nyumba za upataji nafuu *(sober houses)* pamoja na kusaidia programu nyengine za upataji nafuu dhidi ya dawa za kulevya. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuchukua kila hatua kuwanusuru vijana wetu na matumizi ya dawa za kulevya ili jinsia zote zipate ahueni na tatizo hili. Jambo hili tunafaa sote kwa pamoja kushirikiana na kupambana nalo.

Azimio Nambari 9. Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali iandae utaratibu maalum kwa skuli zote za Serikali na binafsi zilizopo Zanzibar kuwatambua wanafunzi wote wanaotumia dawa za kulevya na hatua zinazostahiki zichukuliwe kwa mwanafunzi yeyote atakaebainika kutumia dawa za kulevya ili kukomesha matumizi ya dawa hizo kwa wanafunzi wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inatambua hatari iliyopo kwa wanafunzi kutumika katika usambazaji pamoja na wao wenyewe kutumia dawa za kulevya. Serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufanya uhamasishaji na kutoa taaluma kwa vijana juu ya kinga ya msingi dhidi ya dawa za kulevya *Primary Prevention* pamoja na kufuatilia kwa karibu mtandao huo ili kunusuru watoto wasiingie katika balaa hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya katika kikao cha Sitini cha Kamisheni za Dawa za Kulevya Duniani kilichofanyika Vienna, Austria tarehe 13 – 17 Machi, *2017 THE SIXTIETH SESSION OF THE COMMISSION ON NARCOTIC DRUGS HELD FROM 13-17 MARCH, 2017 IN VIENNA, AUSTRIA* kilizungumza na taasisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani *UNODC* kuhusiana na kupata taaluma zaidi juu ya kuwasimamia vijana na watoto wasijiingize katika janga hili la dawa za kulevya.

Shirika hilo lilikubaliana na hoja hiyo na kupitia Ofisi yake ya Kikanda iliyopo Nairobi ilikuja rasmi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kuanzisha mradi wa *Strong Family,* ambao utaratibiwa na Tume na kuwashirikisha moja kwa moja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Mradi huo uko katika hatua ya awali ambapo watendaji watatu, kutoka Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto walidhaminiwa na *UNODC* kwenda New Delhi, India kwa ajili ya ziara ya kimasomo ili wapate taaluma ya jinsi ya kuwanusuru wanafunzi wetu na kadhia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua kila hatua kuhakikisha wanafunzi wetu wanakuwa salama ili kuepukana na vitendo hivi viovu vyenye athari kubwa kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, hitimisho. Baada ya kutoa maelezo hayo kuhusu hoja binafsi iliyowasilishwa Mhe. Mohammed Said Dimwa, katika Baraza lako tukufu kwa mara nyengine tena napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dimwa kwa kuweza kuja na hoja hii ambayo inamgusa kila mmoja wetu, na nimpongeze sana kwa juhudi zake katika mapambano haya dhidi ya madawa ya kulevya juhudi ambazo zinahitaji kuwa jasiri na sote tunapaswa kufanya hivyo ili kupambana na tatizo hili gumu lililo mbele yetu, naamini kwa mashirikiano yetu tutafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Suala la mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya bado linaleta changamoto kubwa katika ngazi zote. Mashirikiano katika vita hii yanahitajika kutoka kwa wadau wote wakiwemo vyombo vya Sheria, Taasisi za Serikali na vyombo vya Ulinzi na Usalama, viongozi na wananchi kwa jumla ili kwa pamoja tuweze kufikia azma ya Serikali ya kupunguza na hatimae kuondosha kabisa biashara na matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini. Naamini kwa pamoja tunaweza na Zanzibar bila ya dawa za kulevya inawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa taarifa. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tunayo nafasi ya kutoa maoni.

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Hoja ya Serikali tunaomba muongozo wako kama hoja hii inachangiwa au laa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe nimeisikia hoja yako na matokeo ni kama ifuatavyo. Waheshimiwa Wajumbe, taarifa hii mnaweza kuijadili na kutoa maoni yenu kwa hivyo karibuni. Kwanza namwita Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ushauri au uzoefu unasema mtoa hoja aanze yeye halafu baadae na sisi tutafuata, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa ridhaa yangu mwenyewe lakini halafu unipe tena naomba umpe aendelee halafu baadae kwa ridhaa yako ya kiti nitaomba tena kusimama niendelee ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa hivyo Mhe. Mohammed Said Mohammed karibu sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini nimshukuru Mhe. Hamza kwa kuona ipo haja ya mtoa hoja akaweza kuchangia kuwa ndio mtu wa mwanzo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa majumuisho ya hoja yangu na kutekeleza maazimio yote ambayo Baraza liliazimia, jambo ambalo limeoneshwa na Serikali yetu ni jambo la kiungwana sana kwa sababu sisi Wawakilishi wa wananchi tunapoleta hoja tunakusudia kujenga nchi yetu, lakini na Serikali ime-*respond* vizuri tunasema tunaishukuru sana na tunaipongeza kwa hatua kubwa ambayo imefanya.

Mhe. Mwenyekiti, jambo ambalo liloopo mbele yetu ni jambo linalo kadhia kubwa sana na limejitokeza sana lakini baada ya kutoa hoja ile na tumeiona jinsi gani Serikali ime-*react* na jambo lile kubwa limeanza kupungua sasa mitaani, tunawapongeza sana na tunawaambia tu waendelee kutusikiliza wawakilishi wa wananchi ndio tunaokaa na wananchi kule chini.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kutoa pongezi tu kwa Serikali kwa hoja ambayo nimeitoa lakini Serikali ime-*react* vizuri niwapongeze sana na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya mwanzo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa nakuruhusu Mhe. Hamza Hassan Juma uendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kueleza machache katika hoja hii ambayo iko mbele yetu inayohusiana na masuala mazima kuhusu ongezeko la madawa ya kulevya Zanzibar. Kwanza nataka nimpongeze Mjumbe aliyeumiza kichwa chake akafanya utafiti na mpaka akaweza kuona ukubwa wa tatizo akaweza kuleta hoja yake Barazani ili kuishauri Serikali nini cha kufaya ili kuweza kuondokana na tatizo kubwa la madawa ya kulevya. Mhe. Dimwa hongera sana tunakupa pongezi na tunakuomba usichoke na kufanya hizi jitihada kwani hayo ndio majukumu ambayo tumeletewa hapa Barazani na wananchi wetu.

Lakini vile vile nataka niipongeze na Serikali yetu katika kipindi hichi Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Makamu wa pili wa Rais, kwa sababu baada ya kufanya marekebisho ya kanuni zetu kwa kweli sasa hivi Serikali tofauti na vile ilivyokuwa zamani kila hoja tunayoileta Serikali wanakaa na wanatuletea jawabu ambazo zinaridhisha kwa kweli. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kama tutaendelea na utaratibu huu basi mambo mengi yatafanyika na dalili zuri tumeiona katika kipindi cha mwaka uliopita hata mapato yetu ya nchi yameongezeka kwa sababu ule ushauri mwingi ambao tunautoa na sisi Serikali wanaufanyia kazi na ndio maana hili gurudumu sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwa pamoja viti vya mbele na viti vya nyuma naamini hakuna chochote ambacho kitakachoweza kutushinda.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya hili ni tatizo sugu kweli kweli na hii ni vita na nchi inapoingia vita watu wote wanakuwa kitu kimoja bila ya kuangalia mjomba, bila ya kuangalia shangazi yoyote ambae adui aliyekuwepo mbele yenu mnatakiwa mshirikiane kuweza kupambambana nae. Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru jitihada za Serikali zilizochukuliwa hivi karibuni za kuwashika wale wote ambao waliokuwa wanatuhumiwa na kesi hizi za madawa ya kulevya. Wenzetu Marekani Mhe. Mwenyekiti, sheria zao ziko mbali zaidi, Marekani wao sheria zao sio lazima ukutwe na yale madawa yenyewe, Serikali au vyombo vinavyohusika vikikutuhumu kwamba unajihusisha na biashara ya madawa ya kulevya basi sheria yao wao wanapiga *ambush* popote ulipo na tuliona na kushuhudia aliyekuwa *General* wa kule Colombia kama sikosei alikuwa *General* Noriega alikwenda kuchukuliwa juu ya kiti chake cha urais na akenda akadhibitiwa katika masuala mazima ya madawa ya kulevya.

Sasa kitu ambacho ninatoa ushauri Mhe. Mwenyekiti, naomba tutoe elimu sana kwa vijana wetu na hasa vijana wetu au wananchi wetu wanaosafiri safiri. Hivi karibuni kumetokezea kadhia moja nilikuwa nazugumza na Mnadhimu wetu hapa kwamba kuna mtu yeye alikuwa anasafiri anakwenda China, kwa bahati akapigiwa simu na mwenzake kule akamwambia kuna mzigo

utaletewa naomba unichukulie uniletee amepewa begi ile kwa bahati kwa kuwa yeye ni *innocent* hana wasi wasi wowote na yeye akachomeka nguo zake mule mule, kumbe ile begi imeshonewa madawa ya kulevya kwa ndani kufika China kule wamemkamata mpaka sasa hivi yuko ndani. Lakini dada yule anahangaika na jinsi ya kuweza kumtoa sio kitu rahisi.

Kwa hivyo tunatoa wito kwa wasafiri wetu na hasa sisi ambao tunasafiri safiri tukapitia *transit* pale Dubai, Mhe. Mwenyekiti, tena hili naomba mpaka kwa waheshimiwa wenzangu. Kwa sababu mashehe siku zote wanatwambia kwamba nakuhusia pamoja na kuihusia nafsi yangu. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna utaratibu na sio sasa hivi huo muda au hilo tatizo liko muda mrefu au huo utamaduni umekuwa muda mrefu wasafiri wengi wanavyopita Dubai hasa ukionekana kwamba huna mzigo wa mkononi basi unawakuta wafanyabiashara na sisemi hivi kwamba landa ni watu wa madawa ya kulevya, wao wanafanya kwa nja njema anaweza akakwambia bwana wee, hebu naomba nichukulie kilo zangu unisafirishie ukifika Unguja kule au ukifika Dar-es-Salaam utamkuta mtu anakuja kuupokea nzigo ule. Sasa kwa nia njema hata mimi mwenyewe nimeshawahi kufanya, kwa sababu ni watu ambao tuaminiana, unajua Wazanzibari tunavyoishi. Nachukua mzigo ule matokezeo yake sijui mle ndani kuna kitu gani. Sasa kule anakwambia nitakwenda mpaka nitausafirisha mimi mwenyewe. Anakuja anauleta mpaka Uwanja wa Ndege lakini kule Uwanja wa Ndege unakofikia mzigo ule unakuja kwa *TAG* ya jina lako wewe. Waswahili wanasema mkamatwa na ngozi ndio mwizi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa unaposafiri kwenda nje, hata Mheshimiwa mwenzako usikubali kumbebea begi yake, usikubali kumchukulia labda pesa, pesa mchukulie lakini kitu chochote kilichokuwemo ndani ya kifurushi ni hatari. Mhe. Mwenyekiti, tumeshaona katika *clip*. Kuna mwari mmoja Oman pale alitumwa anakwenda kufanya kazi matokeo yake kumbe ule mzigo anaambiwa ampelekee yule anayempelekea ndani kuna madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema suala la madawa ya kulevya ni suala kubwa na ni suala zito na tujitahadhari kabla ya athari. Sasa kitu ninachokiomba, mimi nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wangu wa Mjini Magharibi kwa kweli kazi kubwa anaifanya. Kazi ambayo anayoifanya sisi kama wana wa Mkoa Mjini na Magharibi tunaomba tumuunge mkono, kwa sababu sasa hivi kwa kiasi fulani ukipita maeneo ya Miembeni hata kule kwangu Mboriborini, Mboriborini wamebakia wale tu simba mwitu, ukipita na simu wanakunyakuwa, naomba Mhe. Mkuu wa Mkoa ajitahidi katika eneo hilo.

Lakini katika suala zima la madawa ya kulevya kwa kiasi kikubwa sasa hivi kwa kweli limepungua. Nampongeza sana Kamanda Hassan Nasir, Kamanda Mkadam na Kamishna wa Polisi kwa kweli kazi kubwa wanaifanya kwa kuweza kusaidia katika suala letu hili. Sasa kitu ninachokiomba kwa upande wa serikali. Serikali tunashukuru kwa majibu ya serikali na serikali imekubali kwamba tatizo bado lipo na wateweza kulifanyia kazi. Kitu ambacho ninachokiomba ni mashirikiano. Sisi Waheshimiwa tunapoona tatizo tusisubiri tena Barazani, tunapoona tatizo pale pale tujitahidi tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa upande wa serikali sasa hivi tunajenga Uwanja wetu wa Ndege wa Abeid Amani Karume Terminal II. Lazima kitengo cha Madawa ya Kulevya na Jeshi la Polisi wawekewe sehemu yao maalum ya kuwakafini wale watu ambao walioficha madawa ya kulevya waliyotiwa tumboni. Tuna tatizo la miundombinu, utaratibu wa dunia mtu wa madawa ya

kulevya akishakamatwa uwanda wa ndege hatakiwi yule kuondoka kupelekwa katika kituo chengine, yule anatakiwa mambo yake yote yamalizwe pale pale kama kukafiniwa akafiniwe pale pale atoe vitu vyote uchukuliwe mzigo, unaotakiwa aondoke pale. Kwa sababu ukimtoa kituo kimoja kumpeleka kituo chengine hapa kati kati hapa kuna mambo mengi yanaweza yakafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tumeshashuhudia mtu alikamatwa na madawa ya kulevya kayabeba tumboni yalipokwenda kwa mkemia tukaambiwa saruji. Sisi tulimlaumu Mkemia Mkuu, lakini unamlaumu kitu kilichotoka huko unajua hapa kati kati kilibadilishwa vipi. Pengine madawa ya kulevya watu wametia mfukoni wakatia saruji wakampelekea Mkemia Mkuu. Tunaweza tukalaumiana wenyewe kwa wenyewe watu wenye dhamana zao, watu wenye taaluma zao tukawalaumu lakini kumbe tuna tatizo sisi wenyewe.

Kitu ninachokiomba maana kwa bahati nzuri ule uwanja tunaambiwa (*design and building*) una-*design* na halafu unajenga. Sasa katika *design and building* kama hakijawekwa Kitengo cha Madawa ya Kulevya naomba kiwekwe Kitengo cha Madawa ya Kulevya pamoja na Jeshi la Polisi, ili mtuhumiwa wa madawa ya kulevya asitoke *airport* mpaka mambo yake yote yameshamalizwa kule kule.

Nashukuru sana kwa jitihada ya serikali na naamini katika hili kama nilivyosema tukienda pamoja tutashirikiana. Lakini bado kwa upande wa Pemba naomba sana Pemba bado tuna taarifa kasi kidogo haipo vizuri. Tunaomba Wakuu wa Mikoa kwa upande wa Pemba huko nako kufanyiwe hiyo kazi ili tuhakikishe, mtu ukimuona anasinzia sinzia tu akamatwe mpaka aseme mahali alikoipata tuhakikishe tunamaliza tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo machache niya yangu ilikuwa ni kuunga mkono na kuona kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa umoja wetu tunaumia na hatulipendi jambo hili na tutashirikiana na serikali kuhakikisha kwamba tatizo hili la madawa ya kulevya linaondoka kabisa kabisa ndani ya nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kupongeza sana kuliko kitu chengine nitakachokisema. Nianze na kutoa pongezi nyingi sana kwa serikali. Baada ya kuleta hoja hii binafsi kuna matunda ambayo tuliyaona katika Mikoa yetu na katika mitaa yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii iliumiza watu wengi sana katika Baraza hili. Lakini nishukuru serikali iliona ni kiasi gani wananchi wanaumia na walilichukulia siku ile ile walianza kufanya nguvu za ziada katika suala hili. Baada ya kupitishwa tu hii hoja mitaani kwa kweli kulikuwa na hali tete sana. Wavuta unga, watumiaji madawa mengine kwa kweli walikuwa na hali mbaya sana, hospitali zetu zilijaa watu wanaotumia madawa, afya zao zilikuwa mbovu, arosto nyingi, kwa kweli ilikuwa ni mtihani katika mitaa yetu kutokana na suala hili.

Kwa hivyo nipongeze sana serikali, kwa kipindi kile mimi nasema walifanya kazi zaidi ya asilimia 100 kwa suala hili niwapongeze. Lakini sasa baada ya jitihada zile kunaonekana kwamba kulifanywa kazi nzito sana baadaye ilipunguzwa kasi kwa sababu dawa zile sasa hivi

tunaona tayari zinaanza kuenea tena kwa kasi. Kipindi cha nyuma dawa zile zilikuwa zina bei kubwa sana baada ya kubanwa sana lakini sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, madawa yale bei tayari imeshaanza kupungua na vijana wetu wanatumia sana madawa yale.

Mhe. Mwenyekiti, tukuombe sana na tuiyombe tena sana serikali suala hili sio la kulegeza kamba kwa sababu suala hili bado lipo na zito na linaumiza. Pia niipongeze serikali kwa kusema kwamba watafanya uchunguzi juu ya wanafunzi wote ili waweze kubainika ni wanafunzi wangapi wanatumia madawa haya. Kwa kweli wanafunzi wengi sana wanaharibika tunaona kwamba sasa hivi kiwango cha kufeli kinazidi, ukiuliza tutakaa chini tutasema. Japo tunasema kwamba walimu wana hivi na hivi lakini na suala hili likiingia mashuleni wanafunzi hawa wanapoteza akili zao kwa ajili ya haya mambo ambayo hayana maana.

Kwa hivyo niipongeze sana kufikiria kwenda kwa wanafunzi, kwa sababu tukianza kuwapa elimu wanafunzi naamini kwamba na wao watajifahamu kulikoni kuwasubiri mpaka wakishaanza. Wale ambao hawajatumia watapewa elimu, wataogopa na wale ambao wanatumia baada ya kuona kwamba ah! sisi mpaka maskulini tunachunguzwa naamini wataacha hili suala kuliko kuwaacha tu hivi hivi mpaka wakawa watu wazima wakaja wakawa arosto kali kama mitaani ambavyo tunawaona.

Niipongeze sana serikali kwa kuwaona wanafunzi na kutaka kuwafanyia uchanguzi. Pia nimpongeze sana Waziri wetu wa Katiba na Sheria kwa kweli kafanya kazi nzito katika Mahakama zetu. Tunaona siku hizi mtu akikamatwa na madawa tu kabla hajapelekwa Mahakamani anaanza kutetemeka mwenyewe kwa sababu anajua kwamba sasa hivi suala hili sio la mchezo mchezo.

Mimi niwapongeza kwamba watu wapo wananyimwa dhamana na tunaona kwamba kesi hizi sasa hivi zimeshaanza kwenda kwa kasi kubwa sana tofauti sana na zamani. Zamani ilikuwa kesi hizi zinakwenda unaambiwa tunasubiri ushahidi, mtu unamkuta nje anadunda kama kawaida. Lakini sasa hivi ukienda na madawa ujuwe kwamba tayari wewe umeshakuwa muhalifu mkubwa sana katika serikali yetu. Kwa hivyo nimpongeze sana na kama kuna uwezekano Mheshimiwa achia dhamana mimi naomba mtu akikamatwa siku ile ile ichunguzwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama sasa hivi Pemba unakuta kwamba suala hili linarudishwa nyuma kidogo na Mkemia Mkuu. Mkemia Pemba ni mmoja tu na kiofisi chake ni kibovu sana na Mkemia huyu huyu unaweza ukiaenda wiki nzima ukaambiwa hayupo. Kwa hivyo kwa sehemu hii huyu Mkemia kwanza azidishiwe nguvu ili aweze kufanya kazi kwa haraka kuliko kwenda ukaambiwa kwamba kesi iko kwa Mkemia kwa kweli hapa hizi kesi zetu zinaharibiwa, utakuja kuambiwa bangi mwisho wake utaambiwa ni mchicha. Kwa hivyo nikuombe sana huyu Mkemia kidogo azidishiwe nguvu ili hizi kesi kama ambavyo serikali imetia nguvu naamini kwamba na huyu mkemia akipewa nguvu na sisi tutazidi kufaidi juu ya suala hili.

Pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa tumeona katika Mkoa huu jitihada gani anazichukua wale madada powa na wengine wote sasa hivi wanabanwa hizi biashara hawazifanyi. Kwa kweli ni kazi nzito ambayo wanaifanya, nimuombe na Mkuu wa Mkoa wangu wa Kusini Pemba jema huigwa na yeye pia aige akiiga na sisi tuko nyuma yake tutafanya. Kwa sababu nguvu zake zote atakazozifanya na sisi tukiungana naamini kwamba kitu kimoja tutakifanya na kitaleta faida.

Lakini sasa hivi bado Pemba suala hili bado limelala sana. Hata sasa hivi Ramadhani hii wanazitumia hizi dawa katika majumba ya wauzaji, nenda katika majumba ya wauzaji ambao hawapo siri kwa kweli Pemba hakuna siri Mheshimiwa. Muuza unga popote Pemba si siri kwa sababu kama tuanvyoifahamu Pemba ni ndogo na Pemba sote tunajuana na wauza unga naamini kwamba tunawajuwa ingawa tunawanyamazia.

Lakini niombe sana askari wetu kwa kweli wauza unga wanawajua, Chakechake hakuna siri. Halafu mvuta unga hana siri ukimuhoji tu kidogo umepata wapi hivi na hivi anaogopa anakutajia fulani. Kwa hivyo mimi naomba kwamba wale wanaotajwa wote wakae ndani bila ya kufanyiwa uchunguzi kwanza waonje tu ile nyota ya jiwe ambayo wanaipata wenzao hawa watu wakiwekwa ndani itapungua hata akifanyiwa uchunguzi akijakujulikana kama hajauza basi itakuwa kama ni adhabu fulani tu anapewa. Kwa hiyo niwaombe sana suala hili lizidi kuangaliwa na niipongeze sana serikali kwa kuchukua jitihada zake na sisi tuseme tumefurahi, lakini tunaiomba serikali bado izidishe nguvu hasa Pemba.

Pemba bado madawa yanauzwa kiholela sana na watu wa Pemba, vijana wa Pemba bado wanaathirika sana kwa sababu siku hadi siku watu hawa wanazidi badala ya kupungua. Niwaombe sana Pemba wabanwe, ingawa wenyewe wakisikia wanakuwa wanakasirika. Kwa sababu mimi baada ya kuchangia hapa nilipata changamoto mbili tatu. Lakini nikawambia mimi kufa kwa ajili ya suala hili niko tayari, wameshakufa wengi sana tu itakuwa siyo ajabu mimi.

Nikuombe sana Mhe. Waziri wa hii wizara ukiangalia na wewe pia unatoka Pemba unakuwa unakwenda pale kwenu ukiangalia pale kwenye eneo la nyumba yako pana watu ambao haya madawa wanayatumia. Naamini kwamba unaumia na linakuumiza sana pengine hata katika familia yako yuko mtu ambaye anakuliza kila siku kwa suala hili. Kwa hivyo nikuombe sana tuungane kwa wote mimi na wewe ili tupige vita madawa ya kulevya. Zanzibar bila ya madawa ya kulevya inawezekana. Ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuichangia japo kwa muhtasari, ripoti hii ya majibu ya hoja ya Mhe. Mohammed Said (Dimwa) inayohusiana na Madawa ya Kulevya ambayo iliwasilishwa katika kikao kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mohammed Said Dimwa kwa kuileta hoja ile ambayo kwa kweli inaigusa jamii yetu ya Zanzibar ,Tanzania na ulimwengu kwa ujumla.

Nichukue fursa hii kuishukuru sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na nimshukuru sana Mhe. Mohammed Abou Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuonyesha uungwana lakini vile vile kuwa kufuata Kanuni na Taratibu za Baraza kwa kuileta Barazani majibu ya hoja hii muhimu ambayo hivi sasa ni hoja ambayo imetawala katika mataifa mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba suala la madawa ya kulevya tumelijadili kwa kina, lakini ni suala ambalo bado lipo na tunaendelea kuwa nalo. Japo baadhi ya Wajumbe wameweza kuonyesha kufarijika kupungua kidogo kwa madawa haya katika kipindi hichi ambacho hususan katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi baada ya Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib kuweza kufanya uperesheni za hapa na pale kwa kushirikiana na jeshi la polisi.

Nikweli kwa kiasi fulani kunaonekana kupungua lakini juhudi bado zinahitajika zaidi kuweza kuona tatizo hili linapungua na ikiwezekana kuweza kuondoka kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema mchango wangu hautokuwa mkubwa katika hili lakini nielekee sana katika suala la madawa ya kulevya na kulihusisha na masuala ya rushwa. Kesi za madawa ya kulevya ni nyingi sana na tunazisikia karibu kila wiki au karibu kila siku katika vyombo mbali mbali vya habari. Kesi hizi za madawa ya kulevya huwezi kusifahamu mwisho wake zimefikia wapi. Utazisikia awali zinapokamatwa lakini uendelezwaji wake katika kesi hizi unakuwa huufahamu mwisho wake. Sasa hapa kuna tatizo na ni lazima tuweze kujiuliza tatizo liko wapi. Inaonekana dhahiri kwamba suala la rushwa ndilo ambalo limetawala na kuzifanya kesi hizi za madawa ya kulevya zisiweze kupiga hatua na hapo zikawatia hatiani wahusika wanaokamatwa nayo au wanayohusishwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba rushwa inaviza kesi za madawa ya kulevya nchini na hii sijui ni kutokana na nini. Inawezekana kwamba watendaji wetu wanaohusika na kesi hizi basi roho zao bado hazijakinai na hapa mapambano yatakuwa makubwa zaidi. Kuna suala zima la kuweza kubadilika kwa watendaji wetu katika ngazi mbali mbali tukea ngazi ya Polisi, DPP mpaka katika ngazi za Mahakama. Kama hatujabadilika tusitarajie kwamba kesi hizi za madawa ya kulevya zitakuwa zinapungua.

Mhe. Mwenyekiti, wa ripoti ya hii ambayo tumepewa jana ripoti ya mwaka kuhusu utekelezaji wa kazi kwa kipindi cha Oktoba 13, Disemba 16, ripoti hii imeletwa na Mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar. Katika ripoti hii katika ukurasa wa 19 zimeelezwa tuhuma zilizoongoza kulalamikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mshangao mkubwa katika tuhuma 12, tuhuma namba 11 ya madawa ya kulevya, tuhuma iliyopo ni moja tu. Sasa tutizame tokea 2013 - 2016 tuhuma ya madawa ya kulevya katika kitengo cha rushwa kuna tuhuma 1, sasa tujiulize lazima hapa kuna tatizo. Haiwezekani ndani ya miaka hiyo 13 mpaka leo tuhuma ya madawa ya kulevya kuna tuhuma 1, hii ni hatari. Wakati sisi tunaimba ukubwa wa tatizo hili, Kitengo hichi au hii Mamlaka mimi naona kama ina matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiacha hilo Mamlaka hii hii ambayo ina kesi nyingi sana juu ya tuhuma mbali mbali za rushwa hakuna hata kesi moja katika *speech* ripoti yao ambayo imepata hukumu. Hakuna hata kesi moja iliyopata hukumu, majalada ni mengi lakini mwisho wa habari hakuna lolote ambalo limeendelea. Sasa hapa kuna matatizo makubwa sana yapo, naweza kusema kwamba hii nchi inaongozwa na tuhuma tu lakini hakuna anayeweza kuthibitishwa kufanya kosa. Hapa lazima serikali iwe makini sana na hii mamlaka kwa kweli kama tumeianzisha mamlaka hii kwa kuweza kuzuwia rushwa na wahujumu wa uchumi lakini miaka hii iliyokuwepo hakuna kesi hata moja mimi naona hii mamlaka itazamwe upya uwezo wake. Lakini vile vile inawezekana kama nilivyotangulia kusema kwamba vyombo vyetu vinavyohusika na madawa ya kulevya lakini na kesi mbali mbali za uhujumu uchumi bado zinatawaliwa na rushwa na hii rushwa bado ni kitandawili kwamba hakipati ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika vyombo vya habari utasikia kwamba askari kategewa mtego akakamatwa kapewa rushwa *red handed* lakini kesi ile huwezi kuja kuisikia imemalizikia vipi, sasa seuze kesi hizi za madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, la kushangaza vile vile Mkurugenzi huyu huyu wa Mamlaka anaingia katika Tume ya Madawa ya Kulevya kwa nini tumemuingiza mule, tumemuingiza kwa lengo la kusaidiana na tume hususan katika swala la rushwa kuendana na madawa ya kulevya lakini tuhuma iliyopo ni moja tu, hapa kuna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naona itakuwa tunajidanganya sana, tunajidanganya sana kuwa unazungumzia swala la madawa la kulevya na kesi nyingi zinakufa kwa rushwa lakini tuhuma iliyokuwepo ni moja katika miaka yote hii, hapa kuna tatizo na mimi ningeomba sana Serikali kuweza kuchunguza tatizo hili ili kuweza kuona kwamba tunapiga vita kikweli kweli madawa ya kulevya. Kesi ni nyingi kila siku lakini hakuna kesi ambayo inapata ufumbuzi lazima tuzipunguze hizi tuhuma hatuwezi kwenda na nchi hii kwa tuhuma tu lazima tufikie pahala tuhuma hizi ziweze kupata suluhusho basi matatizo mengi yanayohusiana na madawa ya kulevya na hata wahujumu wa uchumi yanaweza yakapungua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli nimeguswa sana na suala hili kwa sababu ndani ya kila familia basi utakuta kwamba kuna muathirika wa madawa ya kulevya. Naomba sana tushirikiane ndugu wawakilishi, viongozi mbali mbali tuwe kitu kimoja kuweza kuona kwamba tunapiga vita madawa ya kulevya lakini tuwache muhali na suala la rushwa kwa kweli hivi sasa lifungiwe njuga kuweza kuona kwamba halina nafasi kwa sababu hili ndio ambalo linavuruga kesi zote za madawa ya kulevya tokea chini.

Baada ya mchango huu Mhe. Mwenyekiti mimi naunga mkono Ripoti hii ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wamejitahidi na tuendelee kushirikiana na kuunga mkono kitengo hiki pamoja na Tume hii ya Kuzuia Madawa ya Kulevya ili tuweze kuona kwamba nchi yetu inabaki salama.

Ahsante sana Ndg. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid mchango wako mzuri umeonesha jinsi ulivyoathirika na hoja hii, sasa namwita Mhe. Ali Suleiman Shihata na baadaye Mhe. Said Soud ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kuchangia hotuba hii muhimu au taarifa hii muhumu juu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Ongozeko la Uingizaji na Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuliona hili suala zito na leo tukaletewa majibu yake na mambo ambayo matarajio ya kuona kwamba huko mbele tunakokwenda hili suala linabakia historia halipo katika nchi yetu. Lakini nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa taarifa hii nzuri aliyoileta hii kuhakikishia kwamba nchi yetu viongozi wake wako imara na tunafanya kazi kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya Zanzibar ni visiwa kuna visiwa viwili vikubwa Unguja na Pemba na visiwa vidogo vidogo, kwa mtazamo huo kazi ya ulinzi wa visiwa hivi ni ngumu na vita hivi tunavyopigana katika nchi yetu ni vikubwa. Kwahivyo, kuna wavuvi wa aina kwa aina wanaweza kuingia kwa njia wanazozijua wao, hasa tukizingatia kwamba mvuvi Zanzibar Unguja na Pemba anaweza kwenda kuvua Bagamoyo, Tanga na kwengineko Dar-es-Salaam, siku nyengine Mwenyezi Mungu atunusuru huko anakokwenda kapata vitu vyake kaweka katika dhana zake kwenye uvuvi hawezi kumjua mtu. Mvuvi karudi baharini anajulikana yuko salama kumbe huko ndio kwenye soko la kuja kuhatarisha vijana wetu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika nchi yetu kuna aina kwa aina ya udanganyifu au ya utaalamu wa kazi hizi za kuingiza madawa katika nchi yetu kwanza tukiri kwamba hili suala lipo na lionaendelea. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali tukazingatia kwamba tuwe na vifaa bora na vya kisasa, ambavyo vinaweza kumujuwa mtu kwa njia fupi kabisa akiingiza au akitoka kwasababu watalaamu hawa wa kuingiza madawa ya kulevya wana njia nyingi za kudanganya jinsi waweze kuingia na madawa hayo na kuharibu watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, usafirishaji wa dawa za kulevya nimesema mapema tuu kwamba kuna njia nyingi na hasa tukizingatia Zanzibar tumezungukwa na bahari, kuna bandari bubu nyingi katika nchi yetu hizi naamini kwamba bandari bubu hizi wanaweza kuzitumia wajanja hawa kwa njia zao za mkato na kuhatarisha uingizaji wa madawa katika nchi yetu. Kwahivyo, naiomba serikali kabisa tuwe na dhamana ya kuhakikisha kwamba ulinzi unaongezeka hasa katika madiko yetu. Madiko maana yake bandari ndogo ndogo hapo kidogo tunaweza kuleta usalama na kuhakikisha kwamba watu wanaishi salama katika nchi hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwamba katika ripoti hii au taarifa hii bahati nzuri ina wajumbe wengi sana na wajumbe hawa ni uti wa serikali yetu, na nakiri kwamba kama itafanywa kazi kweli kweli bila ya kutumika rushwa, basi naweza kusema hili suala linaweza linaweza kuondoka. Lakini katika nchi yetu tukiri kwamba rushwa ni adui wa haki na mwenye kutowa rushwa ndio anayepata haki. Kwa hivyo ningeiomba serikali hili tuliangalie rushwa ni hatari na rushwa ni adui wa haki katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu niwasome wajumbe hawa katika tume hii. Wafuatao ni wajumbe wa Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar pamoja na Taasisi zao.

1. Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, ujuwe ni tume kubwa
2. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni Mjumbe ambaye ni Makamo Mwenyekiti,
3. Waziri anayeshughulikia masuala ya Afya - Mjumbe
4. Waziri anayeshughulikia Vijana, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto - Mjumbe
5. Waziri anayeshughulikia Elimu - Mjumbe
6. Waziri anayeshughulikia Bandari na Viwanja vya Ndege - Mjumbe
7. Waziri anayeshughulikia Utalii - Mjumbe
8. Waziri anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Idara Maalum - Mjumbe
9. Waziri anayeshughulikia Sheria - Mjumbe
10. Mkurugenzi wa Mashtaka - Mjumbe
11. Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar - Mjumbe

12. Kamishna wa Polisi Zanzibar - Mjumbe
13. Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa - Mjumbe
14. Naibu Mkurugenzi wa Forodha Zanzibar - Mjumbe
15. Mkemia Mkuu wa Serikali - Mjumbe

Na wajumbe wawili ambao watateuliwa na Waziri husika hapo baadaye ambao ni:
16. Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Rushwa - Mjumbe
17. Katibu Mkuu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Mjumbe
18. Mkurugenzi Mtendaji wa Tume - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, serikali yote ipo hapa na hili suala si dogo la kitaifa. Naamini kwamba kama kweli na naamini itakuwa kweli maana Mhe. Rais hili suala analipiga vita na wananchi wake wote pamoja na sisi mimi nilokuwepo hapa na wenzangu waliokuwemo humu, hili si suala la masihara hivi ni vita vikubwa mimi naweza kutoa pongezi rasmini kwa Serikali ya Muungano, mheshimiwa likifanyika zuri popote tulisifu hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likiwa jema Bara na hapa liwe jema nalipongeza Jeshi la Polisi Tanzania kwa kuharibu mashamba makubwa maekari kwa maekari ya bangi lakini pia kuzuiya madawa ya kulevya siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, vita vimepigana vizuri leo Tanzania Bara unahakikisha kwamba kwa asilimia imekuwa salama baada ya kuhakikisha kwamba Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya, Jimbo kwa Jimbo, Shehia au Kata kwa Kata nimuombe sana Mhe. Waziri hili suala Wakuu wetu wa Mikoa ni watu wa kwanza kuhakikisha kwamba ni ngao yetu. Nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini pia Wakuu wetu wa Wilaya na Shehia zetu pamoja na bado kadhia ndogo ndogo imo, lakini nampongeza Mkuu wa Mkoa kwa kuonesha mfano naiomba serikali itowe wito kwa Wakuu wa Mikoa mengine. Tuna Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkoa wa Kusini Unguja, Kusini Pemba, Kaskazini Pemba tufanye kazi hii kusaidia jamii yetu isiangamie. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wanakufa, wanakosa uwezo wa kufanya kazi, wanakuwa wezi. Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi yumo Mhe. Mwakilishi humu siwezi kumtaja jina lakini huko mbele mawaziri sitaki kumtaja, nilipita kule Muyuni wanasema shamba la Mhe. Mwakilishi fulani limeibiwa mihogo yake yote, yupo hapa hapa na mwenyewe ananisikia.

Kwahivyo, hii ni kadhia ambayo ipo na inaeleweka leo Mhe. Mwenyekiti ukenda Paje, Kizimkazi, Nungwi, Michamvi, Kiwengwa, Uroa, Bwejuu mashaka makubwa yamo Mhe. Mwenyekiti ya unga na bado utasikia tu katika ripoti mpaka sasa hivi tumefika salama watu hawa ushahidi haupo, ushahidi ushapatikana ushakamatwa.

Lakini pia katika taarifa hii nisikitike kidogo ukurusa wa tatu, ukurusa wa tatu Mhe. Mwenyekiti pana *paragraph* hii inasema hivi kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu: "Mantiki ya kanuni za kutafautisha viwango vya dawa za kulevya, kumtambua mfanyabiashara wa dawa za kulevya, na mtumiaji wa dawa za kulevya na kuzuwiya dhamana kwa wale wote watakaokutwa na viwango vikubwa vya dawa za kulevya. Aidha kanuni hizi zitasaidia kuzuwia dawa za kulevya kutokurudia tena mitaani, na pia kuzuwia uharibifu wa kesi za dawa za kulevya kutokana na upotevu wa vielelezo pamoja na kuharibu vielelezo hivi".

Hapa nashangaa Mhe. Mwenyiti, kifungu hiki nakisikitia sana, kwasababu akikamatwa huyu mkubwa huyu mdogo akikutikana nacho kakipata wapi. Mhe. Mwenyekiti, naomba adhabu ya hapa yoyote hata kama mtoto mchanga kakamatwa nayo akamatwe asitolewe. Kwasababu akipewa dhamana huyu anakwenda kuchukuwa kwa yule mkubwa wake mwengine alompa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba adhabu iwe adhabu haina au sheria haina mkubwa, sheria inakwenda kutokana na utaratibu wa nchi ulivyopangwa, kaharibu mkubwa na mdogo kaharibu pia kavunja sheria. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili, hivyo kifungu hiki dawa za kulevya anaekutwa nazo yoyote asitolewe wala asipewe dhamana hapo tutaishi salama katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, najuwa unaangalia muda, kwa taarifa rasmi tu kwamba hivi sasa hivi walaunga wengi tunao katika mitaa yetu na katika Jimbo langu la Kijitoupele wamo. Kwahiyo, naiomba serikali kwamba kamati hii ifanye kazi za ziada kupita katika maeneo na ikitaka kupata ukweli isiwatafute masheha, isiwatafute nani, wananchi wema wamo tele katika mitaa yetu wawaelekeza walipo na si vyema kama tunatumia maaskari wetu wakenda na *uniform* hawawapati hata siku moja, wawatumie watu wa kawaida tu, wanakwenda eneo fulani hii kazi inafanyika wala haina kificho yaani, haina kuficha iko wazi kabisa.

Kwahivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri hii ni taarifa nzuri na taarifa hii ni kubwa serikali yote iko hapa, wizara zote kwasababu ukienda wanawake na watoto Mhe. Waziri ndiye anayeshughulika na vijana wetu, kinamama na watoto, lakini pia Afisi ya Makamu wa Pili tunao walemavu wanaathirika na watu wengine, pili na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yeye ndio wanafunzi wote anao yeye na huko huko katika skuli zetu utasikia tu watoto fulani wanakwenda pale kama wana usingizi wamelala wakati wanasoma, kumbe wametumia madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza serikali kwa hili, naipongeza kamati hii lakini kamati sitoipongeza mpaka ifanye kazi zake vizuri. Lakini naipongeza serikali kwa kuandaa hili, na naamini azma ya serikali kuundwa kamati hii ni kuleta faraja na amani katika nchi yetu madawa ya kulevya yasiingie, ili kunusuru vizazi vyetu tulivyonavyo na vijavyo.

Baada ya hayo, Mhe. Mwenyekiti naunga mkono taarifa hii naitakia kheri na Mwenyezi Mungu aijalie tufanye kazi zetu kwa salama ya nchi yetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa ninamwita mchangiaji wetu Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) na baadaye Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nitampa dakika tatu iwe ni mchangiaji wa mwisho kwa hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii na kueleza namna gani serikali imechukua hatua katika kupambana na hoja hii. Hoja hii ni nzito sana, lakini ni hoja ambayo kwa mshikamano wa wananchi wa Zanzibar na Watanzania wote naamini wazi kwamba hoja hii tunaweza tukashinda vita hivi.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikurupuki tu kufanya mambo bila ya kuzingatia kitabu hichi. Kwakweli ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilikwishaona udhaifu mkubwa wa madawa ya kulevya, madawa ambayo yanaathiri nguvu kazi na yanaharibu utaifa wa Tanzania katiki kujenga taifa jipya ambalo linategemewa baadae.

Kama tunavyoelewa vijana wetu wengi wameathirika, lakini sababu ya msingi inatokana na kwamba watu walikuwa hawana uwezo wa kufahamu nini athari ya madawa ya kulevya. Lakini kwa uwezo wa Chama cha Mapinduzi ambao wao hawakukurupuka kusimama ni kupiga vita madawa ya kulevya, bali walikwisha ona athari yake na kweli wamepambana nalo hili wametoa agizo na serikali zote mbili zinatekeleza agizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka jana kuna gunia mia moja na sitini (160) za madawa ya kulevya zimekamatwa Arusha huko katika mazingira ya serikali kupambana na madawa ya kulevya. Halikadhalika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo ina watu maalumu ambao tayari wanawachunguza, na kuwapeleka mahakamani pale ambao utaratibu wa ushahidi utapatikana hatua kali zitachukuliwa. Hii ni kwani, kwasababu tayari wamekwisha ona CCM kwamba tusipowajenga vijana katika maadili, tusipowaweka vijana katika mstari tutakosa nguvu kazi.

Sasa kabla ya kuelezea yale ambayo yameelezwa humu, Mhe. Mwenyekiti naomba kuchukuwa nafasi hii kuwambia wawakilishi wote wa Unguja na Pemba, kwamba ni wajibu wetu kusoma ilani hii na kuwasomea wananchi wakafahamu yaliomo katika kitabu hiki, tukiyafanya haya kwa umakini na ukweli kabisa tukaona *reality* ya uhakika ninahakikisha mwaka 2020 CCM itashinda tena na mtarudi tena. *(Makofi)*

Lakini lazima kitabu kisomwe kwa umakini, na msione haya kukisoma kitabu hiki kwenye magogo, kwenye minazi, kwenye mazungumzo, kwenye mabao ya karata kisomeni kitabu hiki. Hiki kitabu ni kitabu kilichofanya uzalendo wa Wazanzibari namna ya kuendesha nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie kupitia vyama vyetu sisi vya upinzani hakuna maneno yaliyomo humu, kuna maneno ya kudanganya tu Zanzibar tutaifanya Singapore, sijui nitaleta meli, sijui kitu gani yaani, ni maneno ya kudanganya danganya tu, lakini humu yamo maneno ya uhakika, kama una akili yako timamu basi maneno haya ni maneno ya uhakika. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa Unguja na Pemba tumieni kitabu hiki katika kutafuta ushindi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kidogo tu yakuwakumbusha wananchi wa Zanzibar, Waheshimiwa Wawakilishi waliomo katika Baraza utekelezaji uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kitabu hiki.

Kwanza, kuendeleza na kuimarisha mashirikiano miongoni mwa vyombo vinavyosimamia mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kitabu hiki kinasema sio mimi, ni kitabu hiki. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunaona sasa hivi majeshi, polisi, usalama, mgambo wote tunapambana, kwa ajili ya kuzuia madawa ya kulevya.

Pili, kushirikiana na taasisi za kimataifa zinazoendesha mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, ili kudhibiti usafirishaji na biashara haramu za madawa ya kulevya, hivyo bila ya kujali mipaka ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, ndio pale tunapoambiwa kwamba kuna Watanzania hutiliwa dawa za kulevya kwenye mabegi wakakamatwa Ulaya huko, na wanakamatwa kwasababu gani? Wanakamatwa kwasababu hiki kitu si kizuri. Kwahivyo, ni wajibu wetu kuelimisha watu kwamba sasa hivi hata mtu akikupa noti nichukulie basi zipekue kwanza hamna vitu humo, usichukue tu kwasababu ni pesa aah! Inawezekana hizo pesa zimewekewa vitu humo. Hivyo, zitizame kwanza usije ukakamatwa na mzigo huo pesa hazina maana nchi hii, madawa ya kulevya ndio yanayotafutwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendeleza mapambano ya Chama cha Mapinduzi dhidi ya madawa ya kulevya, demokrasia na utawala bora ni moja ya nyenzo muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010/2015 mafanikio yafuatayo yamepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, programu maalum, elimu ya uraia juu ya sera ya utawala bora na haki za binadamu imeandaliwa na kutekelezwa, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa imeanzishwa na kuanza kazi. Aidha, kanuni za kudhibiti rushwa na uhujumu uchumi zimeandaliwa na kuanza kutumika. Kazi ya CCM hiyo. *(Makofi)*

Pia, mafunzo juu ya mapambano dhidi ya rushwa yametolewa kwa wafanyakazi na viongozi mbalimbali wa serikali, kazi ya CCM hiyo. Ujenzi wa jengo jipya ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ofisi ndogo ya wanasheria Mwera na nyumba za waendesha mashtaka wa Mahakama za Wilaya ya Makunduchi, Mkokotoni Unguja na Madungu Chake-Chake Pemba umekamilika. Kazi ya CCM hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kupambana na madawa ya kulevya CCM inafanya kazi hii. Ujenzi wa jengo la Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyopo Unguja na lile la Wete Pemba umekamilika. Aidha, mafunzo ya ukaguzi kwa kuzingatia thamani na mazingira yametolewa kwa wafanyakazi kutokana na juhudi hizo, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sasa imefikia kiwango kinachokubalika kimataifa. Kazi ya CCM hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa nini basi, kwasababu tunataka kuchimba mafuta, tukichimba mafuta vijana kama wameathirika itabidi tuagize nje. Sasa lazima tuhakikishe kwamba wale vijana wetu wanadhibitiwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakuja kufanya kazi yake vizuri, ili mapato ya nchi hii yatumike ndani ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala zima la mapambano dhidi ya madawa ya kulevya hilo halina mjadala. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunasema kama serikali tuna uhakika kabisa mtu yeyote atakayekamatwa na madawa ya kulevya, basi tuna uhakika kwamba mtu huyo hawezi kupewa dhamana, na kwa nini hawezi kupewa dhamana? Kwasababu hiki kitu ni kitu kinachopigwa vita katika Tanzania pamoja na dunia. Kwahiyo, sisi kama Tanzania ni sehemu ya dunia na lazima tushirikiane na mataifa mengine.

Vilevile, nachukua nafasi hii Mhe. Mwenyekiti kumpongeza sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kusimamia suala zima la madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu ili nchi yetu ifikie hatua ya kimataifa tuondoshe muhali juu ya suala zima la madawa ya kulevya, tusejenge muhali kwa serikali iko tayari usiku na mchana. Mhe. Mwenyekiti, ninahakika ukifika kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ukimwambia kwamba kuna mzigo unakuja wa madawa ya kulevya, basi yuko tayari kutoa *battalion* nzima ili yakadhibitiwe madawa ya kulevya. Kwakweli, ninahakika yuko tayari, kwasababu yakutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa huu ndio muongozo wetu, ikiwa kweli tuna imani na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar twende na ilani hii ya uchaguzi, kama kweli tunataka kurudi tena kwenye Baraza hili, twende na ilani hii ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuona sasa niwape nafasi wenzangu pia ningetaka kuchukua nafasi hii kuwaambia kwamba wasikubali kuyumbishwa na visera sera vyengine vya vyama vyengine, viilani vya vyama vyengine, hapa bwana ndio kiboko yao. Hii ndio kiboko ya sera, hii ndio kiboko ya ilani na nasema hivi vyama vyote visikie Tanzania. Nasema kwa uhakika kabisa nimepitia sera na ilani za vyama vingi na mimi mwenyewe nikiwa Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Tanzania, sithubutu kutunga sera kama hizi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hiki kitabu kimetungwa kwa uhakika na nawapongeza wale wote walioshiriki kutunga chombo hiki, mimi mwenyewe sipati usingizi kama sijaipitia hii, na nafanya hivi kwa maana ya kutaka kuona hivyo kweli kuna sababu gani ya nchi hii kutopiga hatua ya maendeleo kama tunatekeleza kweli sera hizi. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu tupige mstari hayo yaliyopita tukamate ilani ya uchaguzi tuongoze kuijenga Tanzania na Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, humu mna mambo mpaka ya Konde, Gando, Wete, Chake-Chake, Mwera, Simiyu, Morogoro, Mwanza yote yamo humu, sio kama maana yake hiki kiilani labda kimechukuliwa kimefanya labda Pemba mbali, Unguja mbali hamna ni Tanzania, hii CCM inaongoza Tanzania, sasa Tanzania imeingizwa humu. Ikiwa wewe unakaa Makunduchi basi Makunduchi imo humu, ikiwa unakaa Micheweni, basi Micheweni imo huku, ikiwa wewe unakaa Chwaka basi Chwaka imo humu hebu soma upate kujua humu mna nini, ikiwa unakaa Tumbatu basi humu imo.

Kwahiyo, sasa soma upate kujuwa nini cha kuwafanyia wananchi, ili ujiandae usingoje yale maneno ya kudanganywa kwamba Zanzibar tutaifanya Singapore, Zanzibar sijui kutakuwa na nini hayo maneno achaneni nayo ni maneno ya kitoto kabisa, na siku zote tumbili akikosa zile zabibu nyengine husema hazijawiva, ndio kawaida yetu hiyo. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hili ndio jembe la kufikia pahala pakubwa pakuiongoza nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, naipongeza sana serikali kwa hatua za kupiga vita madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum). Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeshapata mchangiaji na mchangiaji wa mwisho kwa hoja hii kwa leo, kwasababu tuna hoja nyengine huko mbele yetu inataka kujadiliwa nayo, ili wale

ambao watakuwa na maoni mengine wanaweza kupeleka kwa maandishi kwa Mhe. Waziri. Lakini kwa mchangiaji wa moja kwa moja namkaribisha Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa dakika tatu kama alivyoniomba.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa michango yao mikubwa ambayo wawakilishi wameshaisema, lakini pia kuona umuhimu wa jinsi gani wawakilishi wamekuwa wakiona hoja nyengine ziongezwe ili ziweze kufanyiwa kazi vizuri. Kwa hiyo, naendelea kumpongeze sana Mhe. Mohammed Said Mohammed pamoja na wengine wote waliochangia. Lakini pia niipongeze serikali kwa jitihada inayofanyika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba madawa ya kulevya yanapigwa vita.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii tena kwa kusema kwamba zamani kulikuwa na lugha ambayo inazungumzwa ilikuwa ni MTAMBUKA ni lugha ambayo ya mapambano ya siku nyingi ambayo tumekuwa tukizungumza, mapambano yaanze na vijana wenyewe. Kijana mwenyewe akiamua akajitambua kwamba nikitumia madawa ya kulevya nitakuwa kama fulani ambaye ni arosto yuko tayari mitaani anaweza kuacha, kwasababu utashi uko ndani yake mwenyewe kijana.

Kwakweli, tayari alishawaona wenzake wanaumia anaona jinsi mwenzake alivyo anaendelea kuwa katika hali mbaya, lakini inakuwaje yeye mwenyewe anakwenda kujaribu kile kitu. Ingekuwa kama kila kitu kinajaribiwa mbona kuna wakati mwengine hatuwezi kuthubutu kujaribisha kula sumu, mbona hawajaribishi sumu za panya wanajua wataishia kufa. Lakini haya masuala anasema ngoja ajaribu waangalie itakupaje starehe na nini, na akijaribu kwa nini anaendelea kujaribu kila siku, atasema nataka nitoe mawazo. Anatoa mawazo hayo mbona siku ya kwanza hayajaisha siku ya pili yamerudia mawazo tena na umeendelea tena.

Kwahiyo, natoa wito kwa vijana kwamba tusiendelee kutumia madawa ya kulevya au kujaribu kutumia dawa za kulevya sio mbaya kwa matumizi ya kila kitu, yanapohitajika kutumika mahospitali kwa ajili ya kuwalaza watu wafanyiwe operesheni ili wasisikie maumivu hayana tatizo. Lakini yanapotumiwa vibaya ndio pale yanapoleta hatari katika maisha yetu.

Kwamaana hiyo, kitendo hiki tuendelee kupambana kabisa kwasababu hivi sasa tuko katika mtizamo wa kutaka kuweza kuwa na viwanda mbalimbali katika nchi yetu. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jonh Pombe Magufuli na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein ana mawazo ya kuanzisha viwanda mbalimbali ambavyo vyengine tayari vipo. Tuna kiwanda cha sukari ambapo kwenye viwanda mara nyingi kunakuwa na mambo mengine yanajitokeza hata pamoja na *spirit*. Sasa kama vijana wakiwa tayari wana tabia za kutumia madawa ya kulevya wakienda kwenye viwanda vile wakikosa wanaweza kutumia hata *spirit* wakaendelea katika masuala ya ulevi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ni jambo ambalo linazungumzwa siku zote kwamba hata ukinywa dawa ya kifua unashauriwa kwenye boksi la dawa ya kifua kwamba unapokunywa dawa hii usiendeshe gari, usiendeshe pikipiki, usishone charahani, usikae karibu na moto kwasababu dawa ile inaweza ikakulevya, seuze pale unaichukua dawa yenyewe ukaanza kuitumia kwa ajili ya matumizi, kitu ambacho kitatisha waajiri kuona kwamba mtoto ambaye anakuwa na dalili za

madawa ya kulevya hawezi kuajirika. Kwahiyo, tunaendelea kusema kwamba ajira hazipo wakati sisi wenyewe tunaendelea kujiandaa katika masuala ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitoe wito kwa wazazi ambao wanahusika moja kwa moja na watoto, pale unaposikia mtoto wako anaambiwa na jirani au watu wanasema kwamba mtoto huyu siku hizi tabia zake si nzuri au mtoto huyu siku hizi anaonekana kuchukua madawa ya kulevya. Badala ya kunyamaza kimya na kuweza kusema mwanangu anasingiziwa tuweze kuchukua hatua za mapema, ili kuwasaidia vijana wetu.

Kwakweli, sidhani kama kila mtu ataweza kukusingizia, na pia wanapoanza kuwa na tabia za kupewa pesa ndogo ndogo wanaona matumizi ya mapesa. Kwahiyo, wanataka wapate matumizi makubwa, na hao wauzaji wa madawa ya kulevya maisha hawatafuta familia ambazo wanahisi kwamba wakizituma hazitaleta pesa kwao. Watajitahidi watafute familia ambazo ni kubwa ambazo leo na kesho akikwambia nenda katuletee kitu fulani ataleta kwa urahisi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanaoathirika eti wanasema kwamba suala la kuonja, tusiweze kutaka kuonja onja vitu visivyofaa. Mhe. Mwenyekiti, wazazi sasa hivi karibu na sikukuu naomba kutoa wito, sasa hivi ni muda mrefu ambao mwezi mtukufu wa Ramadhani ulikuwa kwa salama na amani na mnaendelea kumaliza wakati mzuri, umesaidia sana kupunguza joto kubwa sana la masuala mengi ambayo yalikuwa yanatokea kipindi kilichopita. Kwahiyo, nawaasa wazazi wawe karibu sana na watoto weo mara tu watakapokuwa wanaanza kwenda kwenye sikukuu kuhakikisha kwamba wanakwenda na watu ambao watakuwa karibu na sisi tuweze kuwadhibiti kwa karibu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana watumishi wa Mungu ambao wamekuwa wakitoa mawaidha mazuri katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, ambacho kimesaidia sana kupunguza joto la watoto kufanya mambo mengi ambayo yasiyokuwa mazuri. Lakini niseme tu kwamba zamani kulikuwa na lugha iliyokuwa inazungumzwa kusema kwamba, ukinywa kinywaji unasema kuna maziko ya saa nane. Ilikuwa ni pombe za kawaida ambazo zinatengenezwa lakini kwa njia ya *spirit* akinywa huyu mtu hachukui muda saa nane ameshafariki. Tuendelee kuwakumbusha watoto kitu hicho kwamba ni kitu kibaya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kwenye suala zima la kuvuta watakapoingia kwenye viwanda vya mafuta, mafuta kuna mambo mengi sana yanatokezea ambayo yanasababisha kuwe na vitu ambavyo vinaweza kuwa ni vivutio vya kulewa. Tunajua huko nyuma watoto walikuwa wanavuta hata *petrol* sasa kama tunakuwa na mpango wa kutaka kuanzisha viwanda na Mungu akitujaalia tukapata mafuta, vijana hawa watakuwa hawawezi kuajirika wakionekana kuwa wameathirika kwa namna moja au nyengine itakuwa sio nzuri. Vilevile, sasa hivi utaona kwamba kipindi hicho walikuwa na masuala mengine, lakini hivi sasa kila siku kunakuwa na *advancement* ya matumizi ya madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, yameanza kwa kuonja, yameanza kwa kutumia sasa hivi yameingia kwenye sindano na hatujui kesho na keshokutwa yataingia katika njia gani.

Naomba tutokane na masuala haya tusipende kutoa pesa kwa watoto kila wakati kuwapa pesa kwa matumizi madogo madogo pasipokujuwa mtoto anakwenda kutumia nini, kwasababu pale

anapokuwa na pesa anakuwa na kishawishi cha kuona kwamba anaweza kushawishiwa akanunua vitu hasa wanapokuwepo maskuli. Kwahiyo, nawaomba akinamama kwa hali na mali kwa jinsi yoyote tuliyonayo tusipende kuwapa watoto pesa badala yake tuwalishe mapema kabla hawajenda skuli, kwa hali zetu hizo hizo za umasikini, wale mapema wakiwepo majumbani, ili watakapokwenda sehemu za skuli wasiweze kununua peremende, wakanunua vitu ambavyo vingi vinategeshewa kwa ajili ya madawa haya.

Mhe. Mwenyekiti, pia nawaomba na wafanyabiashara watakaokuwa karibu wapende taifa lao wasiwafundishe watoto au wasiwauzie vitu ambavyo ni hatarishi kwenye maeneo ambayo yanazunguka maskuli, kwasababu wakifanya hivyo wao wanajua kabisa wanahitaji watu wazima baadaye watakaowachukua na watakaorithi utajiri wa nchi yetu. Hivyo, wakiwaumiza wote kwa faida ya leo kuona kwamba wao wanatajirika inakuwa haina maana.

Mhe. Mwenyekiti, pia nipende kusema kwamba tunaendelea kuwatia moyo viongozi wa serikali katika suala zima la kupiga vita madawa ya kulevya. Napenda kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na afisi yake katika suala zima la kupinga madawa ya kulevya, ni jana tu tuliona watoto walivyokuwa wanasheherekea masuala ya sherehe hizi wale waliokuwa ni watumwa wa dawa za kulevya walivyokuwa wanaonekana kabisa wamependeza na wana nia ya kutaka kuacha. Nafikiri tuwatie moyo wakitoka kwenye madawa yale tusiwatenge tuwapende na tuendelee kuwashauri na kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mhe. Mjumbe, kwamba tuendelee kushikamana, ili tuweze kuendeleza nchi yetu vizuri. Ahsateni sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, aidha naomba niwashukuru sana sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote na hususan wale waliochangia hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ruhusa yako naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe saba waliochangia hoja hii.

1. Mhe. Mohammed Said Mohammed
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Ali Suleiman Ali
6. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
7. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kunisaidia kazi hii kwa kueleza vizuri yale yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyasema. Lakini pia

niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwasababu wote walionyanyuka kuzungumzia hoja hii, waliipongeza serikali kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo kati yetu na Baraza hili tukufu na katika kupambana na tatizo hili kubwa na gumu. Kwahivyo, nataka kuwashukuru sana na niwaambie kwamba tunazipokea pongezi na shukurani hizo na zote hizi zinazidisha kututia kasi na kutupa moyo wa kutenda wajibu wetu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tatizo hili ni sugu na ni vita vikali, lakini kutokana na mashirikiano yetu ya pamoja naamini sana tumeanza vizuri na tutaweza kuikamilisha kazi hii ya mapambano. Nataka nipokee ushauri sana kwa Waheshimiwa Wajumbe waliosema kwamba tuendelee kuzidisha kasi tusirudi nyuma na pia Pemba ambako kasi wanaiona bado iko ndogo nayo tuizidishe kwa *speed* zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tumejipanga kupitia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kasi itaendelea. Juzi tulitoa tamko rasmi wakati tunaadhimisha siku hii ya madawa ya kulevya duniani, kwamba shughuli hii operesheni zake sasa zitaanza kwa kasi iliyo kubwa zaidi. Pia tukawaomba wananchi wote tushirikiane na pale hatua zinapochukuliwa wasije kuwaombea wale ambao wameguswa katika mkondo wa sheria, waache sheria ichukue nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea kuwa wasikivu sana kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na maoni yao na maelekezo yao. Kwakweli, tunajenga nyumba moja kadiri wanavyotushauri ndivyo tunavyopokea na sisi tunaamini ushauri wao na miongozo yao inakuwa dira katika utendaji wetu wa kazi. Tunawashukuru sana Waheshimiwa na hongereni sana. *(Makofi)*

Nataka na mimi niungane na Waheshimiwa Wajumbe kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi nzuri anayoifanya ya mapambano haya. Mhe. Mwenyekiti, juzi tu, tulimpongeza na tukamhakikishia kwamba tutampa *certificate* maalum kwa mapambano yake na wakati huo huo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameridhia kwamba naye awe mjumbe wa kualikwa katika Tume ile ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya, ili azidi kupata maoni mbalimbali ya kuweza kuendeleza mapambano haya.

Kwakuwa, tayari Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alishatuagiza tuwaambie Wakuu wa Mikoa wote waunge mkono jitihada alizofanya Mkuu wa Mkoa mwenzao wa Mjini Magharibi. Kwahivyo, pamoja na wito uliotolewa na wajumbe hapa napenda kuwaambia Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wa mikoa yote waendeleze mfano hu mwema ambao Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ameuanzisha. Mhe. Mwenyekiti, na wao tutawapelekea barua zao rasmi kama tulivyoagizwa na Mwenyekiti wetu wa tume hii, ili kila Mkuu wa Mkoa ashiriki kwa ukamilifu wake katika mapambano haya. Haya ni mapambano yetu sote na tuna wajibu sote kushirikiana katika kupambana nayo.

Kuhusu kutoa elimu kwa umma Mhe. Mwenyekiti hili ni wazo zuri, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba tutazidi kuliendeleza na hususan kwa vijana. Ni kweli upo umuhimu kwa wananchi kuelewa na vijana kuelewa, lakini kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba kwenye kuelewa pia kutasaidia kuepukana na makosa, kwasababu ni kweli sisi Wazanzibari tunao muhali na imani yetu mtu anakuja anakwambia mzigo wangu huu leo nasafiri kwenda Dubai au mahala pengine nichukulie umpelekee fulani huko, pengine

anakupa ki-*packet* cha haluwa kumbe ndani yake kuna madawa ya kulevya ama unaweza kupewa mzigo wa aina yoyote.

Kutokana na hali hiyo, ni vizuri kukataa kuchukua mizigo, ni hatari sana dunia ya leo kuchukua mzigo wa mtu usiyemjua au hukuupekua vizuri ukawa una ushahidi nao unaweza kukuingiza matatizoni. Kwahiyo, tujitahidini sana kwasababu baadaye huyo anayekupa anakataa kama alikupa.

Nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuendeleze mapambano ya rushwa, kwasababu rushwa ni chanzo kimoja kinachopunguza kasi ya mapambano haya ya kupambana na dawa za kulevya. Lakini tayari kuna miongozo ya marais wetu kwamba, mtendaji yeyote wa taasisi ya serikali ama askari yeyote yule atakayeshiriki ikiwa kwa njia ya rushwa au kwa namna yoyote nyengine kuendeleza vitendo hivi vya biashara haramu ya dawa za kulevya, basi mtu huyo jambo la kwanza ajue kuanzia siku hiyo nafasi yake katika kazi ameikosa na hatua nyengine za kisheria zitachukuliwa. Kwahiyo, mapambano haya yanaendelea na kamati mbalimbali zimeundwa kuchunguza hao wahusika wa mapambano hayo waliyo mstari wa mmbele, ili watu wote sasa tuzungumze lugha moja na tushirikiane katika mapambano haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mawazo ya kuweka vifaa vya kisasa katika *airport* na bandari zetu kama nilivyosema awali, huo ni mpango wa serikali imeamua kabisa kuweka vyombo vyote na vifaa vyote vya kisasa vitakavyopambana na kila aina ya uhalifu yakiwemo madawa ya kulevya. Sasa hivi hata maeneo ya mjini wanaona kazi kubwa inaendelea ya kuweka *CCTV*, yote hayo na kuna mitambo mingine ni namna ya kuwatambua wahalifu ili kuweka mji wetu salama. Lakini wakati huo huo kwenye vianzio vya uingiaji kama *airport* na bandari mambo haya yataimarishwa zaidi ili kuwatambua wahalifu hususan wa madawa ya kulevya.

Vilevile, ushauri wa kuwa na Kitengo cha Madawa ya Kulevya pale kwenye *airport* mpya, huu tumeupokea na tayari umeshaanza kufanyiwa kazi kwasababu nia na dhamira ni kuwa na vifaa vya kutosha pale *airport* kila kifaa kinachotakiwa kiwepo, ili kutambua wale wanaoingiza madawa ya kulevya na wahalifu wengine, ili nchi yetu ibaki katika hali ya usalama.

Nakubaliana na ushauri hususan aliyoutoa Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwamba kasi iimarishwe kwa upande wa Pemba mapambano haya, tutafanya hivyo ili hawa wahalifu wasiondoke Unguja na kuhamia Pemba. Vilevile, wenzetu waliokwishaanza kuathirika huko Mwenyezi Mungu awasaidie waepukane na jambo hili, lakini mapambano yataendelea kwa kila hali na hususan katika madiko na sehemu nyengine ni lazima kuimarisha mapambano.

Mhe. Mwenyekiti, sote itatubidi tushirikiane kwa undani zaidi katika kuwasaidia wanafunzi wetu. Watoto wetu hawa ni wadogo wanaweza kughilibiwa kwa namna moja au nyengine. Kwakweli, ni jambo la kusikitisha sana kwamba watu hawa wameharibikiwa kiasi ambacho sasa wanataka kuwatumia watoto wetu wadogo washiriki katika mambo haya ambayo hayasaidii hata kidogo katika maendeleo ya taifa letu, lakini pia kwa kuamini kwamba vijana wetu hawa ndio taifa la leo na kesho na ndio viongozi wetu wa kesho inabidi tufanye kila njia kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha tunawatunza wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Kuhusu kuwa na mkemia mmoja Pemba ushauri tumeupokea, ili wakemia wawe wengi shughuli zifanyike vizuri. Tutapambana na askari yoyote atakayeshiriki katika madawa ya kulevya nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kazi hiyo imeanza na yeyote atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Kuhusu kuharakisha kwa kesi, ndio mtazamo wa serikali kesi zifanywe haraka, ili majibu yapatikane haraka na wale waliofanya makosa sheria ichukue mkondo wake. Tayari utaratibu umewekwa mzuri wa kuharakisha hizi kesi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la rushwa kweli lipo tatizo hili, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe tutashirikiana katika mapambano haya ili tuliondoe kabisa. Takriban kwenye kumarisha ulinzi itakuwa ni kipaumbele katika maeneo yote.

Kuhusu viwango ni kweli mule katika taarifa kuna neno la viwango vikubwa. Hilo limejitokeza kwa makosa nia yetu ya kuanzisha kanuni ya viwango vidogo vidogo maana yake hata kikiwa kidogo cha namna gani kosa hilo litakuwa sawa na vile viwango vikubwa, hakutokuwa na tofauti kwa mujibu wa kanuni zetu na marekebisho ya sheria iliyopita. Kwa hivyo, viwango vidogo vya aina yoyote vitachukuliwa ni sawa sawa na hicho kikubwa na haki itendeke na sheria ichukue mkondo wake kila anayehusika kwenye mambo hayo sheria ichukue mkondo ili wahusika watiwe hatiani na waweze kuhukumiwa. *(Makofi)*

Kuhusu kamati kupitia katika mitaa. Mhe. Mwenyekiti, ushauri tumeupokea tutakaa na Mhe. Makamu wa Pili tujipange wajumbe, ili kupitia katika mitaa yetu kuona namna gani tunafanya kazi. Kuondoa muhali tunaupokea ushauri huo, ili tuondoe muhali na mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo haya nataka tena niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi hii nzuri tuendelee kushirikiana wote, twende tukapambane ni kazi kubwa na nzito. Lakini naamini Zanzibar bila ya madawa ya kulevya inawezekana na tutashinda. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi wa hoja hizo. Sasa, Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwaulize kama hoja yetu hiyo iliyotolewa mbele yetu tumeipokea au laa. Kwahivyo, wale wanaokubali kuipokea hoja hii wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo Mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa mara nyengine kwa kunipa nafasi hii. Aidha tuendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na kutujaalia kuendelea na shughuli zetu kwa leo hii na naamini Mwenyezi

Mungu atatuwezesha kuzimaliza shughuli hizi kwa leo kwa salama ili tuamkie keshi kwa ajili ya shughuli nyengine kama zilivyopangwa na Baraza letu na Mwenyezi Mungu atujaalie uhai na afya.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru sana Mhe. Asha Abdalla Musa, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Kiwengwa juu ya suala lake alilolileta katika hoja hii ya Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Kisheria unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Asha Abdalla kwa namna alivyowasilisha hoja na niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia katika hoja hii na mwisho wake tukafikia maazimio ya Baraza lako tukufu na naomba leo nieleze utekelezaji wa maazimio haya kwa upande wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na azimio nambari moja.

Azimio Nam. 1. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018, serikali iliweke suala la kupambana na kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali, ili kuweka mazingira mazuri ya kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji, ikiwemo kuviwezesha Vituo vya Mkono kwa Mkono na kufanya kazi zake kitaalamu na kwa uhakika pamoja na kuviwezesha vituo hivyo kufanya kazi kwa masaa 24, ili kushughulikia kesi wakati wote zinapojitokeza.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ikiwa ndiyo mratibu mkuu wa kusimamia mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto hapa nchini, mbali ya kutenga bajeti kwa ajili ya uratibu pia imeandaa Mpango wa Miaka Mitano wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Utekelezaji wa Mpango huu utashirikisha wadau wote katika ngazi zote kuanzia shehia hadi taifa.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika bajeti yake ya mwaka 2017/2018, tayari imetenga jumla ya shilingi milioni mia moja sabini na tano na laki moja (175,100,000/-) kwa ajili ya kusimamia na kuratibu mapambano ya vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika vikao vyake vya uratibu imelijadili kwa kina suala la kuviwezesha Vituo vya Mkono kwa Mkono na kwa kupitia Wizara ya Afya, imekubaliana kuviimarisha vituo hivyo, ili viweze kutoa huduma kwa masaa 24. Wizara ya Afya pia imepeleka maombi Tume ya Utumishi Serikalini ya kuajiri Washauri Nasaha kwa ajili Vituo sita(6) vya Mkono kwa Mkono mbali na kituo kilichopo Hospitali ya Mnazimmoja ambacho kimeongezewa wafanyakazi sita (6), ili kutoa huduma hizo kwa muda wote.

Azimio Nam. 2. Serikali katika bajeti ya mwaka 2017/2018 iweke utaratibu maalum wa kupunguza vifungu vya fedha kwa kila bajeti ya wizara, ili kuweza kupata fedha za ununuzi wa mashine ya *DNA***.**

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, serikali kupitia Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kupitia fungu la Mkemia Mkuu wa Serikali, ili kununua mashine ya *DNA* tayari imetenga jumla ya shilingi bilioni moja (1,000,000,000) kwa kazi hiyo.

Azimio Nam. 3. Mhe. Mwenyekiti, ili kuipatia jamii uelewa wa matatizo haya, serikali iandae siku maalum ya kupinga udhalilishaji wa watoto kitaifa, ambayo itaadhimishwa kwa kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusiana na kupiga vita udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na taasisi nyengine za serikali inachukua jitihada kubwa za kuielimisha jamii juu ya namna ya kupambana na kuvitokomeza vitendo hivi kupitia vyombo vya habari, mikutano, maskuli, Madrasa, Mihadhara ya kidini na Makongamano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile ziko siku maalum ambazo huadhimishwa kimataifa na kikanda kama vile Siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Mwanamke Duniani na Siku 16 za Wanaharakati za Kupinga Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia, kuweka siku maalum nyengine itakuwa sio vyema. Serikali itaendelea kufanya kila jitihada ya kuvitokomeza vitendo hivi kwa kuielimisha jamii juu ya suala hili kila siku na kupitia siku hizi kwa kutumia njia mbalimbali.

Azimio Nam. 4. Serikali ndani ya mwaka mmoja, ilete katika Baraza la Wawakilishi Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Namba 7, ya mwaka 2004, ili kuongeza Mamlaka ya Mahakama za Mkoa kutoa adhabu zaidi ya miaka saba 7 na kufanya marekebisho ya kifungu namba 150 (1), ili kuingiza makosa ya kujaamiiana kuwa miongoni mwa makosa yasiyopatiwa dhamana.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, serikali inakubaliana na hoja ya Mamlaka ya Mahkama ya Mkoa kuongezewa nguvu ya utoaji wa adhabu kubwa zaidi kwa kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa wa Jinai 7/2004 pamoja na Sheria ya Adhabu Namba 6/2004. Suala la Uwezo wa Mahakama za Mwanzo kuhusu adhabu ya kifungo kama ilivyoelezwa na Kifungu cha 9 cha Sheria Namba 7 ya mwaka 2004 umeongezwa kuwa zaidi ya miaka 7. Aidha, makosa ya kujamiiana katika Kifungu cha 150(1) yamependekezwa kuwa miongoni mwa Makosa yasiyokuwa na dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Baraza la Wawakilishi jukumu lake moja kuu ni kutunga sheria ya Zanzibar. Hivyo, serikali itaendelea kupokea ushauri wa Baraza hili katika kupendekeza mabadiliko zaidi ya vifungu kwa mujibu wa hali halisi ilivyo katika suala zima la udhalilishaji ili kulinda haki kwa waathirika na vitendo hivyo vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la makosa ya udhalilishaji kutokupatiwa dhamana, kwa hivi sasa kikao cha Wajumbe wa Kikundi Kazi kilichofanyika tarehe 10 Februari, 2017 chini ya Uenyekiti wa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na kuhudhuriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadhi ya Mawaziri, Mkurugenzi wa Mashitaka, Kamishana wa Polisi Zanzibar na Mrajis wa Mahakama kimetoa tamko la kuunga mkono “Operesheni

Maliza Udhalilishaji" na kufuata mkondo wa sheria kwa watuhumiwa wa makosa haya wasipatiwe dhamana.

Azimio Nam. 5. Pamoja na marekebisho hayo, serikali iweke utaratibu wa kisheria wa kuwachukulia hatua kali wahusika wa kesi, ambao watachukua hatua za kusuluhishana katika ngazi ya kijamii na kufuta kesi za udhalilishaji na wale watakaokataa bila ya sababu za msingi, kutoa ushahidi na watakaovuruga ushahidi wa kesi hizo.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho ya Sheria ya Adhabu Namba 6 ya 2004, inapendekezwa kwamba, kosa la kusuluhisha kesi za udhalilishaji katika ngazi ya kijamii na kuzifuta litiliwe mkazo na sheria iweke kifungu cha "yeyote atakayeshiriki au atakaesimamia usuluhishi wa kesi za udhalilishaji awe ni mshiriki wa kosa na ashitakiwe kwa mujibu wa kosa, na ikithibitika apate adhabu ya kosa la udhalilishaji kama marekebisho yatakavyofaywa na sheria, ili sheria ichukue mkondo wake".

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kukataa kutoa ushahidi, shahidi anapogoma au kukataa kwenda Mahakamani kutoa ushahidi bila ya sababu za msingi, hili ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai katika Sheria za Zanzibar na hushtakiwa chini ya Kifungu cha 116 cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

Vile vile kuvuruga ushahidi ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai ya mwaka 2004 kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 99 kuwa kuvuruga ushahidi ni kosa, lakini pia sheria imeeleza kuwa mtenda kosa hilo atawajibika kwa '*Misdemeanor'*. Kwa jicho la sheria kosa linapopewa hadhi ya '*Misdemeanor'* maana yake ni kuwa kosa hilo sio '*serious'* na mshitakiwa akikutwa na hatia adhabu yake ni kifungo cha miaka miwili na sio zaidi. Hivyo, marekebisho ya sheria yazingatie kwamba katika kesi za udhalilishaji makosa ya kuvuruga ushahidi yaondolewe kwenye '*Misdemeanor'* na adhabu yake iwe ni kali ili wahusika wawe makini katika kudhibiti vielelezo pindi vinapokuwa katika milki yao.

Azimio Nam. 6. Mhe. Mwenyekiti, serikali iunde tume ambayo pamoja na kufuatilia mambo ya jumla yanayosababisha kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji, lakini pia ifanye utafiti wa kina ili kujua sababu zinazosababisha idadi ya kesi zinazoripotiwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) kuwa ni kidogo ukilinganisha na idadi ya kesi zinazoripotiwa na wananchi katika vituo mbalimbali. Aidha, tume hiyo ifanye uchunguzi, ili kubaini wale ambao wamekuwa wakikiuka maadili ya kazi zao na kusababisha kesi hizi kuongezeka siku hadi siku na kupendekeza adhabu kali za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi yao, na ripoti ya tume iwasilishwe ndani ya Baraza kwa ajili ya kujadiliwa. *(Makofi)*

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, serikali tayari imeunda Kamati ya Mawaziri inayojumuisha Wizara inayosimamia masuala ya Wanawake na Watoto, Wizara inayosimamia masuala ya Sheria, Wizara inayosimamia masuala ya Elimu, Wizara inayosimamia masuala ya Afya, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Mahkama ambayo inasimamia mwenendo mzima wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kesi kidogo zinazopelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ukilinganisha na matukio yanayoripotiwa na wananchi ni kwamba matukio baada ya

kufanyiwa upelelezi mengine huonekana hayana ushahidi wa kutosha wa kufunguliwa kesi. Yale ambayo yana ushahidi wa kutosha ndio yanapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, ili kujiridhisha na ushahidi na kufungua kesi Mahakamani ndio maana kuna tofauti baina ya matukio yanayoripotiwa na wananchi na yanayopelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hatahivyo, hatua zitachukuliwa kuhakikisha kesi inayostahiki inapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na zile zinazothibiti kupelekwa Mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria.

Azimio Nam. 7. Mhe. Mwenyekiti, bila ya kuathiri uhuru wa mahakama, uandaliwe utaratibu wa kuharakisha muda wa kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi za udhalilishaji, ili haki itendeke kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeandaa Operesheni Maalum ya Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia ikiwemo kuweka msukumo wa kuharakisha utoaji wa hukumu wa kesi hizo. Kuanzia tarehe 1 Machi, 2017 jumla ya kesi 54 zilifunguliwa na kufanyiwa kazi na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kati ya hizo, hadi kufikia tarehe 14 Juni, 2017 kesi 26 zimemalizika. Kesi 28 zilizobakia zinaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali za kimahakama.

Azimio Nam. 8. Kamati husika ya Baraza la Wawakilishi ijumuishe katika ripoti yake ya kila mwaka, namna ilivyosaidia katika kupambana na tatizo hili la udhalilishaji wa watoto na wanawake nchini.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinawasilisha ripoti katika Baraza mara moja kwa mwaka katika mwezi wa Februari na hoja ilipojadiliwa Kamati za Baraza la Wawakilishi zilikuwa tayari zimeshawasilisha ripoti zao. Hivyo, kwa mwaka ujao wa fedha serikali itatoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya kisekta kuingiza taarifa ya masuala ya udhalilishaji kwa wanawake na watoto katika ripoti ya kamati hiyo. Aidha utaratibu huo utakuwa unafanyika kila mwaka, ili iwezekuwasilishwa katika Baraza hili lako tukufu.

Azimio Nam. 9. Serikali kupitia wizara husika, ilete mbele ya Baraza, ripoti ya namna inavyolishughulikia tatizo hili katika awamu, ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wapate fursa ya kusaidia fikra na mikakati ya kupambana na tatizo hili.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto huwa inawasilisha Ripoti ya Mtoto kila mwaka ifikapo mwezi wa Juni. Hivyo, ili kufikia lengo la azimio hili, wizara itajumuisha katika ripoti hiyo, ripoti ya namna inavyolishughulikia tatizo la ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto na kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kila mwaka. Aidha, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Ustawi wa Jamii itakuwa inapata taarifa hizo katika kila taarifa ya robo mwaka za wizara inapowasilisha kwenye kamati ya kudumu husika.

Azimio Nam. 10. Serikali iandae utaratibu maalum wa kuzifuatilia na kuzisimamia nyumba binafsi za kulelela watoto, ili kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa na kuwa katika mazingira salama.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imekamilisha uandaaji wa kanuni za Uanzishwaji Makaazi na Matunzo. Kanuni hizo zinatoa utaratibu wa utoaji wa leseni kwa vituo vyenye viwango na kuvifunga vituo visivyo na viwango. Aidha, wizara kupitia Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii inafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa nyumba binafsi za kulelea watoto, ili kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa na wako katika mazingira salama.

Azimio Nam 11. Serikali iwe na *program* maalum kwa ajili ya kuwapatia elimu Mahakimu na wahusika wengine, elimu ambayo itawashajihisha na kuwapa muamko wa kuweza kuzipa kipaumbele kesi hizi wakati zinapofika mbele ya Mahakama na vyombo vyengine.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inao utaratibu wa kuwapa mafunzo Mahakimu na Watendaji wa Sheria ikiwemo Polisi na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya namna ya kuzishughulikia kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Kuhusu suala la kuweka programu maalum serikali italifanyia kazi kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika, ili suala hili liweze kutekelezwa vizuri na kumbana na udhalilishaji.

Azimio Nam. 12. Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wakiwa kama Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi za Mikoa na Wilaya, waongeze kasi ya namna ya kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji katika maeneo yao.

Majibu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya inashiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, ikiwemo kuunda Kamati za mapambano na ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji katika ngazi za mikoa, Wilaya na Shehia. Kamati hizo pia zinafuatilia kesi za udhalilishaji na kuhakikisha kuwa wahusika wanachukuliwa hatua ipasavyo. Aidha, kunatolewa elimu kwa wananchi kupitia Kamati za Uhifadhi za Wilaya na Shehia, kufanya Makongamano ya Vijana na kufanya operesheni maalum katika maeneo hatarishi yakiwemo ya starehe.

Azimio Nam. 13. Uwepo utaratibu maalum kupitia kwa masheha kuweza kupeana taarifa juu ya wahusika wa matukio ya udhalilishaji, ambao wanahama kutoka Shehia moja kwenda nyengine ili kuwezesha kuchukua tahadhari juu ya watu hao, kabla hawajafanya vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto na wanawake.

Majibu ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kupeana taarifa za kuwatambua wahusika wa matukio ya udhalilishaji wanaohama mitaa upo katika ngazi ya Shehia, Wilaya na hatimae Mkoa. Taarifa hizi zinajadiliwa kwenye vikao katika ngazi hizo kwa lengo la kuwatambua wahalifu wanaotoka sehemu moja kuingia nyengine, ili kuhakikisha kuwa wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Aidha, Masheha wana utaratibu wa kupeana taarifa pindi inapotokea kesi ya udhalilishaji ili kuzuia wahalifu kutorokea katika shehia zao kutoka maeneo waliyofanya makosa hayo. Kila shehia kuna mratibu wa Wanawake na Watoto na Mabaraza ya Watoto, ambayo kwa pamoja hushirikiana kutoa taarifa katika taasisi zinazohusika. Naamini utaratibu huu utasaidia sana kuwashughulikia wahalifu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, serikali itaendelea kuchukua juhudi kubwa za kuweka mifumo itakayosaidia wadau wote kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, ili kukomesha vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto pamoja na makundi mengine ambayo yamo katika hatari ya kukumbwa na vitendo hivyo thakili.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeamua kupambana na wahalifu wa aina hii ili watoto wetu, vijana wetu na wananchi kwa jumla wabaki salama.

Baada ya maelezo haya Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya serikali imshatolewa. Lakini kabla sijaruhusu mchangio naomba nitoe tangazo lifuatalo.

Katibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wa Baraza anawatangazio wafuatao wakutane chumba namba 3 baada ya kuakhirishwa kikao hichi. Waheshimiwa wenyewe ni Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Ussi Yahya Haji. Hawa wanaombwa wakutane baada ya kuakhirishwa kikao hichi chumba namba 3. Ahsanteni.

Sasa anayefuata ni Mhe. Mjumbe aliyeanzisha hoja hii ni Mhe. Asha Abdalla Mussa kutoa maoni yake. Mhe. Asha Abdalla Mussa karibu sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia majibu ya serikali yanayohusiana na hoja ambayo niliyoiwasilisha katika kikao kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona kwamba upo umuhimu wa kuleta majibu au kufanyia kazi hoja za Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuleta maendeleo katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kusema kwamba mimi ndiye niliyeleta hoja, lakini pia nakubaliana na majibu ambayo yameletwa na serikali, pia naamini kwamba majibu haya yaliyoletwa kwetu wakiyafanyiwa kazi ipasavyo, basi naamini suala la uzalilishaji Wanawake na Watoto litaondoka hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mambo ya kuchangia mafupi sana. Kwanza kabisa niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kutenga shilingi milioni mia moja na sabini na tano na laki moja kwa ajili ya kusimamia na kuratibu mapambano ya vitendo vya udhalilishaji vya wanawake na watoto. *(Makofi)*

Naamini kwamba fedha hizi ambazo ambazo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walizipigania kutoka shilingi milioni hamsini na tano na hatimaye kufikia shilingi milioni mia moja na sabini na tano na laki moja, naamini kwamba zikifanyiwa kazi ipasavyo basi lile lengo ambalo tumelikusidia litafikia.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya serikali pia tumeona kwamba kupitia Wizara ya Afya imekubaliana kuviimarisha vituo, ili ziweze kutoa huduma kwa masaa 24 yaani, vituo hivi ni Vituo vya Mkono kwa Mkono.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikli kupitia Wizara ya Afya, Mhe. Waziri wa Afya yupo na usumbufu mkubwa unakuwa unatokezea hadi sasa unazidi kuendelea katika Vituo vyetu vya Mkono kwa Mkono. Wahanga wa matatizo haya wanapofika katika Vituo hivi vya Mkono kwa Mkono wanapata tabu sana wanapofika huduma ile hawaipati ipasavyo, na wakati mtoto anapobakwa anatakiwa apelekwe kituo cha Mkono kwa Mkono na hatimaye baadaye afanyiwe uchunguzi na mwisho ripoti iandikwe kwa ukamilifu.

Lakini jambo la kusikitisha kwamba wanapofika pale wahanga hawa wale wahusika hawawakuti na huduma ile hawaipati, na hatimaye siku ya pili yake watakapofika pale ule ushahidi utakuwa umepotea. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali kupitia Wizara ya Afya, basi wahakikishe suala hili jibu ambalo wametuletea hapa lifanyike ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala jengine la Sheria ya Adhabu. Kwakweli Sheria Nam. 7 ya mwaka 2004 ambayo ilitoa uwezo wa Mahakama za mwanzo kuhusiana na adhabu za kifungo cha mwisho yaani, kisichozidi miaka 7. Kutokana na hali hiyo, serikali imeleta majibu kwamba wanaanda sheria hiyo ili iletwe hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba kwamba ifanyiwe haraka sana kwa kuwa vitendo hivi vinaongeza siku hadi siku iletwe hapa Barazani tuweze kupitisha na iweze kutumika kama kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwamba niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutenga pesa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununua mashine ya *DNA*. Mhe. Mwenyekiti, mashine ya *DNA* ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wetu wa Zanzibar, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wale watu ambao wamefanya vitendo hivi.

Lakini na pia wale watu ambao wahusika wa kuziendesha kesi hizi ili kuhakikisha kwamba ushahidi unapatikana. Hivyo, basi niseme kwamba fedha zimetengwa tunaomba sana hii mashine inunuliwe, lakini mashine itakaponunuliwa basi wale wataalamu ambao watakaowekwa katika kitengo hichi tuwatafute wataalamu ambao wako makini, vilevile wanaoweza kufanya kazi wakati wowote bila ya usumbfu wowote na hatimaye baadaye waweze kutoa ripoti, ambayo itakayoweza kuisaidia serikali yetu kuhakikisha kwamba kesi hizi zinakwenda kiutaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la mwisho kwamba kuna masuala mazima ya kuvuruga ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba wananchi wetu wengi wanalalamika kwamba yanapotekea matukio haya kuna sehemu nyingi sana ambazo ushahidi unapotea, ikiwemo Jeshi la Polisi pamoja na hivyo vituo vya afya kwasababu nimezungumzia mwanzo, lakini na polisi nao wanaturudisha sana nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anapopatwa na tukio hili anapokwenda polisi kupeleka kesi yake, basi yule mshatakiwa anapokwenda pale kwakweli wale polisi wakati mwengine hawatutendei haki. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano hivi juzi tu Pemba lilitokea tukio la mwanafunzi kupigwa katika Skuli ya Binafsi na hatimaye baadaye kupoteza maisha mtoto yule. Lakini cha kusikitisha Mhe.

Mwenyekiti, baada ya tukio hili kufanyika basi inasemekana kwamba polisi au mkuu wa kituo kile alipoteza ushahidi hataki kusema ukweli kwa tukio lile ambalo limetokezea katika eneo lile.

Kwakweli tukiwa hatuko makini katika kazi zetu kwa ngazi husika tatizo hili litabakia kuwa lipo pale pale. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kamati iliyoundwa ifatilie kwa kina, ili iweze kutuletea ripoti katika Baraza hili la Wawakilishi na tuone tunaweza kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba naamini kwamba sote kwa pamoja kwa kila mmoja na wajibu wake akitekeleza ule wajibu wake, natumai kwamba suala hili tutalitokomeza la vitendo vya udhalilishaji vya wanawake na watoto. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Asha Abdalla Mussa. Sasa namwita Mhe. Ali Suleiman Ali na baadaye Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia maelezo ya utekelezaji kwa maazimio ya hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na uimarishaji wa mfumo mzima wa kisheria unaohusiana na uendeshaji wa kesi za udhalilishaji kwa wanawake na watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, bado naipongeza serikali yetu kwa kuamini kwamba haya maazimio yanayotolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huwa ni kichocheo ua ni kielelezo tosha kwamba jamii yetu imo katika mazingira ya hatari na yanatakiwa kufanyiwa kazi.

Lakini niipongeze wizara au serikali kwa jumla kwa majibu mazuri waliyotoa na majibu ambayo yanakidhi haja, na naamini tu kwamba ni wajibu wetu kutoa changamoto mbili tatu juu ya utekelezaji wake kuendeleza haya yanayotarajiwa ili kuleta imani kwa serikali yetu na wananchi wake ambao inaitegemea serikali hii.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye azimio namba 4 katika majibu ya serikali, naomba ninukuu kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti, "serikali inakubaliana na hoja ya Mamlaka ya Mahakama ya Mkoa kuongezewa nguvu ya utoaji wa adhabu kubwa zaidi kwa kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo ya Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004, pamoja na Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya suala la uwezo wa Mahakama ya Mwanzo, kuhusiana na adhabu ya kifungo kama ilivyoelezwa na kifungu Nam. 9 cha Sheria Nam. 7 ya mwaka 2004, umeongezwa kuwa zaidi ya miaka 7 aidha, Makosa ya Kujamiana katika kifungu cha 150(1) imependelezwa kuwa miongoni mwa makosa yasiyokuwa na dhamana".

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa imani yangu hili suala nalikaribisha kwa hamu, tena nalikaribisha kwa haraka zaidi. Pamoja na kuambiwa ndani ya mwaka mmoja sheria hii italetwa, mimi naona mwaka mmoja ni mwingi sana watoto wetu na kinamama wanaangamia.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa makusudi natoa ushauri, sheria hii ifanyiwe haraka, hii kuanzia zaidi ya miaka 7 tutakuja kujadili hapa, lakini haitoanzia miaka 7, itakuwa kwenye miaka 40 au

50 ili liwe ni komesho lisitokee tena katika nchi yetu. Lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri kwamba palikuja na hoja hapa. Hili naomba kusema kwa nia safi kabisa, juu ya suala ambalo, na mimi dereva naendesha gari katika mji wetu ulikuwa katika mazingira magumu katika wanyama wanaohangaika kwenye barabara zetu mjini, wanyama wasiofugwa, mswada uletwe haraka sana ili kuondoa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa vizazi vyetu watoto wetu na kina mama wanaathirika siku hadi siku, naiomba serikali bado pamoja na taarifa hii iliyoletwa na majibu mazuri, naiomba iharakishe kwa muda mfupi, iwe ni kama mswada wa dharura ili kuhakikisha kwamba suala hili linaondoka katika nchi yetu na libakie historia lisiendelee katika maisha ya watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, watoto wetu wanaishi katika mazingira magumu. Watoto wakitoka hawajui kama watarudi salama, mtoto anakokwenda wakati mwengine haamini hajui kama hatobakwa. Kwa hivyo, niseme kwamba umefika wakati Mhe. Mwenyekiti, pasiwe na muda mrefu Baraza la Mapinduzi likae, liulete mswada huu kwa wakati unaofaa, hasa tukizingatia Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, katika mikutano yake na katika maelezo yake anasikitishwa na tunasikitishwa sote na vitendo ambavyo watoto wetu na kinamama wanaathirika siku hadi siku. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili pamoja na kulipenda zaidi kuwa litaletwa lakini muda usiwe mrefu.

Jengine kidogo tu Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yatakuwa yanajirudia, lakini na mimi pia niseme tu, kwa sababu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inanigusa na mimi kama mwenyekiti wa wizara. Kwa hivyo, naipongeza sana serikali yetu kwa kuleta mfumo mzima wa kuhakikisha chombo cha *DNA* kitawasili karibu katika nchi yetu na kitatumika ili kuondoa matatizo ya kupatikana ukweli wa jambo lililotendeka kwa wakati.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia Wizara ya Afya, Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia mengi, serikali ina mipango mizuri na mipango yake iwe neema kwa wananchi wake, lakini neema ile inapofika huwa ni kadhia au shida kwa wananchi wake haiwahudumii ipasavyo, huduma inakuwa finyu na inakuwa na matatizo. Hofu yangu hapa pasijekuwa na rushwa, kwa sababu serikali imesema tu kwamba chombo hiki kitaletwa na kiwe kinafanya kazi katika njia za busara na za utaratibu ili ukweli upatikane. Hofu yangu pasijekuwa na rushwa iangaliwe na wawe waaminifu wanaofanya kazi hiyo, ili ukweli ujulikane juu ya kadhia inayotokea katika nchi yetu.

Jengine kwa ufupi tu Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hii taarifa nzuri na imekuja kwa wakati wake. Mimi nimeyazungumzia mambo mawili makubwa la kwanza tunamuomba Mhe. Waziri mswada wa sheria uletwe haraka na uwe ni wa dharura, kwa sababu vijana wetu au watoto wetu wa kike na wa kiume kwa bahati mbaya wanadhalilishwa na wanafanyiwa vitendo viovu, kwa hivyo hili liondoke.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji vina njia nyingi. Kuna kudhalilishwa kwa vitendo vichafu, kuna kupigwa bakora, kuna kuchomwa moto na mambo mengineyo. Lakini kwa bahati mbaya tumepata taarifa juu ya mtoto aliyepigwa Pemba katika skuli ya Laurent kama sikosei, ndio hiyo hiyo. Tunaomba tupate taarifa kwa kuwa jambo hili haliko mahakamani, labda tuambiwe tu kwamba tumefikia hatua gani juu ya kadhia iliyotokea

mtoto yule kafa, lakini mpaka leo tunaona tuko kimya. Kama kuna taarifa tupewe ili wananchi wajuwe juu ya maendeleo ya utaratibu mzima wa kesi au mambo mengineyo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa naunga mkono taarifa hii, naipongeza serikali, naipongeza kamati iliyoleta kwa kupitia chini ya Mhe. Asha Abdalla Mussa, kuwa ni taarifa ya kuhakikisha kwamba watoto wetu wawe salama wanapotembea au wanapoishi, juu ya kutokewa na athari ambazo zitawaharibia maisha yao. Naunga mkono kwa asilimia mia moja sina tatizo Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Ali Suleiman Shihata. Sasa namwita Mhe. Suleiman Makame Ali, akifuatiwa na Mhe. Simai Mohamed Said Mpakabasi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu kuhusu suala zima la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Said Soud Said Waziri asiyekuwa na wizara maalum, kwa kuichambua vyema ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio ilani inayotekelezeka na hakuna asiyejua hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ilani ya Chama cha Mapinduzi imesheheni kila kitu, udhalilishaji, madawa ya kulevya na mengineyo. Suala la udhalilishaji naona tena hapa Zanzibar imekuwa kama wimbo wa taifa, kila kukicha udhalilishaji udhalilishaji, ukenda mitaani huko udhalilishaji, ukenda majimboni udhalilishaji, ukenda mikoani yaani nyimbo ni hiyo tu.

Mhe. Mwenyekiti, sote humu wajumbe wako nadhani ni wazazi na ni walezi wa watoto. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nadhubutu kusema kwamba roho huwa hatunazo tunafikiria huko majumbani watoto wetu wako katika hali gani, yaani ukenda ukamkuta mtoto yuko salama basi ushukuru kutokana na tatizo hili la udhalilishaji liliopo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuwaomba tu kuanzia ngazi ya masheha, kwenda Polisi mpaka Mahakama, basi wahakikishe kwamba masuala haya ya udhalilishaji hawayafumbii macho na wanatoa ushirikiano na wale wazee ambao watoto wao wamefanyiwa vitendo hivyo vilivyokuwa havifai. Sio vizuri kuwapiga danadana wakati ule wa kesi kwa sababu kile mtu ni mzazi hakuna hata mmoja asiyejua uchungu wa mtoto humu ndani kusema kweli, na hata huko nje hakuna mmoja asiyejua uchungu wa mwana. Ikiwa kama yeye mwanawe hapendi kufanyiwa vile, basi na yule mwana wa mwenzake inapokwenda ile kesi sio tena ampige danadana amwambie kesho na keshokutwa, mpaka inafika tena wale wazazi wengine wanachoka kufuatilia zile kesi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo na mimi ninyanyuwe tena ilani ya Chama cha Mapinduzi hii katika ukurasa wa 223, ibara ya 169 inasema; kila mtoto ana haki ya kuishi, kukua na kulelewa kikamilifu ili taifa kwa siku za baadae lipate raia wema na waadilifu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, uadilifu huo utakuja wapi ikiwa masuala ya udhalilishaji sasa hivi yameshika kasi kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman hapa alisema kuhusu suala lililotokea kule Pemba katika skuli ya Laurenti. Nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri hapa wa Elimu na Mafunzo ya Amali, hii

sheria ya kumchukua mtoto mwanafunzi wa skuli akapigwa kama mwizi inatoka wapi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iko hii ilikuaje hata mtoto yule apigwa bakora apitishwe kila darasa alazwe chini apigwe mpaka asababishiwe maafa kusema ukweli. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli ni suala la kusikitisha na kwa kila aliyekuwa mzazi ameumia kwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Ali Suleiman Shihata alisema anataka tupate majibu, basi na mimi naungana na yeye naomba tupate jibu kwenye suala hili. Kwa sababu leo ni yule, kesho ni huyu na yule pale. Mimi sitaki niseme mengi lakini nataka nitie msisitizo zaidi kwamba kwenye suala hili la udhalilishaji lipewe kipaumbele ili likomeshwe hapa Zanzibar au Tanzania kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wanajitoa mshipa wa fahamu kabisa, wanafanya vitendo hivi makusudi na kuona kwamba labda hakuna hatua zitakazochukuliwa. Lakini mimi najua kwamba serikali yetu kwa kupitia Rais wetu makini Dk. Shein basi nina imani vitendo hivi vitakomeshwa. Lakini sasa kwa sababu ili Rais zionekane jitihada zake ni wale watu ambao wanamsaidia zile kazi watendaji wa taasisi mbali mbali wafanye kazi hizi kwa uadilifu, na aliyekuwa hawezi kutekeleza ilani hii ya Chama cha Mapinduzi Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba atupishe na aondoke kabisa, kwa sababu itakuwa tayari atapakwa matope Rais wetu na serikali kwa jumla.

Kwa hivyo, mimi naomba kwa yeyote yule ambaye kuwa ana nafasi ya kulikomesha suala hili la udhalilishaji, kwa nafasi yoyote aliyonayo, na kama hawezi kutekeleza ilani ya CCM basi atupishe. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa namwite Mhe. Simai Mohamed Said Mpakabasi na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hii hoja muhimu ambayo leo tumepata majibu yake kutoka kwa serikali, na maelezo ya utekelezaji wa maazimio ya hoja juu ya mfumo mzima wa kisheria unaohusiana na uendeshaji wa kesi za udhalilishaji za wanawake pamoja na watoto hapa Zanzibar. Lakini pia nimpongeze ndugu yangu Mhe. Asha Abdalla kwa uwasilishaji wake na maelezo aliyoyatoa siku ya uwasilishaji pamoja na leo pia kutoa majibu yake na kuunga mkono yote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi yangu yatakuwa ni machache, lakini naamini haya yatakuwa ni mambo ya msingi. Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo ambayo yametolewa na Mhe. Waziri, kuna maeneo ambayo tuliwahi kuzungumza hapa Barazani, lakini naomba niyatilie mkazo.

Suala la kwanza nikuwaangalia watoto wetu hasa vijana juu ya matumizi ya simu hizi zinazoitwa *Smartphone* hasa katika maeneo wanapokwenda maskulini na maeneo tofauti. Hizi simu kwa kweli zina mambo mengi na zina vitu vingi ndani, kwa hivyo ningeshauri sana serikali kwa kupitia viongozi hasa kutoka katika wizara husika zote wasimamie utekelezaji katika masuala haya ya simu ya *Smartphones* ili kuhakikisha kwamba vijana wetu hasa wanalindwa na wanatumia hizi *Gadget* kwa wale ambao wanastahiki na umri unaofaa.

La pili, nilizungumza juu ya suala la malezi ya watoto, ni sahihi kwamba wapo binadamu ambao wameumbwa na Mwenyezi Mungu, lakini ukiangalia matendo wanayoyafanya hawa binadamu hasa kwa watoto wetu, ni mambo ya kinyama, ya kishenzi na hayazungumziki. Sasa nashauri sana suala la malezi lipatiwe nafasi maalum hasa kwa kina na kina mama. Mhe. Mwenyekiti, hii ni ukweli kabisa leo hapa ukiangalia kwenye Baraza lako ukiambiwa kuna maziko basi utasikia kila mwanamme, kila mama anakwenda kwenye maziko au shughuli kama ni harusi katika familia kuweza kwenda kujumuika au kuwafariji watu au familia au ndugu na marafiki.

Lakini ni kweli kabisa ukiwauliza kinababa wengine kufuatilia matokeo, mwalimu wa skuli na walimu wa madrasa hata kuwajua hawapiti wala hawawaelewi. Kwa hivyo, nashauri sana kwamba mkazo utiliwe kwa kupitia kwa masheha pamoja na walimu kuwaandikia mabarua rasmi wakati mwengine na vipindi vya televisheni Zanzibar, vitowe zile katuni kama za kolera kuwahimiza wakinababa kushiriki katika malezi na mfumo mzima wa maendeleo na elimu na mustakabali mzima wa mtoto, kutoka anapoanza kwenda shuleni au skuli au pamoja na madrasa na pale anaposhiriki pia katika vipindi ambavyo ni *extra* vya *curriculum*, kama kucheza mchezo kama ni mpira au ni ufundi, basi waelewe mtoto anakwenda wapi na nani anakuwa anamsimamia na ijulikane katika jamii pia hawa watu wote ni aina gani.

Mhe. Mwenyekiti, pia na hizi madrasa zinazofumuka katika maeneo ya kulea watoto katika maeneo tofauti, basi hawa wanaoingia katika biashara hizi watambulike rasmi kwenye utaratibu wa mfumo katika sheria za kwenye jamii, kutoka kwa upande wa sheha mpaka kuja ngazi ya wilaya na mkoa, sio lazima ziende katika serikali kuu. Lakini katika mfumo wa ugatuzi tujuwe katika maeneo ya shehia zetu wale ambao wanalea watoto au nyumba ambazo wanasomesha ikiwa ni *tuition*, madrasa na elimu ya pembeni basi wote watambulike.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilizungumza suala la *uniform* kwa ajili ya walimu wetu. Nisingependa niliongelee sana, lakini kwa sababu nachangia hii hoja, nafikiri nikipata nafasi nitakuja kulifafanua zaidi na kuliunganisha hapa jinsi gani litatusaidia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza suala la *DVD* katika mchango wangu na kwenye hii hoja zijaliona humu, lakini najua katika maazimio yaliyotolewa, nashauri sana Mhe. Waziri alitafutie katika haya maazimio ambayo Mhe. Waziri ameyataja wizara husika waangalie hawa vijana ambao wanauza *DVD* au kanda za njiani wanaotembea, hazistahiki kwa watoto wetu kuziuza au kuwa ni mfano kwa ajili ya hawa maadui katika jamii, basi ziondoshwe mara moja na zile zinazostahiki yatembezwe katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nichangie katika haya maazimio. Mimi nataka niyachangie katika azimio namba 3, 4 na azimio namba 5 nafikiria. Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika azimio namba 3 suala la elimu litakapotoka basi nashauri sana. Ukisoma hili azimio namba 3 linasema hivi:

> "Ili kuipatia jamii uelewa na matatizo serikali itaandaa siku maalum ya kupinga udhalilishaji na mambo mengine na kadhalika".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sisi tuliokuwemo humu ndani, basi tushirikishwe kikamilifu katika mambo yote ambayo yatakuwa yanafanyika, ili

Mhe. Waziri upate *support* ya kutosha na wananchi wetu watuone tunakuunga mkono, na wewe mwenyewe pia tuweze kukusaidia kwa yale yote ambayo unayakususudia. Hili naliunganisha katika wizara yako pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa mambo yote ambayo mtashirikiana kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukisoma azimio namba 5 linasema hivi:

> "Pamoja na marekebisho hayo serikali iweke utaratibu wa kisheria kuwachukulia hatua kali wahusika wa kesi, ambao watachukua hatua ya kusuluhishana katika ngazi za kijamii".

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana, panapotokezea tatizo mara nyingi ndugu na familia hutafuta viongozi wenye nafasi ndani ya serikali, ndani ya kijamii au ndani ya Chama cha Mapinduzi, kwenda kujaribu kusuluhisha suala hili. Mimi nashauri sana Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri, ikiwa kiongozi ndani ya serikali au ndani ya chama atahusika katika suala zima la kusuluhisha, basi utaratibu uanze moja kwa moja wa hatua za kinidhamu aidha kumsimamisha kazi na ikiwezekana amefika mbali, basi mafao yake ambayo atakapomaliza kazi yake yafutwe yote, ili kuhakikisha watu ambao wanajaribu kusuluhisha masuala haya wanakaa mbali na wale mashahidi wanapotoa maelezo yao, basi yawe na nguvu zaidi kuliko yule mtu ambaye anatumia nafasi yake ndani ya serikali kujaribu kufuta hizi kesi.

Ukitaka mfano Mhe. Mwenyekiti, angalia kesi za *traffic*. Ukiangalia matatizo ambayo yapo barabarani na kesi ambazo zinafika mahakamani, basi hazilingani kabisa. Utamkuta mtu wanamalizana kutokana na kusaidiana. Lakini katika kesi ya udhalilishaji hii basi iwe ni jambo ambalo mtu akitafakari iwe ni moto asilikaribie, na pale akikutikana basi katika hii sheria ambayo Mhe. Waziri sheria ya adhabu Na.6 ya mwaka 2004 iunganishwe hapa kuhakikisha kwamba viongozi wote wanakaa mbali.

Lakini pia kwenye azimio Namba 4 nataka nishauri Mhe. Mwenyekiti kwenye Azimio Namba 4 linazungumza kwamba serikali ndani ya mwaka mmoja ilete katika Baraza la Wawakilishi Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Namba 7 ya mwaka 2004, lakini pia lengo lake hili ni kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho ya kifungu Namba 150(1) ili kuingiza makosa ya kujamiiana kuwa miongoni mwa makosa yasiyopatiwa dhamana. Mhe. Mwenyekiti, endapo mtu atagundulikana na makosa haya na akichezea hiki kifungo nashauri sana wanapoingia kwenye magereza basi wasichanganywe na wafungwa wengine, kwa sababu hawa ni wadudu kama *Virus* hatujui kiasi gani hawa wananchi wanafanya uchafu huu wameathirika kiakili. Wanapoingizwa katika magereza yetu wanakwenda kuchanganywa na watu wengine wanaochezea adhabu ikiwa ni ya wizi, uhalifu au ya *traffic* au jambo ambalo mtu amefungwa kwa bahati mbaya. Lakini anachanganywa na mtu ambaye amefanya kosa la uchafu ambalo halizungumziki na anaishi nae miaka mitatu au mitano, tutarajie nini yule mtu ambae anapotoka nje kuja katika jamii.

Mimi nashauri sana wafungwa hawa wanapoingia gerezani basi watengwe kutoka nguo zao, mavazi yao na mwenendo mzima wa kesi zao wanapofika Mahakamani wawe wanavaa rangi ambayo mtu akimuona asimkaribie, wazungu wanaita *the shame list* mtu ambaye huyu hafai hata kumuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sitochukua muda wako mkubwa sana mimi naunga mkono hoja naomba sana Mhe. Waziri yale maazimio yote ambayo ameyazungumza hapa yote yafanyike kwa haraka sana, na zile sheria ambazo tutakuja kuzibadilisha ziletwe tuzifanyie kazi ili wananchi wetu waweze kupata matumaini. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja mia juu ya mia ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Waheshimiwa kwanza kuna tangazo naomba tuwatambue wageni wetu wa leo hapa katika ukumbi huu ambao kuwa ni wageni wa Mhe. Abdalla Maulid Diwani wa jimbo la Jang'ombe hawa ni wajasiriamali wa viguta *Mikoba Group Union* wakijishughulisha na ujenzi wa nyumba za bei nafuu, ofisi yao ipo Dar es Salaam maeneo ya posta. Wageni wenyewe ni kama wafuatao.

1. Ngugu Iddi Mtoro
2. Ibrahim Daud
3. Jeremiya Richard
4. Salmin Daud.

Nasema karibuni sana Mhe. Suleiman Sarahan endelea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache kwa kadhia hii ambayo imetufika katika nchi yetu, Mhe. Mwenyekiti awali ya yote nimpongeze Dkt. Ali Mohammed Shein katika jitihada zake kubwa za kulikemea sana jambo hili na kwa kweli sisi tunamuunga mkono kwa hali na mali kwa sababu linaharibu kizazi ambacho tunakitegemea baadae.

Mhe. Mwenyekiti, mimi pia nataka niseme kidogo kuhusu suala la mashine ya *DNA* hii mashine tunaitafuta kwa hali na mali lakini Mhe. Waziri juzi alipokuja alitoa indhari Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Mahamoud labda watu walitegemea hivyo itakavyotumika itakuwa sivyo watu walivyotegemea, maana yake watu waliona kila mtu ambae kama kazaa mtoto atampeleka pale akamtizame ni wake au sio wake. Lakini mashine ni ya kwa sababu maalum ambazo zitakuwa za kisheria ambazo zitatumika kwa masuala hayo mengine Mhe. Waziri naona ameshaanza kuyatolea hoja naona kidogo watu walipungua nguvu kuhusu mashine ya ***DNA***, watu walitegemea hayo. Kwa hivyo labda tumuombe Waziri tena apunguze masharti ili tufanye hayo lakini kwa hili Mhe. Waziri alishatoa indhani kwamba itatumika kwa kazi maalum.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Waziri kwamba pamoja na sheria zake lakini kuna watu wana pesa zao wanataka kuhalalisha mambo yao, basi aweke kiwango angalau cha milioni moja kama mtu anataka akatizame kadhia ya nyumbani lakini akimkatiza kabisa kabisa wale wenye pesa zao hutaka kuji-*proud* sasa hivi si kuna watu wananunua namba za gari milioni kumi na tano milioni ngapi, basi na yeye aweke kwamba milioni tano ukitaka kuja kumtizama mtoto njoo. Lakini najua watu wa chini watakuwa hawafikii huko lakini wale wanaoji-*proud* kwamba mtoto wangu huyu nimempima basi wapewe uhuru, lakini milioni kumi, milioni tano tupate kununua nyengine Mhe. Waziri au kufanya mambo mengine tusiifunge tutoe mwanya lakini uwe mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba hii mashine ya DNA mashine inapima pengine ina ukweli kwa asilimia 80% lakini watendaji nao pia wana kasoro zao kama binaadam ni kitu cha msingi sana wakawekwa watu ambao wamekubali kujipima na dini wamekubali ukweli, tunayo mifano mingi tumeona kwa sababu waliokuwa kidogo miaka ya nyuma wakifuatilia fuatilia tulikuwa na mwimbaji mmoja Michael Jackson aliwekwa karibu makosa kumi, nilikuwa nafanyiwa usahihisho yalikuwa 31 sijui makosa mengi na yalionyeshwa katika *TV live* lakini Mheshimiwa yule Mwenyezi Mungu alimjaalia hata kosa moja hana. Lakini katika sisi hapa tungelisema katika makosa yote basi hata moja hana lakini kama hana ndio hana, kwa hivyo lazima tuangalie ukweli wa masuala haya tusiyapigie chapuo baadae yakaja yakawa na mashaka makubwa sana hasa kwa nchi yetu dini ipo, siasa ipo na kila mtu uelewa wake ulivyo hili suala ni kwamba tunaliona mchango mkubwa ni viongozi wetu wa dini lakini wameondoka asilimia kubwa kwenye mustakabali wao wa kufundisha watu wamekamata siasa.

Hivi sasa kesho kutwa utakuta watu wanakula sikukuu mbili na mashehe ndio wanaotangaza mambo haya baada ya kukamata haya mambo ambayo yana maana na kadhia katika nchi yetu wanajikita kwenye siasa zaidi kuliko mambo hayo, sasa niangalie vizuri kwa Mhe. Waziri wa Afya hii DNA itumike kama ulivyokusudia mwenyewe isije ikatuletea balaa kubwa sana badala ya kuwa na faida juu yetu.

Lakini kwenye kesi hapo nilimsikia Waziri akizungumza habari ya mashahidi kuhusu kuja sijui kufanya kitu gani, lakini na nauli zisije zikawa zinachelewa kama anapelekewa sheha kama anapelekwa kitu gani ipitie kwa sheha kabla ya tarehe yake kupelekewa asijekuwa na sababu hana nauli, maana yake sasa mtindo wa nauli ndio unatoa sababu kubwa na huwezi kumpinga huwezi kujua kipimo chake kwamba yule bwana pesa au hana. Kwa hivyo hilo ningeomba sana ulitizame kwamba mtu huyu vigezo vyake vya nauli anakabidhiwa kabisa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, Waziri atakapokuja aje atwambie hicho chanzo kikubwa cha hii kamati imeona nini ambacho matatizo haya ambayo yametukabili angalau wameona chanzo nini katika kuona hatua za mwanzo, ili ifike kuja kututizama kwamba tumefikiwa na nini chanzo chake nini mambo haya yaliyotufika maana yake kila kukicha yanazidi. Lakini mimi nilifikiri kwamba kila kukicha yatapungua kwa sababu kama mashehe wetu wanavyotwambia sasa hivi Mheshimiwa mijini kumeharibika watu wanakwenda bila ya nguo lakini zaidi wanaoathirika ni watoto sana. Sijui ata wazee tumefikwa na nini katika masuala kama haya mimi nafikiri ni laana inayotupiga hii, lakini sifikirii kwamba kuna aina yoyote ya raha au jambo lolote mtu ambalo anafuata kwa mtoto zaidi ya laana ambayo inatufika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna udhalilishaji mwengine unakuwa sio huo tunaoufikiria tu mimi ningeomba Wizara ya Wanawake na Watoto ikafanya jitihada kubwa za kupita kijiji kwa kijiji, kuna udhalilishaji wa wazee watoto wao wanawadhalilisha, kuna udhalilishaji wa vilema kuna watu wamewakomelea ndani hawapeleki shule wala hawafanyi chochote na wanawakomelea ndani. Kuna udhalilishaji wa watoto wanaolelewa tunaona kwenye mitandao, tujaribu sana kupita kwenye vijiji na kuangalia nini ambacho adha nyengine inatufika. Tunaona kwenye mitandao kuna mpaka kina dada wanawachukua watoto wadogo wanawadhalilisha watoto wa kiume wanawadhalilisha madada. Kwa hivyo tunagalie sana Wizara ya Wanawake na Watoto badala ya kuwa ilete ripoti ipitie vijiji kwa vijiji tena ule wakati wa mchana ambao wazazi hawapo wapate kujua taswira nzima nini ambacho hapa kipo katika maelezo, hodi salama

hamjambo wanaangalia wanajua, tunapata utaratibu wa kuangalia nini ambacho kinaweza kikatokea pale. Kwa sababu ukigonga nyumba ukichungulia tu ukiangalia unajua kama hapa kuna tatizo gani uweze kulifanyia ufuatiliaji.

Lakini jengine ni kwamba Wizara hiyo hiyo isichukulie kwamba Masheha wapo sijui watu gani wapo wao ndio wachukue jukumu la kufika vijijini kutembea na Sheha, kutembea na watu wengine sio kwamba Sheha atoke huko kwa kwenda kwa Wanawake na watoto, kuna watu wengine wanazijua siri lakini hawawezi kusema. Lakini pia Waziri weka mtandao wako wazi waambie hasa mtandao wa wanawake na watoto wa udhalilishaji huu, nitumie *message* pahali fulani kuna mtoto anadhalilishwa weka wazi, waambie mtandao huu ukae wazi kwamba mtu yoyote anayekutumia meseji udhalilishaji kwenye nyumba fulani upo ili asionekane kwa sababu anatoa siri wengine hawawezi wanaogopa kutokana na matatizo ambayo yapo. Kuna wanaume wanapiga watoto wao mpaka wanataka kuwaua hakuna kusema naogopa mie kuja kunipiga akaniua kwa hivyo weka mtandao wazi waujue kwamba mtandao upo ambao utarushwa tu na wewe utafuatilia kwa mtandao wako, kwa hivyo ningeomba kwamba maelezo ni hayo.

Lakini pia wazazi kuhusu mitandao ya simu ambayo watoto wadogo wa miaka kumi mtoto anapewa simu linafika hapa na kashatiliwa na MB anachati anachotaka, anaangalia mambo umri wake haujafika anataka kuyajaribu hawezi kuyajaribu kwa mtu mzima atajaribu kwa mtoto mwenziwe. Kwa hivyo ni mambo ambayo wazazi wenye uwezo tumezidi na wazazi wasiokuwa na uwezo wao wana mitandao yao wanalala nyumba moja na mtoto ambae umri umeshaanza kuwa mkubwa anafahamu wanamuonesha mambo ambayo siyo, kwa hivyo lazima hizi taaluma yote yale madhara yake ndio yanajiletea baadae. Mimi pale Chake Chake Mgogoni kuna siku moja tulikuwa na huyu Mkuu wa Mkoa tuliwakamata watoto wasiopungua sita wote wanafanya mshikaki watoto wa kiume wote ….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman muda.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Da! Mheshimiwa kidogo tu namalizia…

Mhe. Mwenyekiti: Malizia muda na wengine malizia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Sasa Mheshimiwa…..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe, nakupa dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nizungumze na Mwenyekiti na kauli ya Serikali hebu kauli ya Serikali iweke wazi haya mashule pamoja na madrasa bado kupiga wanafunzi ipo au haipo tena au inakuwaje, maana yake kila mmoja anachukua sheria mkononi mwake, Sasa serikali itakapokuja itwambie imeshapiga marufuku kupiga mtoto na kama anapigwa ni kiasi gani au adhabu yake iwe kiasi gani. Kuna watu wa madrasa anakwambia mimi napiga tu nitajua mwenyewe kwa hivyo hili kidogo tuliangalie.

Jengine ni kwamba hata mashehe wetu katika vyanzo ambavyo wengine wanatuletea ni kwamba sasa hivi kumekuja na mitandao mingi ya mashehe hawa akina Kipozeo na nani, unajua sasa hivi akina mama wengi wameingia katika dini wanavaa majuba wanavaa kitu gani, akina mama ndani

hawamalizi shughuli za mzee inakuwa tabu kweli kweli mpaka mashehe wanapiga kelele. Mzee yule wa kiume akitoka mule akili hana anaweza kwenda kumvamia mtu yoyote nje kutokana na akili zake, kwa sababu wengine kuowa wake wanne hawawezi. Huyo mmoja na nyumbani hupati kitu unashindwa na ndio mashehe wetu sasa hivi wanasema kina mama lile jambo ambalo mnalijua litekelezeni sio mbadilike. Kwa hivyo ni moja katika mambo mengine ambayo akina mama wanakuwa hawatekelezi wajibu wao vizuri wanawapa akina baba kwenda kufanya mambo yasiyokuwa ya lazima kwa hivyo lazima mambo haya wayaangalie sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti…..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa naomba unilinde nina moja tu moja wanaume wanaotelekeza wake zao na watoto. Bado serikali haijachukua hatua za watu hawa wengine wanafanya kazi serikalini ambao serikali ina mkono wake wa kushika ule mshahara wake, mimi natoa wazo kwamba kama mtu ambae anafanya kazi serikalini ambae ametelekeza wanawake na watoto mshahara wake moja kwa moja wote uende kwa wanawake na watoto kwenye mama, ili mama yule aweze kujikidhi na watoto wale wasipate kusambaratika.

Mheshimiwa naungam kono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ninamuita Mhe. Mwanaasha na baadae nitamuita Mhe. Waziri wa Afya kwa dharura maalum.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii niseme machache kuhusiana na maelezo ya utekelezaji wa maazimio ya hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na uimarishaji wa mfumo mzima wa kisheria unaohusiana uendeshaji wa kesi za udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Rais wa Zanzibar kwa kuona kuwa ipo haja ya yale majumuisho yote ambayo yameletwa ndani ya Baraza hili katika hoja binafsi ya Mheshimiwa Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Kiwengwa, kwa hivyo niipongeze Serikali kwa kutuletea maelezo haya. Lakini pia nimpongeze sana muwasilishaji Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed nae kwa kutoa hoja hii au kuleta hoja hii hapa Barazani kwa niaba ya serikali kwa hivyo niwapongeze sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja kuhusiana na azimio la siri kuhusiana na suala zima la *DNA.* Naipongeza sana serikali kwa kuona kuwa ipo haja sasa hivi katika bajeti iliyopita kutokana na jawabu aliyotupa humu kuwa tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya kununua hiyo mashine ya *DNA*, Mhe. Mwenyekiti, hichi kilikuwa ni kilio cha muda mrefu sana kwa wananchi wa Zanzibar hususan wanawake ambao wanafanyiwa masuala mazima ya udhalilishaji. Kwa hivyo nina imani leo hii watu wetu wote watakuwa wamefarijika kuona kuwa mashine hii tayari imo katika bajeti ya 2017/2018 mwaka huu wa fedha basi itanunuliwa ili iweze kutoa nusura kwa hao wote wanaofanyiwa vitendo hivyo vya uzalilishaji, naipongeza sana Serikali.

Lakini jengine pia Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nije katika azimio la nne kuhusiana na uwezo wa Mahakama ya Mkoa kutoa kifungo zaidi ya miaka saba ya makosa mbali mbali yakiwemo makosa ya udhalilishaji, pia nipongeze ripoti hii kuhusiana na suala zima la sheria ya mwenendo wa kosa la jinai 2007/2014 kupendekeza marekebisho ya makosa ya kujamiiana kuwa ni miongoni mwa makosa yasiyokuwa na dhamana. Mhe. Mwenyekiti, tupongeze sana uamuzi huu wa Serikali kuona kuwa mapendekezo yataletwa tuone tunabadilisha vipi kuhusiana na suala zima la haya makosa ya jinai yasipewe dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi walikuwa wakilalamika hususan na sheria hii kuhusiana na sheria namba saba ya makosa hayo ya jinai, kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti tumefarijika na tumeona kuwa kile kilio chetu cha muda mrefu sasa hivi kimeshapata muarubaini na nina imani wananchi watajenga imani na serikali yao, kwa sababu hapo mwanzo makosa haya yalikuwa yanatolewa dhamana na yule anayefanya kesi hii ya udhalilishaji akishapewa dhamana anajiona yeye ndio bingwa mitaani na inawezekana akafanya tena tendo lile kwa mtu mwengine. Lakini hapa kama sheria hii italetwa basi nina imani tutaondosha ile tabu ya wale wanaoathirika na suala hili, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali ilete mapema iwe ni mswada wa dharura ili tubadilishe hii sheria ipate kufanya kazi ipasavyo ili hili suala la udhalilishaji ambalo limekuwa ndiyo kilio kikubwa kwa wananchi, ni kilio kikubwa kwa akina mama, tuone tunalifanyia kazi na wananchi watajenga imani kwa serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niipongeze sana ripoti hii kwa sababu tayari tumeshaona kuwa sisi Wawakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi tuna haki ya kusimamia na kuihoji serikali ili na wao wabebe yale mapendekezo yetu tunayoyatoa na kuyafanyia kazi. Hili limedhihirika leo kwa sababu tayari yale maazimio yote yaliyoletwa katika hoja binafsi ya Mhe. Asha Abdalla Mussa ya kuhusiana na suala zima la udhalilishaji, serikali imelipa upana wake na wametuletea ripoti hii na kuifanyia kazi.

Kwa hivyo naiomba serikali hii ripoti isibaki tu katika karatasi, lakini iletwe kwa mara moja yale ambayo wameyakubali yafanyiwe kazi, basi naomba serikali ifanyie kazi kwa mara moja ili tujenge imani kwa wananchi wetu waliotuchagua na wanawake wote tuliowakilisha ndani ya Baraza hili tukufu tayari watakuwa na imani na serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa sina mengi zaidi nilikuwa nataka niseme tu hayo na kuipongeza sana serikali kwa kutuletea majibu ya maazimio hayo na naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia ili ifanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanaasha, sasa namwita Mhe. Waziri wa Afya na baadaye Mhe. Mwinyihaji Makame ajitayarishe.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, kwanza na mimi naomba nimshukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa kuja na maazimio haya ambayo pia yatasaidia kuelimisha jamii maana mengi yapo na serikali hii inafanya kazi kubwa sana.

Kwanza kabisa naomba nimnukuu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 12/01/2017 akiadhimisha miaka 53 ya Mapinduzi

Matukufu ya Zanzibar kuhusiana na suala hili na azimio ambalo yeye tayari ameshalipanga leo sisi tunaendeleza tu.

Ukurasa wa 40 naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti,

"Aidha katika kukabiliana na vitendo vya udhalilisha wa wanawake na watoto hapa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendeleza Kampeni kwa kupiga vita vitendo hivyo ambapo vituo vya mkono kwa mkono vimesaidia sana. Wananchi wengi wametuunga mkono katika mapambano haya. Hata hivyo tatizo la udhalilishaji bado lipo. Katika mwaka huu serikali itaandaa mikakati maalum katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto hapa Zanzibar. Natoa wito kwamba sote tushirikiane kwa pamoja katika kuvikomesha vitendo hivi viovu"

Mwisho wa kunukuu, haya ni maneno ya Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uwanja wa Amani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tayari baadhi yake yameshatimizwa na namshukuru sana Mhe. Mohammeid Bin Aboud (Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais) kila moja ya maazimio haya ametutolea ufafanuzi wa kutosha naomba nimpongeze sana kwa umahiri wake. Mimi nitajaribu kuongezea ongezea katika yale ambayo Mhe. Rais ameshayatamka, Mhe. Asha ameyarejea na Mhe. Mohammed Aboud ametoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika Azimio Nam. 4 mnamo tarehe 10 Februari 2017 tulikaa pamoja chini ya Uwenyekiti wa Mhe. Maudline Castico (Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto) tulikaa pamoja. Hii naomba niseme Mhe. Mwenyekiti, nakuwambia Waheshimiwa Wajumbe ilikuwa ni *operation* maalum siyo *operation* ya mchezo nayo imepewa jina ya *operation* "Maliza Udhalilishaji Zanzibar".

Katika *operation* ile siwezi kutamka yote yaliyopangwa, lakini katika *operation* ile yamepangwa mengi na moja wapo hili alilolitaja Mhe. kwamba watuhumiwa wa makosa haya wasipatiwe dhamana. Sisi tunajua nini kimepangwa Sheria itarekebishwa lakini tunajua nini kimepangwa. Mhe. Simai Mohammed Said, amerudia pale amesema kwamba mtu anayefanya makosa haya apate ule ukali ajisikie amepata ule ukali.

Naomba nitamke rasmi baada ya terehe ile ya 10/02/2017 kuanzishwa *operation* hii udhalilishaji umepungua kwa kiasi kikubwa hapa Zanziar. *Operation* ile imefanya kazi na mimi napeleka tena ombi kupitia kwakwe Mhe. Waziri kupitia serikali yangu, kwamba *operation* ile iwe endelevu isite pale. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi watupe mashirikiano yao tunapoendeleza *operation* ile, wasija wakalalamika ukali unapozidi, *operation* ile watupe dhamana na watupe mashirikiano yao, watuunge mkono. Mhe. Rais keshasema kwamba tutapiga vita vikali kabisa katika vitendo hivi viovu. Mimi ni mjumbe wa hii *operation* na *operation* hiyo tunaendelea nayo.

Kuhusu huyu kijana aliyepigwa hivi karibuni, inatuhumiwa kwamba kapigwa mpaka kauwawa Kisiwani Pemba. Naomba niseme wazi kwamba Wizara yangu Wizara ya Afya imeshapokea barua rasmi kutoka vyombo vinavyohusika na sheria katika kufanya uchunguzi kutoa mtaalamu

wetu kwenda Kisiwani Pemba kufukua kaburi. Huyu mtaalamu tunayemtoa ni mtaalamu bingwa kwa hapa Zanzibar wa kupekuwa maiti na kufahamu maiti ile sababu za kifo kilichosababishwa.

Naomba niseme serikali tayari imeshachukua hatua haikukubali, imeshachukua hatua yakulifanyia uchunguzi na tayari kibali cha kufukua kaburi imeshatolewa na tayari mtaalamu wetu sisi tumeshamruhusu kwenda kisiwani Pemba. Bado sijapa mrejesho ya majibu yake baada ya kurudi safari yake Pemba ni Dokta Marijani Msafiri aliyekuwepo pale Hospitali ya Mnazimmoja huyu ni mtaalamu bingwa wa masuala ya *pathology* kuangalia mwili wa binaadamu hata ukiwa umeharibika ana uwezo yeye wa kuangalia mwili wa binaadamu kwamba kifo kile kimesababishwa na nini. Ushahidi huo utatolewa na kufikishwa kwenye vyombo husika vya sheria na sheria itafuata mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili nilitolee ufafanuzi barua hiyo tumeipokea na hatua husika Wizara yetu tumeshachukua kwa hilo, hatobakishwa mtu. Naomba nimpongeze tena Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kasema humu ushahidi lazima utolewe kwa mashirikiano na yule anayekataa kutoa ushahidi pia tutamchukulia hatua. Sheria ile ya ushahidi mpya imepitishwa yule atakaekataa ama yule atakaeshiriki katika kujaribu kupatanisha, kufifirisha ama kuwarubuni wale wazazi ili ule ushahidi wasiendelee kuutoa basi serikali nayo ina mkono wake na ina mkondo wake itachukua mkondo wake katika kufanikisha masuala ya ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la hii mashine ya *DNA*. Kama alivyotamka Mhe. Rais katika nukuu niliyoitoa ya hotuba yake tunamshukuru serikali imepanga fungu maalum la bajeti, tayari tumeshapata *invoice* ya mashine ya *DNA* hivi sasa ipo pale Wizarani, tunafuata taratibu tu zile za kufanya tenda na ununuzi, baada ya hapo mashine hii itanunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kupitia Baraza lako Tukufu yule aliyekusudia kukifanya kitendo kama hichi ama ana dhamira, ama ana nia, ama anataka, ama anafikiria, ama anaota, aache mara moja kabla ya mashine hii haijaja. Mashine hii inampeleka mtu moja kwa moja bila ya kurejea nyuma au kuangalia chochote inampeleka moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, ikitumika kwako wewe hapa mashine hii itakuwa inauwezo wa *trace* mpaka babu yako alikotokea ina uwezo huo, siyo wewe tu. Wewe mzazi wako mpaka *third generation* inayo uwezo huo inafanya *tracing* mashine ya *DNA* ya kisasa kabisa. Nimebahatika kidogo kusoma soma yale makaratasi na *inshaallah* ikifika tutakaobahatika tutaandaa utaratibu maalum wa Wawakilishi wote. Kwa wananchi wote anaefikiria naomba tafadhali hili liishe mara moja.

La pili hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha ametaja Mhe. Mohammed Aboud amejibu, mimi nilikaa na watendaji wangu Wizarani kuhusiana na hivi vituo vya Mkono kwa mkono. Watendaji wangu na wao wakawa na mawazo yale yale kwamba tuongeze vituo vya Mkono kwa mkono vifunguliwe kwa saa 24 kwa siku kuwe na wataalamu zaidi kwa sababu mle ndani kuna madeksi matatu lipo deksi la Mhe. Maudline Castico mtu wake anakaa, lipo deksi la polisi ambalo lipo Chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na lipo deksi langu mimi la mtu wetu wa Afya anayekaa kufanya ule uchunguzi. Mkono kwa mkono ndiyo imegawika *section* tatu, sasa wale watendaji wangu walivyokuwa wakinambia tufungue hivi vituo viwe vingi zaidi. Nikawauliza kwani tunategemea huu udhalilisha wa watoto kuongezeka Zanzibar?

Naomba niseme tena sisi sote kwa pamoja tunatarajia udhalilisha wa watoto utapungua na utatoweka kabisa Zanzibar, kwa hivyo hatutaongeza idadi ya vituo vya Mkono kwa mkono bali tutaimarisha viwe vikali zaidi. Tutaimarisha vitoe huduma za saa 24 lakini hatutarajii kesi hizi zitaongezeka. Safari hii mtu akenda ndani huko Mhe. Haji Omar Kheir yupo kule Mafunzo tutahakikisha ile miaka yake aliyopangiwa kwa adhabu ile basi inakuwa miaka ile zaidi ya ile. Tutahakikisha hilo kwa sababu tunataka kukomesha, vitendo vingi tumeweza kukomesha kwenye jamii, wizi mdogo mdogo umepungua sasa hivi na hii takwimu inatuonyesha imepungua baada ya kuanzisha kampeni hii maalum ya *operation* ya "Maliza Udhalilishaji Zanzibar" ambayo tunaihusisha pia Tawala za Mikoa, Wakuu wa Mikoa wamo, Wakuu wa Wakuu wa Wilaya wamo ndani mle.

Naomba nitamke tena niseme kwamba vituo vya Mkono kwa Mkono vitaendelea kuimarisha kazi yake ya kufanya, hao waliokuwa wameajiriwa wapya wataendelea kufanya kazi zao vizuri, watapatiwa mafunzo vizuri. Ushahidi hatutokubali sisi tutashirikiana na Mhe. Waziri Castico, tutashirikiana na Afisi ya Mhe. Mohammed Aboud na tutashirikiana na Afisi ya Mhe. Haji Omar Kheir, kuhakikisha kwamba hatua husika zinachukuliwa. Lakini hatutoongeza vituo kwa sababu hatutarajii kesi hizi zitaongezeka Zanzibar.

Naomba niseme tena Mhe. Mwenyekiti, ni jukumu letu sote tulilokuwemo katika Baraza hili tukufu, sisi tuliyokuwepo mbele na wenzetu waliyokuwa nyuma yetu kupiga vita ili udhalilishaji wa aina hii uondoke Zanzibar. Huu siyo utamaduni wetu, huu haukuwepo hapo awali wala hatutarajii kama utaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuhusiana na masuala ya ushahidi, ushahidi sisi tutaendelea kutoa mashirikiano yetu afisi ya *DPP*, polisi wale wanaohusiana na ushahidi. *DPP* naomba niseme kwamba ni mjumbe mzuri sana, mahiri wa hii Kamati yetu ya hii "Maliza Udhalilishaji Zanziar "*operation* maalum yeye ni mjumbe halali, ni mjumbe *very active* ni mjumbe ambaye anafanya kazi yake vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tutaendelea kumsaidia yeye kuhakikisha kwamba ule ushahidi unakamilika. Hapa tulipo hivi sasa tayari tunavifaa vya kutosha vya kukamilisha ushahidi mbali mbali. Mara nyingi huwa tunapata matatizo pale tunapopeleka Mahakamani wakawa wale mashahidi hawahudhurii ama hawapati fursa ama nafasi ya kuweza kuja. Lakini na hilo nalo kwa kushirikiana pamoja naamini nalo tutaliweza na tutalitatua na tutaweza kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa mara nyengine tena nitamke na kunukuu maneno aliyotamka Mhe. Mohammed Aboud katika ukurasa wa 5 wa kutoa ufafanuzi juu ya maazimio haya:

> "Yeyote atakayeshiriki au atakesimamia usuluhishi wa kesi za udhalilishaji awe ni mshiriki wa kosa na yeye pia awe ni mshiriki wa kosa na ashtakiwe kwa kosa lile lile".

Naomba wale wanaojiingiza ingiza katikati katika kuleta ushuluhishi basi hili waliangalie vizuri sana na ikithibitika watapata adhabu ya kosa hilo la udhalilishaji. Marekebisho ya wahusika yote ya sheria, naamini haya yataletwa sote kwa pamoja tukishirikiana na tayari tutayafanyia kazi kupitia Baraza hili tukufu la Wawakilishi.

Namalizia kabisa mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, serikali tayari imeunda Kamati ya Mawaziri amelitamka hili hakuna haja ya kuwa tena na siku maalum ya udhalilishaji nimeshatamka hapo wazi mwanzo hatutarajii kuongeza udhalilishaji Zanzibar, tunatarajia kumaliza, kwa hivyo hakuna tena kuweka siku maalum ya Udhalilishaji. Zipo siku maalum kama ya mtoto wa Afrika, ipo siku maalum ya Mwanamke wa Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tayari serikali imeshaunda Kamati ya Mawaziri inajumuisha Wizara zote zinazosimamia masuala haya ya wanawake na watoto, Wizara ya Sheria, Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Mkurugenzi wa Mashtaka, Polisi na Tawala za Mikoa. Tumeshakaa vikao kadhaa na kupanga mambo kadhaa, huko tunakoelekea naomba kupitia Baraza lako tukufu nitoe hadhari kwa wananchi wote yeyote anayelifikiria suala hili naomba asilikaribie kabisa.

Operation maalum pamoja na hii Kamati maalum ambayo pia mimi ni mjumbe wa hii Kamati na ni Mjumbe ninayezungumza sana, wengine watazungumza kwa upande wao lakini mimi ni mjumbe ambaye nazungumza sana katika Kamati hii. Kwa sababu kila mmoja katika hii Kamati kabla hatujaingia tunakumbushana kama hivi ninavyozungumza na wewe Mwenyekiti, je mwenyekiti hili suala likimtokea mwanao utajihisi vipi? Anza kufikiria hilo kwanza, ukianza kufikiria hilo ndiyo utapata uchungu. Kila mmoja katika Baraza hili tukufu ajifikirie je, tatizo kama hili likimtokezea mwanawe atakuwaje. Wengine, kila mmoja Mungu amemuumba namna yake, wengine kwa hasira anaweza akafanya kosa na yeye kubwa zaidi la kuuwa. Mwengine kwa hasira akachukua sheria mkononi mwake, mwengine kwa hasira akafanya jambo lolote ambalo halijategemewa.

Sasa mimi huwa natoa tamko hilo kabla ya vikao vyetu kuanza kwamba naomba jamani kila mmoja aliyekuwemo humu ndani na leo nalirejea tena tamko hilo ndani ya Baraza la Wawakilishi, kila mmoja aliyekuwemo humu ndani ajifikirie je, suala hili likimtokezea mwanawe ndani ya *feeling* zake ndani ya hisia zake za ndani kabisa atakuwaje. Naomba nimalizie hapo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Afya kwa maelekezo yako na mchango wako. Niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe mnaochangia mwende zaidi katika hotuba iliyowasilishwa na Mhe. Waziri badala ya kuchangia kiujumla. Sasa namwita Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na baadaye Mhe. Chum Kombo Khamis ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia wasaa huu na mimi kuzungumza machache kuhusu maelezo ya utekelezaji wa maazimiyo ya hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na uimarishaji wa mfumo mzima wa kisheria unahusiana na uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto kama ulivyowasilishwa vyema kabisa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana Wizara kwa ujumla kwa kazi hii nzuri sana waliyoifanya ya awali. Ukitizama haya maazimio 13 humu yaliyotajwa, ukichambua moja baada ya jengine kwa kweli huna pa kupenya unaona yote yamekuwa wazungu wanasema *well covered*

yamezungumzwa kwa undani sana, wametoa hasa swali na jawabu wamelileta. Lakini kuzungumza ni jambo moja na utendaji ni suala jengine. Mimi ninachosema nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hii hatua ya awali kwanza kuyatambua haya matatizo. Maana suala siku zote muhimu ujuwe lile tatizo, ukishakujua tatizo sasa unajipanga uwende vipi. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri na ni vizuri zaidi kwa kuyaorodhesha pamoja na michango mizuri sana ya Waheshimiwa.

Sasa naomba nianzie kwenye hoja au Azimio Nam. 1 na jibu alilotoa naomba nisome moja tu. Anasema; "utekelezaji wa mpango huu utashirikisha wadau wote katika ngazi zote kuanzia Shehia hadi Taifa". Hapa Mhe. Waziri kamaliza, kamaliza kabisa ni *paragraph* ya kwanza kabisa ukurasa wa pili kuanzia Shehia hadi Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kweli kasema watashirikisha hivi sasa hivi ina maana haishirikishwi ipasavyo anatwambia wazi kwamba kwa kweli kama kila mmoja hafanyi wajibu wake ipasavyo, sasa mimi naomba kulisisitiza hilo Mhe. Mwenyikiti, kwamba kila aliye na wajibu wake katika suala hili akipelekewa au likimgusa basi afanye wajibu wake ipasavyo. Wamezungumza nimewasikiliza sana waheshimiwa wamezungumza vizuri sana wengine tunajaribu kusuluhisha kinyume na taratibu kinyume na sheria, wengine ahaa zile kesi usiipeleke mbali tuimalize huku huku mpe mume mtoto au mpe mke mtoto tunayamaliza hatujui mambo yalivyokwenda, yamekwendaje au na nini.

Lakini baya zaidi linalonigusa Mhe. Mwenyekiti nimependa hii *title* ya Mhe. Waziri, anasema uimarishaji wa mfumo mzima wa kisheria hapa ndio *keyword* mfumo mzima wa kisheria sasa ina maana Mhe. Mwenyekiti, kuna pengo hapa, kuna pengo katika sheria zetu katika masuala haya au kama pengo halipo naweza kusahihishwa kama pengo hali halipo basi usimamizi wa hizi sheria tuna matatizo. Sasa mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri hili tulikazie, tunakubali muhimili wa mahakama *judiciary* hatuugusi wala hatuingilii wala hatupaswi kuujadili.

Lakini tunawaomba wenzetu ule mhimili nao ufanye kazi ipasavyo kuna wachache sana wanauharibu kesi haziendi ipasavyo mirungura imekuwa mingi, ushahidi unapotezwa imekuwa ule utawala bora tunaozungumzwa na Mhe. Rais wetu anaupigia kelele kila siku haupo, tunapozungumza *good governance* basi *the rule of law* usimamizi wa sheria Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo mimi nampongeza sana Mhe. Waziri hili la kukazia na maazimio mengi yamegusa humu, azimio namba nne, azimio namba tano la kukazia usimamizi wa sheria na mimi ningeshauri sana mwenyewe Mheshimiwa wana utaratibu wao wa kujiwekea *score card* kwa kila mfano mtendaji au kama jaji kesi ngapi kasikiliza, katika hizo kesi za udhalilishaji kazimaliza vipi? Maana jengine linalokera ndio hilo kesi hizi mara nyingi hazimaliziki *inconclusive* unakwenda wewe ushahidi, unakwenda wewe ndio mpaka waheshimiwa wanataka *DNA* ije sasa kusaidia huo ushahidi.

Namshukuru Jaji Mshibe hapa alikuja kupiga *lecture* nzuri sana wakati wa kupitisha ule Mswada wa Ushahidi katuelezea tuziwe waoga, kweli tusiwe waoga lakini wazee wenyewe na sisi tuna jukumu letu, tuna jukumu letu la kulimaliza hili suala lakini kila mzee anaona ahaa mwanangu tumeshafika hivi tena nende huko, nende huku ndoa za usiku usiku za mkeka linamalizwa unaambiwa eee bwana wewe kesho tukakutane tulimalize.

Mheshimiwa lingine Wizara nayo Mhe. Castico na timu yake tuna salamu kwamba na watendaji wa wizara wana vitengo vyao vya *cancelling* vya kuzungumza, kuwaliwaza wanaokosa na wanayamaliza mambo. Lakini wako wengine tunawaita kama *fighter,* wao wanataka huyu bwana aliyotenda lazima afikishwe kwenye vyombo vya sheria. Sasa ningeomba na wao ule ukali wao wa kuwatafuta kuwasaka uendelee sana. Naibu Spika, wetu ni mwanaharakati mzuri wa hili tufate mfano wake *Alhamdulillah,* yuko mwana mama daktari naye *very smart* naye tufate mfano wake pale anaye mwenyewe, Mhe. Mwenyekiti, nataka kuuliza sana suala hili.

Lakini jengine hivi tujiulize Mhe. Mwenyekiti, kwa nini yanatokea leo haya maana yake huku nyuma mbona hayakuwepo kabisa yote tuna *conclude* ni mmong'onyoko wa maadili. Sasa maadili mengine unafunzwa shuleni, mengine unafunzwa nyumbani, mengine unajifunza mwenyewe. Lakini kwa ujumla unasema maadili yameanguka sasa hili humu tunamomuweza kama shuleni, kwenye vyuo masomo yale ya *sociology*, saikolojia yawe *compulsory* kama kwenye vyuo wanafunzi, watu wa elimu wenyewe, madaktari, wanafahamu wenye hizi *profession* za kugusa jamii, za kugusa watu masomo haya ya lazima nashauri sana yasisitizwe, jinsi ya kuishi na watu juu ya tabia njema jua siku zote kumsomesha mtu na kusoma huchoki siku zote unaambiwa ujifunze na ukatafute popote elimu mpaka China tumeambiwa huko.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri sana na namuomba Mhe. Waziri wa Elimu najua wanayo mafunzo haya lakini kwa kweli kwa hapa tulipo sasa kwa jamii yetu mafunzo haya ya *sociology* na saikolojia kwa wanafunzi wetu yawe nayo kama *compulsory* yawe ya lazima kwa vijana wetu maadili wafundishwe, itategemea *level* ya Chuo Kikuu *level* gani, *level* ya *secondary level* gani, *level* ya msingi na kati *level* gani, maandalizi *level* gani lakini nahisi kwa sababu wazee sote muda wetu mdogo kukaa na watoto wetu na wao tena unajua kijana kabla ya baleghe, na baada ya baleghe wanakuwaje.

Sasa kinachouma zaidi chengine utashangaa hao ni watoto lakini watu wazima wewe ushafika miaka hamsini na mwana dini mzuri, mwana darasa unakwenda kufanya hayo unajiuliza,tatizo nini? Huyu anataka nini? Halafu huyo anaekwenda kumdhalilisha ni kijana mtoto hata hayo mambo *astaghfirullah* pengine wala hayajui au pengine ndio kwanza anajifundisha. Sasa wewe mzee mzima miaka hamsini hawa Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri hawa wapewe *CV* ya *punishment* kama nilivyozungumza.

Zamani Mhe. Mwenyekiti, wakati wa awamu yetu ya mwanzo baada ya mapinduzi hata awamu ya pili tulikuwa na sheria ya wanaowapa ujauzito watoto wadogo au waliokuwa hawajaolewa miaka mitano ukionekana umemtia mimba wewe miaka mitano unayo, kidogo ilisaidia sana Mheshimiwa ilikuwa hakuna kama ufanye kisiri uoe japo ilikuwa kisirisiri lakini ilikuwa kali sana ile sheria.

Sasa mimi nasema tusichoke Mhe. Mwenyekiti, lazima tukaze kamba na hasa hivi vizazi vyetu kama si hivyo sisi ndio *responsible* tukiwaachia tutalaumiwa sisi tumewalea vipi watoto, wametushinda vipi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba unaniangalia lakini mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kweli haya mambo kumi na tatu aliyoorodhesha yote ni mazito na yanahitaji kufanyiwa kazi na mimi ningeomba sana Mheshimiwa angeweka *plan work* mengine baada ya mwaka mmoja mimi

nasema afungue kama kalenda hasa la miaka miwili hili litafanywa baada ya muda gani, hili litafanywa muda gani tusaidiane tutamsaidia hili ni letu sisi ndio wawakilishi wenye majimbo. Mimi mara nyingi huwa ninaambiwa ehee bwana weee mtoto kidogo kaharibu mambo njoo tuyatengeneze, tuyatengeneze vipi tumkabidhi mume mimi nawaambia kwa hilo siji, hili siji kabisa. Yaani wewe unamuachia unalihalalisha hilo haya au mkabidhi mwenyewe ende zake huko ajuwe uchungu, ajue matatizo anayoyatafuta, japo Waziri wa Elimu anasema kakosea tu msaidie, ndiyo tutamsaidia vyengine sio hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono sana maazimio haya namuomba Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu hasa Mhe. Mwanasheria Mkuu sheria, sheria, sheria Komandoo alisema tuzisimamie ipasavyo hapa ndio penye matatizo yote Mhe. Mwenyekiti. Kama sheria tunazisimamia ipasavyo, tunazifuatilia sote kwa pamoja tunaonesha vidole bwana wewe ndio unaotukosea tutafika.

Lakini kama hatuzisimamii na wenyewe hasa Mhe. Mwanasheria Mkuu na Jaji Mkuu hasa wenye sheria wao ndio wawe mstari wa mbele Mheshimiwa naunga mkono maazimio yote na Inshaallah namuomba Mhe. Waziri twende vizuri, tutekeleza vizuri tuko pamoja naye naunga mkono ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwinyihaji sasa mchangiaji wetu wa mwisho katika hoja haii ni Mhe. Chum Kombo Khamis na baadaye Mhe. Waziri ajitayarishe kutoa maelezo ya hoja zilizofuatia.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kwa kunipa nafasi hii ili nichangie ripoti hii ambayo iko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa kuleta hoja hii lakini vile vile napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuleta majibu haya mbele yetu na sasa hivi yapo mbele yetu kwa ajili ya kuyachangia.

Mhe. Mwinyekiti, napenda niipongeze kwa dhati sana ripoti hii ambayo ina nia ya kujenga na lengo la dhati ya kusimamia udhalilishaji wa vijana wetu lakini pia kwa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imeeleza mambo mbali mbali yakiwemo maazimio lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema kwamba maazimio haya ya ripoti hii kilichobakia sasa yanahitaji utekelezaji ambao unasimamiwa na na sisi viongozi na wawakilishi lakini pia na wananchi wetu wanahitajika utekelezaji wa maazimio ya ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi bila ya kufuata mila na silka na tamaduni ya kizanzibari ripoti haiwezi kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu mimi ni mwanamke na uchungu wa mwana anaujua mzazi hasa mwanamke, sasa hivi kumekuwa na tabia ambazo tumekiuka mila na silka na desturi zetu kiasi ambacho inapelekea kutotekelezeka na kupelekea udhalilishaji. Niombe sana sisi wanawake na tukiwa ni wawakilishi wa wananchi hili tulisimamie kwa dhati kwani hapa

yametolewa maoni mengi tu, wachangiaji wengi waliopita wameomba sheria tubadilishe sawa, lakini sheria hizi ikiwa hatukuzisimamia hazitotekelezeka na wasimamizi ni sisi tuwasimamie na wananchi wetu tutekeleze sheria hizi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kama nilivyosema kumejitokeza tabia ambayo sio nzuri na haileti tija kwa wananchi wetu, lakini na kwa taifa pia. Sisi akina mama tumeondosha ule upendo wa dhati wa kuona kwamba mtoto wa mwenzako ni wako, leo hii tumepelekea kuondosha maadili yetu na kutojitambua kwamba nini maana ya udhalilishaji na wanaodhalilishwa ni akina nani. Nahisi kuna baadhi ya viongozi au baadhi ya wananchi wanahisi kwamba wanaodhalilishwa ni watoto wa kike tu. Lakini sasa hivi imeonekana kwamba udhalilishaji upo kwa watoto wa kiume mpaka vijana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi utamaduni tuliyouweka ni mbaya sana kwa mfano. Akina mama tunaandaa mashughuli ya harusi, leo utamkuta mwanamke mwenye uchungu, mzazi analiyekamilika na tunazaa watoto hawa tunachukua vijana wale wa kiume kwa mfano tunasema sijui kuna singo na nini tunawaweka pale watoto wa kiume ndiyo wanaoendesha shughuli ile, tunamuweka mtoto yule anakaa pale anacheza eti anamfunza mwari wa kike, ana mafunzo gani mtoto wa kiume akae amfundishe mwari wa kike. Huu siyo utamaduni na silka zetu. Kwa hivyo hii niwaombe sana viongozi wenzangu lakini akina mama katika jamii ambazo tunaziongoza hili ni suala ambalo halileti tija tunaondosha mila na silka, desturi, lakini kwa jamii pia hili halileti picha nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tumesema tusimamie sheria kwamba hizi sheria nazo pia zibadilishwe. Hizi sheria bila ya kuzisimamia hata zikibadilishwa kwa mwenendo kama huu tunaokwenda nao bado zitakuwa hazitekelezeki. Naomba nitoe mfano mzuri nimpongeze Mkurugenzi wa *ZBC* kuna vipindi vizuri tu vya watoto wetu ambao wameshafikia *stage* za kuowa au kuolewa kuna kipindi cha "Mwanakwetu" basi waangalie kile kipindi tuweke na tuweze kufatilia ili wapate mafunzo kupitia pale na sio kufanya singo, sijui *kitchen party* tunawaweka watoto wa kiume pale ule ni udhalilishaji, lazima tujue nini aina za udhalilishaji na nani anadhalilishwa, sio mtoto wa kike tu peke yake anayedhalilishwa.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze hilo tu kwa uchungu kabisa kama mwanamke sipendi kuona matukio kama yale kuna baadhi ya sisi viongozi tunalifanya lile, tunafanya shughuli zijui kuna *matenge party*, sijui nini tunawaweka watoto wa kiume, uchungu umepungua kidogo mtoto wa mwenzako ni wako, ikiwa mtoto yule ni wako awekwe kama vile utajisikiaje kama mzazi.

Niombe sana Mhe. Mwenyekiti, wanawake, tuwe na uchungu basi na hasa nyinyi wa baba na nyiye mkiona yale msikubali mzitetee shughuli zile mzikatae naomba sana hili. Tutaendelea kubadilisha sheria, tutaendelea kutunga sheria, hatima yake hazitotekelezeka kwa sababu sisi tunaotakiwa tuzisimamie sheria zile tunaozivunja. Kwa hivyo niwaombe sana akina mama wenzangu kwa masikitiko makubwa nimpongeze tu Mhe. Waziri anayeshughulikia Wizara hili nalo pia kama anavyosimamia vizuri na hili alisimamie tuone matendo haya hayaendelei na hayaonekani katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante mwisho naunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, Mhe. Chum sasa namwita Mhe. Waziri kuweza kutoa majumuisho Mhe. Waziri tafadhali karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa mara nyengine tena kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho kuhusu michango mbali mbali iliyochangiwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza niwatambue waheshimiwa Wajumbe waliochangia hoja nao ni kama hawa wafuatao:

1) Mhe. Asha Abdalla Mussa
2) Mhe. Ali Suleiman Ali
3) Mhe. Suleiman Makame Ali
4) Mhe. Simai Mohammed Said
5) Mhe. Suleiman Sarahan Said
6) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
7) Mhe. Mahmoud Thabit Kombo - Waziri wa Afya
8) Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini
9) Mhe. Naibu Waziri wa habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mheshimiwa tuwashukuru sana waheshimiwa kwa michango yao hii na niseme kwa ufupi sana kwamba michango yao hii ilikuwa na msingi mkubwa kwa kuyasikiliza lakini tumeelewa nataka niwahakikishie tutaifanyia kazi maana michango ambayo imekuwa na mwelekeo mkubwa kwa nia na dhamira ya kupambana na tatizo hili la udhalilishaji. Lakini kama walivyoeleza baadhi ya mawaziri walionitangulia katika kufafanua hoja hizi niseme na mimi kwamba Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa jamadari sana wa mapambano haya. Kwa hiyo, serikali yake wakati wowote itaendelea kuhakikisha kila hatua zinachukuliwa, kila gumu tuweze kulipatia majibu kwa msingi wa kufanikisha vizuri tatizo hili, ili tuondokane na suala zima la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa niaba ya serikali tunapokea pongezi zote za Waheshimiwa Wajumbe walizotupa kwa namna tulivyoshughulikia kwa pamoja jambo hili. Nataka niendelee kukwambia tu kwamba tutaendelea kushirikiana ili kulimaliza tatizo lililoko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wamesisitiza sana kuhusu kuharakisha suala hili la sheria la adhabu, nataka niwaambie waheshimiwa tutafanya hivyo kuhakikisha kwamba suala hili linapatiwa ufumbuzi kwa sababu ya kuharakisha sheria tuzifanyie marekebisho ili iendane na mazingira ambayo waheshimiwa mmeshauri.

Kuhusu suala la mwanafunzi aliyefariki katika skuli ya Laurent. Mheshimiwa jambo hili tayari limeshughulikiwa na wizara husika zote na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto wamekaa pamoja, wamelifatilia na ndio maana Polisi wakachukua hatua za kufanya uchunguzi na Wizara ya Elimu imefatilia kwa karibu sana kuhusu vibali vya skuli hii pamoja na kuendelea kufanya uchunguzi wa kina na baada ya uchunguzi huo hatua za kutolewa taarifa zitatolewa. Lakini kwa sasa Wizara ya Elimu imechukua hatua ya kuifunga ile skuli na kama alivyosema Waziri wa Afya kwamba imepelekwa timu maalum ya kuendelea kufanya uchunguzi nayo baada ya kukamilisha

uchunguzi wake serikali itatoa taarifa rasmi kila mmoja ataelewa jambo hili. Naomba tutoe nafasi wachunguzi wafanye kazi zao na taratibu nyengine zifate ili haki itendeke vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea kama nilivyosema awali kupambana na aina zote za rushwa na nia yetu ni kuendelea kutoa huduma bora, tutafanya hivyo kadri itakavyowezekana kufanya kutokana na hali halisi ya uwezo wetu wa kiuchumi. Lakini dhamira ya serikali ni kutoa huduma zote zikiwemo za kijamii na nyengine muhimu za maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kanda hizo *DVD* na kanda zisizostahiki, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe hatua zitaendelea kuchukuliwa kuhakikisha vitendo vyovyote vinavyoashiria kwenda kinyume na mila, desturi na silka zetu basi hatua zitachukuliwa ili vitendo hivyo visiendelee kutokea kwa nia ya kuendeleza udhalilishaji kwa kila hatua inayowezekana. Kila jambo au tendo ambalo linaashiria kuharibu utamaduni wetu hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba tunalinda na tunaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kesi kwa wale wanashirikishi kusuluhisha sheria nayo iharakishwe tutafanya hivyo tuhakikishe kwamba marekebisho yanafanyika ili jambo hili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa na wahusika waweze kukumbana na mkondo wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yalikuwa ni ushauri na mimi niseme ushauri huu tunaupokea kwenda kuufanyia kazi na kila linaloonekana tatizo tutalirekebisha na pale penye pengo la kisheria tutalijaza ili mambo yaende vizuri. Kwa ujumla nakubaliana na maneno ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kwamba tutakuwa na *action plan* ya utekelezaji ili kila jambo litekelezwe kwa wakati wake na kwa utaratibu mzuri ili mambo yafanyike vizuri. Nataka nikuhakikishieni kwamba utekelezaji utachukua nafasi yake ili sote turidhike na hatua zitakazochukuliwa katika kupambana na udhalilishaji.

Nawashukuru sana Waheshimiwa kwa ushauri wetu tutashirikiana kuondosha kadhia hiyo. Ahsanteni sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wa michango iliyotolewa. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na hoja ya Baraza la Wawakilishi ya uimarishaji na mfumo mzima wa kisheria unaohusiana na uendeshaji wa kesi za udhalilishaji kwa wanawake na watoto Zanzibar kama mmeupitisha naomba niwahoji wale wanaokubali, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nisimame kuwashukuru sana kwa muda wote ambao tumeendesha kikao hiki kwa utulivu na kwa michango yenu mizuri iliyotoka kuhusiana na hoja zilizoletwa mbele yetu taarifa za serikali na kukubali kuzipitisha pamoja na michango mizuri. Hadi hapa niseme kwamba ndio mwisho wa shughuli yetu ya leo na naliakhirisha Baraza hadi kesho mnamo saa 3:00 asubuhi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 23/06/2017 saa 3:00 asubuhi)